*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 2 Juni, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. JUMA SURURU JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 126

**Kuharibika kwa Pampu za Visima vya Maji Vijiji vya Biharamulo Magharibi**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA** aliuliza:-

Kuna baadhi ya maeneo vijijini mara pampu za maji zinapoharibika au kupata hitilafu husababisha Wananchi kukosa huduma ya maji safi na salama:-

(a)Je, mamlaka husika huwa zina utaratibu upi wa kusimamia matengenezo ya pampu hizo?

(b)Pale inapotokea pampu imeibiwa na mwizi akakamatwa na kushitakiwa na hatimaye kushinda kesi au kukosekana ushahidi; je, mamlaka inachukua jukumu gani la kuwasaidia Wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 324,377, kati yake ni 62% ndiyo wanaopata huduma ya maji. Aidha, Halmashauri ina jumla ya visima vifupi 446, visima virefu 82 na miradi ya mserereko saba na ile inayoendeshwa na nguvu za jua iko minne, yenye jumla ya vituo vya kuchotea maji 683, ambapo vituo 91 havifanyi kazi kwa sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu kwa kupata hitilafu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji ikiwemo visima vya maji, hukabidhiwa kwa jumuiya za watumiaji maji au Kamati ya Maji kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wake. Aidha, kwa mujibu wa Sera ya Maji, Kamati au Jumuiya inapaswa kuwa na Mfuko wa Maji kwa ajili ya uendeshaji wa matengenezo madogo madogo ya mifumo ya maji mara inapoharibika. Inapotokea kuharibika kwa pampu au hitilafu yoyote ile, Kamati ya Maji au Uongozi wa Kijiji husika hufanya matengenezo kupitia mafundi waliojengewa uwezo kutoka kwenye Serikali ya Kijiji. Endapo tatizo litakuwa juu ya uwezo, hutoa taarifa kwenye Halmashauri kwa msaada zaidi wa kiufundi au vifaa vya matengenezo vinavyohitajika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa pampu unapotokea, Uongozi wa Kijiji kupitia Jumuiya yake au Kamati yao ya Maji, hutoa taarifa za wizi kwenye Vyombo vya Kisheria kama Polisi kwa hatua za uchunguzi zaidi. Jukumu la kuwasaidia Wananchi ni la Halmashauri husika kama Wananchi wamekwama kutatua tatizo hilo kutegemeana na ukubwa wa tatizo lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri sasa ina jukumu la kununua pampu na vipuri kama Jumuiya au Kamati itakuwa haina uwezo; kwa mfano, katika Kijiji cha Mubaga, wizi wa pampu ulijitokeza na tayari Halmashauri imefunga pampu nyingine ili kuhakikisha huduma ya maji haikosekani katika maeneo hayo. Serikali inatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kupitia Jumuiya zake au Kamati zake za Watumiaji Maji, kuhakikisha miundombinu ya maji inalindwa wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mbassa, swali la nyongeza!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa sababu kuna maeneo ambayo wizi huu umefanyika na tayari wametoa taarifa Polisi na Wananchi wale hawana uwezo wa kununua au kupata pampu mpya. Je, Serikali kupitia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri; iko tayari kuwasaidia Wananchi wa Lukaragata A, Kituo cha Msasa, ambao pampu yao iliibiwa na wakatoa taarifa Polisi na mwizi akakamatwa lakini hatimaye akasinda kesi sambamba na Kijiji cha Mgera Kitongoji cha Nyangozi?

(ii) Kwa kuwa jukumu la kulinda hizi pampu ni la Wananchi na Wananchi wanapaswa kujengewa uwezo au kupewa mafunzo ya jinsi ya kuhimili matengenezo madogo madogo. Halmashauri au Serikali inatoa wito gani kwa wahusika wa Idara ya Maji kupita mara kwa mara na kukaa na hawa Wananchi ili kuwajengea uwezo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Antony G. Mbassa, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya msingi katika swali la msingi ambalo limetolewa.

La kwanza, kuhusu wizi wa pampu ambao amesema katika maeneo mbalimbali na kama alivyojibu Naibu Waziri kwamba, kuna Kijiji cha Mubaba pampu iliibiwa na Halmashauri ilifanya kila jitihada kuhakikisha Wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji na kupatiwa pampu.

Namwomba Mheshimiwa Antony Mbassa kwamba, tushirikiane naye na sisi tutashirikiana na Halmashauri kuweza kuwaelewa ni nini hasa juu ya hayo anayoyasema kuhusu wizi wa pampu. Tukithibitisha ni nia ya Serikali kuona kwamba, Wananchi hawa na Miradi hii ya Maji iliyojengwa, waendelee kupata huduma ya maji. Kwa hiyo, tutashirikiana kuona tatizo hilo tunalitatua.

Yeye kama Mheshimiwa Mbunge awe sehemu ya kuhamasisha Wananchi walinde miundombinu ya maji ikiwemo na hizo pampu.

Swali la pili, Miradi yote ya Maji inayoendelea kutekelezwa hapa nchini kabla haujakabidhiwa kwa Wananchi, mafunzo yanatolewa kwa Kamati za Maji na ndiyo maana zinakuwa na Mifuko ambayo zinajiendesha na matengenezo madogo madogo, lakini yapo pia mafunzo ya usimamizi na matengenezo. Kwa hiyo, wapo mafundi ambao wanapatikana vijijini na wanapewa mafunzo.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wanajumuiya wote wanaotumia maji kwamba, wataalamu wetu wataendelea kutoa mafunzo hayo ya usimamizi na matengenezo ili Miradi hii iweze kuwa endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Diana Chilolo nilikuona!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kupeleka maji mpaka vijijini; na kwa kuwa watu wengi wanahitaji kuingiza maji kwenye nyumba zao lakini mafundi bomba ni wachache; na kwa kuwa hata pampu zinapoharibika inachukua muda mrefu kutengenezwa kwa sababu ya upungufu wa mafundi bomba kwenye Halmashauri zetu:-

Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka mafundi bomba wa kutosha kwenye Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Mkoa wa Singida Iramba, Manyoni, Mkalama, Ikungi na nyinginezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza na Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba, upo upungufu wa watumishi na tunaendelea kukabiliana nao na kila mwaka tunaendelea kupata vibali na ninaamini kabisa hata mwaka huu bado tutaendelea kupata wataalamu hao. Kwa muda huu wataalamu wetu waliopo wilayani wanaendelea kutoa mafunzo kama nilivyosema, kwa Kamati za Maji, ili matengenezo madogo madogo yanapotokea ambayo hayahitaji sana kuwa na mafundi wakubwa basi waweze kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapokea ushauri wake na tutaendelea kuufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa ufafanuzi kuhusiana na Miradi ya Maji.

Kwa kuwa kuna baadhi ya Miradi ya Maji ambayo imekuwa ikifunguliwa, baada ya kuzinduliwa basi maji yale hayatoki tena. Natoa mfano huu kwa sababu kwenye Mji Mdogo wa Ilula tatizo kama hili liliwahi kutokea na Mradi huu ulifunguliwa na Makamu wa Rais ambaye sasa hivi ni Rais wa Zanzibar. Baada ya kuzindua Mradi ule mpaka leo maji hayajatoka!

Je, uwajibishaji hapo unakuwa ni kwa nani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Vyanzo vya maji vinatoka mahali mbalimbali kama chini ya ardhi, mserereko na Miradi hii inakuwa imesanifiwa. Inawezekana tu maji yaliyopo ardhini kwa wakati fulani yakawa yamepungua. Si kwamba, imekusudiwa kwa makusudi, mabadiliko ya tabianchi, hali ya maji ardhini na kadhalika. Kwa hiyo, haitokei kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahari nzuri nilikuwa Ilula na nilikuwa na Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wetu wa Kamati. Kwa hiyo, kwa Ilula, Miradi ambayo niliitembelea ilikuwa yote inafanya kazi.

Napokea Taarifa hiyo kama ambavyo naisema, basi na sisi tutaifanyia kazi, lakini si makusudio kwamba maji yamepimwa yapo halafu baada ya kuzinduliwa inawezekana ikawa mahitaji ya watu na maji yaliyopo yakawa machache, basi ikaonekana maji hayapo. Kama dosari hiyo ipo, sisi Wizara ya Maji tutaendelea kuifanyia kazi, lengo letu ni kuhakikisha Miradi hiyo kama ilivyokuwa imekusudiwa, Wananchi wanapata maji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali lingine linaekelezwa Wizara ya Ujenzi na litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini!

Na. 127

**Ahadi ya Kujenga kwa Lami Barabara ya Old Moshi**

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI** aliuliza:-

Je, Serikali itaanza lini utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Old Moshi katika Jimbo la Moshi Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Cyril August Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Old Moshi inaanzia Kiboriloni – Kiharara - Tsuduni hadi Kidia na ina urefu wa kilomita 10.8. Barabara hii inaendelea kufanyiwa usanifu wa kina na nyaraka za zabuni zinaandaliwa. Kazi ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2015. Baada ya kukamilika kazi hii, zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara zitaitishwa kwa lengo la kupata mkandarasi atakayejenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, jumla ya shilingi milioni 810 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chami swali la nyongeza!

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu lake zuri ambalo linakwenda kinyume kabisa na taarifa ya mwanasiasa mmoja aliyesimama hapa wakati anachangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kusema kwamba, Serikali imewadanganya Wananchi wa Old Moshi kwamba, itajenga barabara ile kwa kiwango cha lami. Amethibitisha kwamba, lami inajengwa na Wananchi waamini Kauli ya Serikali. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa vile barabara sasa imeshatoka kwenye mikono ya Halmashauri na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, fedha imeshatengwa kwa ajili ya kuanza kazi mbalimbali pale. Sasa hivi mvua inavyoendelea kunyesha inakuwa ni shida kwa Wananchi kuanzia Kidia kuja Tsuduni mpaka Kikarara kufika Mjini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaelekeza mamlaka zote zile iwe Halmashauri au *TANROADS* Kilimanjaro wapeleke moram katika maeneo korofi ya barabara ile wakati wanasubiri ujenzi kuanza rasmi?

(ii) Kwa vile barabara hiyo ni mojawapo ya ahadi za Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais ametoa ahadi za barabara nyingi Kilimajaro, zipo fupifupi lakini ni muhimu kwa Wananchi wa Kilimanjaro ukianza na ile ya Masama ambako anatoka Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Kibosho, Uru na Kawawa Nduoni kule Vunjo na barabara hizi hazijakamilika hadi sasa hivi na

Viongozi wa Vyama vya Upinzani wanapika kule kuwaambia Wananchi kwamba, barabara hizo hazitakamilika zitaisha baada ya Rais Kikwete kuondoka Ikulu:-

Je, Mheshimiwa Waziri atawahakikishia Wananchi wa Kilimanjaro kwamba barabara hizi zitaendelea kujengwa na kukamilika hata Rais ajaye atakapoingia kwenye madaraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Chami, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeze Mheshimiwa Dkt. Chami, kwa namna alivyokuwa anafuatilia utengenezaji wa barabara hizi ambazo ni ahadi ya Rais.

Naomba kusema kwamba, ahadi zote ambazo Rais ameahidi, kwanza, kuna barabara karibu tano katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini, ambazo zinaendelea kujengwa. Kwa sasa kwa sababu mvua bado inaendelea kuonyesha, kuna umuhimu wa kuzifanyia matengenezo. Barabara husika anayoisema iko chini ya Halmashauri, namwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri; pamoja na kwamba, *TANROAD* wataisimamia kuijenga barabara hii kwa matengenezo ya kawaida kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, wakatengeneza angalau hata kwa kutumia moram ili barabara iweze kupitika wakati tunasubiri kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Naomba kumthibitishia pia katika swali lake la pili kwamba, ahadi za Rais huyu ambaye tunaye Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, zile ambazo zitakuwa hazijakamilika, bado Rais mwingine ajaye ataendelea. Kwa hiyo, hakuna haja ya Wananchi wa Moshi Vijijini kuwa na wasiwasi, waendelee kuiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja linalohusiana na barabara ambalo linalingana na la mwulizaji aliyeuliza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ahadi hizo kuna barabara ya kutoka Njombe kwenda Lupembe, barabara ya kutoka Njombe kwenda Ludewa na barabara ya kutoka Njombe kupita Mdandu mpaka Igandu. Serikali ilitenga fedha mwaka wa 2014/2015; je, mpaka sasa ni barabara ngapi ambazo zimetangazwa kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu zilishatengewa bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, maarufu kama *Jah People,* kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nampongeza kwa kuuliza barabara ambazo na mimi natoka Mkoa ule. Barabara ya kutoka Njombe – Lupembe imeshafanyiwa usanifu na mwaka huu tumeweka kwenye bajeti fedha za kuanza kujenga kilomita 30. Barabara ya Njombe – Makete, imekamilika usanifu na mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kilomita 50. Barabara ya

Itone – Manda, tayari tumetangaza kuanza kujenga kilomita 50 katika barabara ile na usanifu unaendelea kwa sababu barabara yote ina urefu wa kilomita 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Barabara ya Njombe - Igandu, Barabara hii iko kwenye hatua ya usanifu na kazi hiyo bado inaendelea. Kwa hiyo, itakapokamilika tutafanya taratibu za kupata fedha tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Richard Ndassa!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza.

Wakati wa uzinduzi wa Daraja la Mto Simiyu, Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, alitoa ahadi ya kujenga ile *approach* mita 50 na mita 50 kwa kiwango cha lami; je, ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri mbele ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kama ni ahadi ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, maana yake ni kwamba, hili ni agizo kwa Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Mwanza, kuweza kufanya maandalizi ya kuanza kujenga. Hizi ni *approaches* kwenye daraja ambalo tayari limeshazinduliwa, kwa hiyo, ni lazima tukamilishe kazi ambayo tulishaianza kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, swali litaulizwa na Mheshimiwa Martha Moses Mlata. Hah, bado tuko ujenzi!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, umeruka swali langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkumba, samahani!

Na. 128

**Ujenzi wa Barabara za Tutuo – Bumba na Sikonge – Mibono – Kipili**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Barabara ya Tutuo – Ibumba kupitia Izimbili – Usoke na ile ya Sikonge – Mibono – Kipiri zilipandishwa hadhi kuwa Barabara za Mkoa:-

(a) Je, matengenezo makubwa ya barabara hizo hasa eneo la Mibono – Kipili ambalo halijatengenezwa kabisa yataanza lini?

(b) Je, Serikali inakubali kuwa Barabara ya Sikonge – Mibono – Kipiri inahitaji fedha nyingi hivyo itengewe fedha za kutosha bajeti ya mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Barabara ya Sikonge – Mibono – Kipili ipandishwe hadhi kutoka Barabara ya Wilaya na kuwa Barabara ya Mkoa katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Serikali imefanya jitihada kubwa kutenga fedha za kutosha ili kufungua sehemu ya barabara kati ya Sikonge na Mibono (Km 42). Hivi sasa sehemu ya barabara hiyo inapitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, sehemu ya Barabara ya Mibono – Kipili imetengewa jumla ya shilingi milioni 300, ambazo zitasaidia kufungua Barabara hii. Hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufungua Barabara hii hadi hapo itakapopitika majira yote ya mwaka kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkumba swali la nyongeza!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa barabara anayozungumza ina kilomita karibu 192, inayotoka Sikonge kuelekea Mibono na Kipili, na eneo analolizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba limefunguliwa, halijafunguliwa kwa sababu hili eneo lilikuwepo wakati wa Halmashauri, kilomita hizo 42.

Nataka kujua zile kilomita 144 ambazo ni pori, kwa miaka mitano tangu kupandishwa hadhi hazijafanyiwa kazi kabisa na hata hizi shilingi milioni 300 anazosema inawezekana zimetengwa lakini hazina uhakika wa kufika:-

Je, ni lini sasa hizo kilomita 144 zitafanyiwa kazi ya kufunguliwa ili barabara hii iweze kupitika kutoka Sikonge – Mibono – Kipili?

(ii) Wakati Mheshimiwa Dkt. Mahanga akiwa Naibu Waziri, aliitembelea hiyo barabara yote; na kwa kuwa majibu aliyonijibu Mheshimiwa Naibu Waziri yanaonesha ni jinsi gani basi Wizara haifahamu kinachoendelea kule:-

Je, ni lini Naibu Waziri au Waziri mwenyewe atakuja kuona hali halisi ya barabara hiyo kama alivyofanya Mheshimniwa Dkt. Makongoro Mahanga kipindi kile?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, Wananchi wa Tabora ni lazima waishukuru Serikali kwa kukubali kupandisha hadhi barabara ambayo haipo. Barabara hiyo ni pori *(is non-existence)*, kwa hiyo, Serikali inaanza kuifungua upya; na ndiyo maana nimesema kwenye jibu la msingi kwamba, tayari tumeshafungua kilomita 42 na kila mwaka tutakuwa tunaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Isingewezekana bajeti yote ya barabara ya Mkoa wa Tabora tuipeleke kwenye barabara moja. Kwa hiyo, tutaenda kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya kila jitihada twende tukaione kazi ambayo tayari Serikali imeshafanya ili tuone namna ya kuongeza kasi kwa sehemu ambayo imebaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Medeye, swali la nyongeza!

**MHE. GOODLUCK J. OLE–MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mwezi Novemba 2012, Rais alipokuwa kwenye Sherehe za Uzinduzi wa Chuo cha Nelson Mandela, alimwagiza Waziri wa Ujenzi kwamba, ajenge barabara ya lami kutoka Kijenge Arusha hadi Chuo cha Nelson Mandela. Sijui ni lini kazi hiyo ya ujenzi wa barabara kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais itafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ole-Medeye, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kuikamilisha na Serikali ilishaanza kufanya kazi ile kwa awamu, nimhakikishie kwamba, tutafanya kila kinachowezekana tuweze kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Tunaenda swali linalofuata, Wizara ya Viwanda na Biashara, litaulizwa na Mheshimiwa Martha Moses Mlata; Mheshimiwa Mshama kwa niaba ya Mheshimiwa Martha!

Na. 129

**Usambazaji wa Kazi za Wasanii**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA (K.n.y. MHE. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Wizi wa kazi za Wasanii bado ni tatizo sugu nchini:-

(a) Je, ni lini Serikali italeta Muswada Bungeni utakaobadilisha Sheria ya *COSOTA* ambayo imepitwa na wakati?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa kwa kutowashirikisha *TRA* katika usambazaji wa kazi za Wasanii inapoteza mapato mengi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya kurekebisha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999 yameanza. Wizara yangu kwa kushirikiana na *COSOTA* na *Rulu Arts Promoters,* ambalo ni Shirika lisilo la Kiserikali *(NGO),* lililoanzisha mchakato wa kukusanya maoni ya wadau kwa ufadhili wa *Best AC*. Rasimu ya kwanza imeshaandaliwa baada ya kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau wapatao 22 kutoka katika Ofisi za Serikali na taasisi binafsi zikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Ofisi ya Mwendesha Mashitaka, Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mawakili wa Serikali, Waigizaji, Wachapishaji, Mawakala wa Kujitegemea na Mapromota. Aidha, Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa ili kupata maamuzi ya Serikali na pindi hatua hiyo itakapokamilika, Muswada husika utawasilishwa Bungeni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuishirikisha *TRA* kikamilifu kwenye usambazaji na uuzaji wa kazi za wasanii unaofanywa na Wakala wao, Mapromota na Wasanii wenyewe ili kudhibiti mapato ya Serikali. Wizara yangu kupitia *COSOTA* inashirikiana na *TRA,* ambaye ni mjumbe kwenye Kamati ya Urasimishaji pamoja na Taasisi za Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu. Kamati pia inashiriki kutoa semina elekezi kuhusiana na masuala ya ulindaji wa kazi za muziki na filamu nchini; kuandaa na kufanya operesheni za

pamoja dhidi ya uharamia wa kazi za muziki na filamu nchini; kutoa *Copy Right Clearance Certificate* kwa mmiliki wa kazi kabla ya kupewa stempu ya kodi na *TRA*.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninapenda nimwulize Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

(i) Tangu nimekuja hapa Bungeni Mheshimiwa Mlata ameuliza swali hili zaidi ya mara tano na kila mara tumekuwa tukipata majibu yanayokaribia kufanana kwamba, vinaandaliwa na wanakaribia. Je, wale waliokamatwa na kazi za Wasanii wamefanywa nini?

(ii) Hivi tunavyoongea huko mitaani kazi za Wasanii zimesambaa na zinauzwa, *especially* kule Kigamboni kila Alhamisi kunakuwa na mnada wa kuuza *CD* na *DVD* kwa shilingi 1000 au 1500. Hali hii ikiachwa Wasanii wetu watakuwa maskini na hawataweza kuongeza kipato na kuwa kama wasanii wa mataifa mengine. Je, ni lini Muswada huo utaletwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda ku-*declare interest* kwamba, watoto wangu ni wasanii na wana kazi zao nyumbani, hawazipeleki hata dukani kwa sababu hakuna faida yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu maswali sijui ni mawili au moja la nyongeza la Mheshimiwa Mshama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Martha Mlata, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika kufuatilia masuala haya ya wasanii na kwa kiasi kikubwa ameweza hata ku-*influence* mambo mengi ambayo Serikali imeyafanya katika kuboresha mapato na kazi za Wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda niongezee kuwa, Mheshimiwa Martha Mlata, amekuwa akileta hoja mbalimbali, siyo hii hii moja kila siku. Kila hoja anayoileta *of course* inahusiana na mambo ya wasanii, lakini inajibiwa na inafanyiwa kazi. Hata hii aliyoileta sasa hivi ya suala la Muswada, Muswada utaletwa mara tu utakapokuwa umepitishwa na Baraza la Mawaziri. Siwezi kusema ni lini *exactly*, lakini unafanyiwa kazi na hatua ambayo tumefikia ni mwendelezo wa kazi ambayo imekuwa ikifanyika tangu suala hili lianze kuuliziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kazi za wasanii ambazo zimezagaa, ni kweli kuwa mpaka sasa hivi bado *control* haijawa ya kutosha, lakini tangu urasimishaji wa kazi za sanaa ulipoanza hadi kufikia Mei 2015, *CD* na *DVD* zilizokamatwa ni 30,984 kwa kazi za ndani na 35,166 kwa kazi za nje. Aidha, stempu zilizotolewa na *TRA* tangu urasimishaji wa sanaa uanze ni 4,570,000 kwa muziki na 18,420,000 kwa filamu, ambapo huko nyuma taarifa kama hizi zilikuwa haziwezi kupatikana. Kwa hiyo, yameshafanyika mambo mengi na hata hivi ninavyozungumza, tayari kuna *tender* itakayotangazwa kwa ajili sasa ya kutafuta mtaalam atakayetengeneza Programu ya Kompyuta itakayoweza kunasa kazi za wasanii zinazotumika kwenye Redio, TV na matangazo ya Simu ili kila siku tuweze kuwa tunapata taarifa ni kazi za nani zimetumika kwa kiasi gani na ni kiasi gani cha fedha msanii huyo anapaswa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni hatua ambayo tumeipiga kwa kiwango kikubwa sana. Tumefika mahali sasa tutaweza, hata hivi ninavyozungumza, tunaweza kujua ni nani ametumia kazi za nani kwa siku moja kila siku. Tunangojea tu sasa utaratibu wa kukubaliana jinsi ya kulipana na nani atakayekusanya hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli hatua imefanywa, siyo kwamba tunajibu maswali yale yale kila siku.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaenda swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi!

Na. 130

**Mafao kwa Waliokuwa Wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi – Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Waliokuwa Wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi Wilayani Muheza walishinda kesi na kutakiwa walipwe mafao yao ambapo *PSRC* ilikabidhiwa jukumu la kusimamia shamba hilo na kuahidi kusaidia kulipa; na *CHC* ilipochukua jukumu toka *PSRC* iliahidi kusaidia kulipa lakini mpaka sasa hakuna malipo na shamba limekabidhiwa Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kutosimamia malipo ya mafao hayo kutolewa ni kudharau maamuzi ya Mahakama?

(b) Kwa kuwa Serikali ndiyo iliyowatafuta wawekezaji wa shamba hilo na kuahidi kuwafuatilia hata nje ya nchi kushindwa; je, kwa nini Serikali isichukue jukumu la kuwalipa Wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili linafanana na Swali Na. 43, lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge huyo kuhusu mafao ya Wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi lililojibiwa tarehe 14 Juni 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali hilo kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imekuwa ikifanya jitihada za kusaidia kumtafuta aliyekuwa mwekezaji wa mashamba hayo, Mercantile Freighters ya nchini Kenya na Jumaan Muhsin El-Ardhi ya Tanzania, kwa kushirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Interpol, ili kuhakikisha kuwa, wanakamatwa na kushitakiwa hapa nchini kwa kukaidi amri ya Mahakama ambayo ilikwishatoa haki kwa wafanyakazi wa mashamba hayo baada ya kesi kuendeshwa kwa muda mrefu. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuwasiliana na Ubalozi wetu wa nchini Kenya kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ili kuwafuatilia waliokuwa wamiliki wa Kampuni ya Mercantile Freighters ya nchini Kenya na Jumaan Muhsin El-Ardhi ya Tanzania, ambapo ilibainika kuwa kampuni hizo zimeshafilisika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na *NDC,* hadi sasa haijakabidhiwa jukumu la kulipa mafao hayo. Aidha, mwezi Mei 2009, *NDC* ilipokabidhiwa rasmi shamba hilo, kulikuwa na deni la shilingi 12,600,000 ikiwa ni mishahara ya miezi mitatu (Machi,

Aprili na Mei 2009), kwa wafanyakazi waliobaki kwa ajili ya usimamizi wa shamba na hao wote walilipwa na *NDC*.

Wizara yangu inafanya jitihada za kuwasaidia wafanyakazi hawa kupata haki zao kutoka kwa waliokuwa waajiri wao, ambapo imekuwa ikiwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje kama ambavyo nimeshaelezea hapo awali na bado tunaendelea na juhudi hizi. Kwa ule muda ambao *NDC* imewachukua wafanyakazi hawa, tahari wamekuwa wakilipwa kama kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Herbert Mntangi, swali la nyongeza!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali ya nyongeza yafuatayo:-

(i) Mgogoro huu ni wa muda mrefu sana, ni zaidi ya miaka 15 na Wananchi hao bado hawajapata haki zao. Jitihada za kuwatafuta wahusika inaonekana zimeshindikana. Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ndiyo inayosimamia Taasisi ya *NDC* inangoja kupata maelekezo ya kuchukua jukumu la kuwalipa wafanyakazi hao kutoka kwa nani, wakati Wizara ni sehemu ya Serikali na Serikali ndiyo iliwatafuta wawekezaji hao? *(Makofi)*

(ii) Huyu mwekezaji ambaye anaendesha shamba hilo hivi sasa naye vilevile ana mgogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, hataki kulipa kodi stahili anazotakiwa kulipa:-

Je, Wizara inayohusika inafahamu juu ya mgogoro huo na kama hawafahamu wako tayari kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili kusuluhisha mgogoro huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli huu mgogoro ni muda mrefu na ulitolewa maamuzi Mahakamani kuwa, waajiri wawalipe wafanyakazi wao. *NDC* wamekuja kuchukua Mradi huo muda mrefu baadaye. Kwa kuwa hili jambo lilikuwa Mahakamani, kwa vyovyote vile itakuwa rahisi zaidi Wafanyakazi wakarudi tena Mahakamani ili waweze kukazia ile hukumu. Kama Mahakama itaona inafaa, wao ndiyo watakaoamua hatima ni vipi hawa watu walipwe baada ya kugundua kuwa wale wahusika wote wamefilisiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili ni kuwa, kwa kadiri ya uelewa wangu, sina taarifa kuwa kuna mgogoro kati ya Halmashauri na *NDC,* lakini niko tayari kwenda kufuatilia na kujua ni jinsi gani tutakavyoweza kutatua mgogoro huo.

**MWENYEKITI:** Tunaenda Wizara inayofuata, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, swali litaulizwa na Mheshimiwa Aliko Kibona, Mbunge wa Ileje!

Na.131

**Wakala wa Hifadhi ya Chakula Kutokulipa Ushuru**

**MHE. ALIKO N. KIBONA** aliuliza:-

Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa wamenunua mahindi Wilayani Ileje kupitia Soko la Isongele bila kulipa ushuru zaidi ya shilingi milioni mia mbili:-

Je, ni lini Serikali italipa ushuru huo ambao ni muhimu kwa uendeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ambayo haina wigo mpana wa vyanzo vingine vya mapato?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu! *(Makofi)*

Hayo makofi ameyapokea ameyaelewa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Jimbo la Ileje, kama ifuatavyo:-

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kupitia ununuzi wa nafaka nchini, umekuwa ukidaiwa ushuru wa mazao kutokana na ununuzi wa nafaka kutoka kwa wakulima katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya nchini, ikiwemo Halmashauri nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje.

Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, inatambua madeni ya ushuru wa mazao inayodaiwa na Halmashauri za Wilaya nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ya jumla ya shilingi 10,830,788,567.50 kwa misimu ya mwaka 2011/2012, 2012/2013, 2013/2014 na 2014/2015. Aidha, katika kushughulikia ulipaji wa madeni hayo, jumla ya shilingi 1,429,501,507.50 zimelipwa kwa Halmashauri za Wilaya nchini katika mwezi Aprili mwaka 2015, ambapo shilingi 72,812,337.50 zimelipwa kwa Halmashauri ya Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa mapato yatokanayo na ushuru wa mazao katika utekelezaji wa mipango ya majukumu ya Halmashauri za Wilaya nchini, *NFRA* itaendelea kulipa ushuru wa mazao kwa Halmashauri itakayonunua nafaka kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, imepanga kulipa madeni yote ya ushuru wa mazao kwa Halmashauri zote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kiasi kilichokuwa kikidaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni shilingi 200,000,000 na kwa majibu ya Serikali ni kwamba, zimelipwa shilingi 72,000,000, bado shilingi 127,000,000. Fedha ambayo ni nyingi sana kwa Uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Ningependa kufahamu ni lini Serikali italipa pesa hii maana msimu mpya sasa unakaribia?

(ii) Wakulima na Watawala wa Dola kwa ngazi ya Halmashauri na Mikoa kote nchini ambako wakulima walikopa mazao, wamepata tabu sana msimu uliopita katika mkanganyiko uliojitokeza kulipa madeni ya wakulima. Ningependa kujua msimu mpya ndiyo huu uko mlangoni; Serikali inatoa kauli gani kwa maandalizi ya msimu mpya ujao wa kilimo maana sasa hivi wakulima wameanza kuvuna mazao mengine na wanahitaji mbolea na vitu vingine?

Ningependa Serikali itupe majibu kwa kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Kweli Halmashauri ile imelipwa shilingi 72,000,000 na bado inadai 127,000,000 na kama nilivyosema katika jibu la msingi, tumeweka katika bajeti fedha za kutosha kulipa madeni yote ya Halmashauri zote nchini. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Ileje italipwa vilevile katika bajeti inayokuja ambayo ni mwezi mmoja hivi kuanzia sasa tunaanza bajeti mpya.

Kuhusu ununuzi wa mazao, Serikali imejipanga kupitia *NRFA* pamoja na Shirika la Nafaka na Mazao Mchanganyiko kuanza ununuzi wa mazao ya wakulima mwezi Julai. Vilevile itashirikisha Sekta Binafsi kwa sababu ni vigumu Serikali kununua mahindi au mazao haya yote peke yake.

Serikali inakusudia kusimamia na kuhakikisha ununuzi unafanyika na kwamba, hakutakuwa na mpango wa kuwakopa wakulima tena. Fedha zinazodaiwa na wakulima kwa madeni yaliyotokana na wao kupeleka mazao, sasa imebakia shilingi bilioni 12 na zitalipwa kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika.

**MWENYEKITI:** Tunaenda Wizara inayofuata, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali litaulizwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda!

Na. 132

**Kukipatia Umeme Kituo cha Polisi cha Ihanja**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Tarafa ya Ihanga Wilaya ya Ikungi ni cha muda mrefu na kinahudumia Wananchi wa Tarafa nzima:-

Je, ni lini Serikali itakipatia umeme kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujajibu tunakupongeza kwa kutanganza nia. Sasa ninakukaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, Kituo cha Polisi Ihanja kinatoa huduma kwa Wananchi wa Tarafa nzima na kwamba, kupatikana kwa huduma ya umeme kutaongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Ihanja Tarafa ya Ihanja, kipo mbali umbali wa takribani kilomita 50 kutoka kwenye njia ya umeme. Hii ni changamoto kubwa kibajeti ambayo imechangia zoezi la kupeleka umeme kuchelewa. Hata hivyo, pamoja na ufinyu wa Bajeti, Serikali inakusudia kuweka umeme kwenye Kituo hicho katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Aidha, chini ya Mradi wa Umeme Vijijini *(REA)*, ni imani yangu kuwa, Kituo hiki kitapewa kipaumbele cha kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kumwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na aendelee kushirikiana na Serikali kwa kuhamasisha

Wananchi katika shughuli za maendeleo kama vile kuchangia gharama za kuweka umeme hapo kituoni.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Naomba nikiri wazi kama kuna siku imekuwa *upset* basi ni leo. Haya majibu ya Serikali ni ya uongo kabisa, hayana ukweli wowote.

(i) Ninataka kujua ni utafiti gani huu umefanywa na watendaji kwenye Wizara hii kujua kwamba Kituo cha Polisi cha Ihanja kiko zaidi ya kilomita 50 toka njia kuu ya upatikanaji wa umeme; ilhali kuna Kanisa la Kilutheri pale hazifiki hata mita kumi wana umeme na majirani wanaozunguka pale Kituo cha Polisi wana umeme? Leo Serikali inasema ni kilomita 50 kutoka njia a upatikanaji wa umeme; ninaomba mniambie utafiti huu umefanywa na Watafiti gani kudanganya Bunge hapa na Wananchi wa Ihanja wanawasikia? Hilo ni swali la kwanza.

(ii) Naibu Waziri amejibu kwamba, mimi Mbunge nivute subira na niendelee kuhamasisha Wananchi kuchangia gharama za kuweka umeme ilhali hiii ni kazi ya Serikali! Wananchi hawa wa Tarafa ya Ihanja wanachangia zahanati, wanachangia madawati, wanachangia shule, wanachagia maabara na kila kitu pamoja na maji wanakosa.

Niseme Tarafa hii ya Ihanja iko katika Jimbo la Singida Magharibi lililoongozwa na Mbunge wa CCM kwa miaka 15. Mnataka kuniambia Mbunge huyu ameshindwa kuhamasisha Wananchi kuchangia kwa miaka 15 ili waweke umeme hapa leo tuhamasishe Wananchi kuchangia? *(Makofi)*

Ninataka majibu ya Serikali kama siyo kugombanisha watu.

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikiri kwamba, mimi ni mgeni sana Singida, ndiko ninakotoka ninapafahamu. Ieleweke na Mbunge atambue kwamba, Kituo kile cha Polisi siyo jengo la Serikali, ni jengo la mtu binafsi. Kwa hiyo, Serikali ina mpango wa kujenga jengo la polisi na pia ndiyo inapanga mpango wa kupeleka umeme.

Swali la pili, ninatambua yeye mwenyewe Christowaja ni mdau mkubwa wa kuchangia shughuli za maendeleo, hapa tupo katika kuhamasishana kukumbushana. Hatujasema hakuna Mbunge aliyeko pale ambaye hachangii maendeleo, Serikali muda wote tuko hapa tunawahamasisha Wabunge kuchangia shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, hata pale Serikali inapotenga bajeti ya kujenga Kituo cha Polisi au kuweka umeme ni wajibu wa Wananchi pia kuchangia shughuli za maendeleo. Mheshimiwa Christowaja kama Mbunge, ninatambua amekuwa akichangia, basi katika hili tutakapofikia tushirikiane na Serikali, lakini kama kuna mambo mengine yoyote yale, yeye awe karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tuweze kumaliza tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara inayofuata, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; swali linaulizwa na Mheshimiwa Rukia Kassim!

Na. 133

**NHC Kulazimisha Wanunuzi wa Nyumba Kukopa Benki**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS (K.n.y. MHE. RUKIA KASSIM AHMED)** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* hulazimisha Watumishi wanaotaka kununua nyumba za Shirika wakope Benki badala ya kukatwa kwenye mishahara yao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo huongeza gharama zaidi ya 50% na kuzifanya nyumba hizi zisinunulike?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Kwenye miaka ya 1960 na 1970 Shirika la Nyumba la Taifa lilikuwa na utaratibu wa kuwakopesha mikopo ya ununuzi wa nyumba Wananchi kama wapangaji au *Ternant Purchase Scheme,* kwa kuwa shirika la Nyumba lilikuwa likipokea ruzuku kutoka Serikalini. Mikopo hiyo ilikuwa inatozwa riba na kuanzia katikati ya miaka ya 1970, utaratibu huu ulisitishwa kutokana na hali ngumu ya uchumi hususan mfumuko mkubwa wa bei na riba kubwa ya mikopo ya ujenzi iliyokuwa ikitozwa na benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Shirika la Nyumba hukopa mitaji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa masharti ya urejeshaji wa muda wa kati ya miaka saba hadi kumi na riba ya wastani ya 15% kwa mwaka. Kutokana na ukweli huu, Shirika la Nyumba la Taifa kwa sasa halina uwezo wa kuwakopesha wanunuzi wa nyumba zake kwa kuwakata mishahara yao moja kwa moja ili walipe kwa kipindi cha muda mrefu. Vinginevyo, Shirika litashindwa kujiendesha na kujenga nyumba zingine zaidi ili kuwafikia Wananchi wengi zaidi.

Shirika la Nyumba la Taifa haliwalazimishi wanunuzi wa nyumba zake kuchukua mikopo ya Benki. Ukweli ni kwamba, Shirika la Nyumba la Taifa limeingia mikataba na benki 15 kwa ajili ya kuwapatia wanunuzi wa nyumba zake mikopo. Wanunuzi wanayo hiari ya kukopa kwenye benki hizi 15 ambazo *National Housing* imeingia mkataba na benki nyinginezo ambazo hazina mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa. Vinginevyo, mnunuzi anaweza kulipia nyumba anazotaka kuzinunua bila kukopa benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, mikopo huongeza gharama kwa wakopaji, lakini hata hivyo manufaa ambayo hupatikana kutokana na mikopo ya nyumba ni makubwa ikilinganishwa na gharama za kukopa. Ninapenda kusisitiza kwamba, utaratibu wa kukopa kwa ajili ya ununuzi wa nyumba au kitu chochote kile ni utaratibu wa kawaida ambao hutumika katika nchi zingine zilizoendelea na zinazoendelea. Ninapenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Wananchi kwamba, wasiogope kukopa ili waweze kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Shirika haliwalazimishi wanunuzi wake kukopa benki bali Shirika limeingia mikataba na mabenki kwa ajili ya kuwapatia wanunuzi mikopo. Je, ni kwa nini Shirika hili linauza nyumba zake kwa bei ya juu sana hasa zile za ghorofa ambazo zinaitwa *medium cost;* mfano mzuri ni nyumba zilizojengwa Mchikichini - Ilala Dar es Salaam, gharama ya kujenga *appartment* moja ya vyumba vitatu ni shilingi milioni 60 lakini zinauzwa kwa shilingi milioni 200? Je, kuna nia kweli ya kuwasaidia Wananchi kupata makazi bora?

(ii) Kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuwasaidia Wananchi wake kupata makazi bora; na Mheshimiwa Rais anayestaafu mwaka huu tukijaaliwa alitoa kauli kwamba watu au Wananchi wanaoishi katika nyumba za Serikali au za Shirika la Nyumba, zile ambazo zilijengwa kwa misaada na wajomba zetu wafadhili, watauziwa nyumba zile. Je, ni kwa nini siku zote Serikali inakuwa na kigugumizi cha kuwauzia watu hawa nyumba hizi ambao wamelitumikia Taifa hili na sasa wamekuwa wazee wastaafu; badala yake kila siku Shirika hili linaongeza kodi nyumba zile badala ya kuzipunguza mfano ni nyumba za Ilala - Dar es Salaam maghorofani?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza alitaka kujua ni kwa nini *National Housing* inauza nyumba zake kwa gharama kubwa na pili ameelezea nyumba hizo ni takribani shilingi milioni 200 wakati wamejenga kwa milioni 60. Kwanza, ninaomba niweke rekodi sahihi; kwa nyumba za Mchikichini, nyumba za vyumba vitatu bei yake bila *VAT* ni shilingi 168,239,749 na *VAT* ni 30,283,155 na jumla kuu ukiweka *VAT* na gharama halisi ni 198,522,903.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nyumba zetu za *National Housing* kwa mfano Kibada, nyumba ni milioni 45.5 bila *VAT*. Ukiangalia Ubungo zipo nyumba ambazo tumeziuza kwa milioni 39 bila *VAT*. Kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama nilivyoeleza ktika jibu la msingi katika swali la Mheshimiwa Rukia, Shirika la Nyumba la Taifa mtaji wake siyo mkubwa hivyo. Lazima na zenyewe ili ziweze kujenga nyumba nyingi za kuuza kwa gharama nafuu zinahitajika nazo kukopa kwa mkopo wa miaka saba mpaka miaka kumi kwa riba ya 15%, bado hujaweka vifaa vya ujenzi na gharama nyingine za kodi ya ongezeko la thamani. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tunayo nia ya dhati ya kuhakikisha tunapunguza gharama hizi. Hivi sasa tayari tumeanza kuchukua hatua, tumewaelekeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa kushirikiana na Wakala wetu wa Utafiti wa Nyumba na Ujenzi, kuangalia namna bora kwa kutumia vifaa mbalimbali vya ujenzi kama ujenzi wa kuta na paa mbalimbali, kuona ni kwa namna gani gharama hizi zinaweza kupungua. Vilevile kwa kuangalia uzoefu wa Watanzania wa kawaida, familia ya kawaida ambayo inaishi kwa pato la kawaida la chini la Taifa la milioni 3.8, ukichukua familia ya watu watano pato lao ni milioni 37, endapo watalipa kwa mkopo wa miaka 25, watatakiwa kukopeshwa milioni 37 tu. Kwa hiyo, tumeanza kulifanyia kazi kwa kuwaelekeza *National Housing* kwa kuangalia ni kwa namna gani sasa mikopo yake ikiwezekana nyumba za gharama nafuu ziwe kwenye milioni 25 na ikizidi sana milioni 35.

Swali la pili alitaka kujua kauli ya Mheshimiwa Rais kuhusiana nyumba mbalimbali ambazo *National Housing* walizijenga na ametoa mifano ya babu zetu na bibi zetu. Nilishajibu wiki iliyopita katika swali la Mheshimiwa Sanya, aliuliza Mheshimiwa Abas Mtemvu swali la nyongeza hususan katika nyumba za kwa Akina Mama Mfuko, Keko na Chang'ombe. Nililieleza hili, bado Shirika linahitaji mtaji, lakini sisi kama Wizara tumewaelekeza *National Housing* kwanza kuangalia tunaweza kulifanyiaje kazi hili na endapo linawerzekana au haliwezekani. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira, tutaendelea na taratibu hizi za mashauriano endapo litawezekana tutatoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda hauko na sisi, tunaenda Wizara ya Maji, swali litaulizwa na Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini; Mheshimiwa Leticia Nyerere kwa niaba yake!

Na. 134

**Serikali Kutolipa Madeni ya Huduma za Maji**

**MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. VINCENT J. NYERERE)** aliuliza:-

Mamlaka za maji mijini zinaendeshwa kwa shida sana kutokana na ukweli kwamba Serikali hailipi madeni ya huduma wanayopewa na mamlaka hizo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa ruzuku kwa mamlaka hizo ikiwemo MUWASA ili ziweze kujiendesha na kupunguza mzigo kwa Wananchi?

(b) Je, ni sawa Wizara na Idara za Serikali kama vile JWTZ, Polisi, Ikulu (Nyumba za Wakuu wa Mikoa) kukatiwa maji kwa kushindwa kulipia huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianzisha Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira nchini ambazo ziko katika madaraja matatu; A, B, na C. Mamlaka Daraja A ni zile ambazo zinajitegemea kwa gharama zote za uendeshaji na matengenezo, ikiwemo mishahara ya Watumishi na gharama za umeme wa kuendesha mitambo ya kusukuma maji na sehemu ya uwekezaji. Mamlaka za Daraja B ni zile ambazo bado zinapata ruzuku ya kulipia sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo. Mamlaka za Daraja C ni zile ambazo bado zinapata ruzuku ya mishahara ya wafanyakazi wake pamoja na kulipa sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo na gharama za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma iko Daraja A na kwa msingi huo, haistahili kupata ruzuku ya Serikali, isipokuwa Serikali inatekeleza uwekezaji wa Miradi mbalimbali kwa ukarabati, kupanua na ujenzi wa Miradi mipya mikubwa kama vile Mradi unaojengwa hivi sasa katika Mji wa Musoma, unaolenga kuondoa tatizo la maji kwa Wakazi wa Miji ya Musoma na Wakazi wa Vijiji vya jirani.

**NAIBU WAZIRI MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali bado inaendelea kutoa ruzuku kwa mamlaka zilizo daraja ‘B’ na ‘C’ pamoja na miradi ya kitaifa kwa kulipia mishahara, sehemu za gharama za umeme na madawa kulingana na mkataba wa makubaliano, uliosainiwa kati ya mamlaka hizo na Wizara zikionyesha majukumu ya Serikali kwa kila mamlaka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Taasisi zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge na nyingine ni miongoni mwa wadaiwa wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Wizara inatambua kwamba Taasisi hizi ni za Serikali, zikiwemo hospitali ambazo zinatoa huduma kwa wagonjwa na zinahitaji huduma hiyo; siyo vyema kusitisha huduma. Aidha, tunawasiliana na Hazina ili kuweka utaratibu wa kulipia Taasisi hizi madeni yake moja kwa moja kutoka Hazina katika mafungu yake ili kuzijiengea uwezo mamlaka hizi kuendelea kutoa huduma bora na endelevu. Hii itapunguza uwezekano wa kubebesha wananchi mzigo wa kulipia huduma hizi.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu. Tupunguze kelele!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nimtaarifu Mheshimiwa Waziri kwamba Mheshimiwa Mbunge anaitwa Vincent Josephat Nyerere na Siyo Vicent Joseph Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ingawa yamekuwa *too advanced.* Umetoa majibu zaidi ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RPC* anadaiwa Shilingi milioni 102, Jeshi la Wananchi wa Tanzania linadaiwa Shilingi milioni nane, *RAS* anadaiwa, hospitali ya Mkoa inadaiwa. Sasa swali, ni kwanini Serikali haiingilii kati kuhakikisha kwamba madeni haya yanalipwa ili kuwawesha MUWASA kufanya kazi yao kikamilifu kwa mafanikio?

Swali la pili, pamoja na kwamba Musoma imewekwa katika daraja 'A', kwa maana ya kwamba ina uwezo wa kujitegemea kuendesha MUWASA na kusimamia shughuli za maji; lakini inapotokea kwamba Taasisi hizi za Serikali zinashindwa kulipa: Kwanini sasa Serikali isiingilie kati na kuwanusuru hawa watu kwa kulipa madeni badala ya kuendeleza miradi au kuanzisha miradi mipya ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi!

**NAIBU WAZIRI MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyojibu katika swali la msingi, tunatambua uwepo wa madeni haya. Hapa nilipo nina takwimu sahihi; nimwambie kwamba hata takwimu alizozitoa yeye siyo sahihi, lakini mimi ninazo hapa, akitaka naweza nikampa kwamba Jeshi la Wananchi linadaiwa Shilingi milioni 2.4, hospitali inadaiwa Shilingi milioni 113 na wadeni wengine wengine. Jumla ya madeni yote wanaodai Mamlaka ile ni Shilingi milioni 390.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika nchi nzima, mamlaka zote kwa ujumla zinaidai Taasisi za Serikali Shilingi bilioni 20. Kwa hiyo, ndiyo maana katika majibu ya msingi tulisema sisi Wizara ya Maji tutashirikiana na Wizara ya Fedha kuona kwamba madeni haya yanalipwa ili mamlaka hizi ziweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, tunatambua. Lakini upo unyeti, kwa mfano hospitali leo nadaiwa Shilingi milioni 113, halafu useme kwamba inafungiwa huduma ya maji, nini kitakachotokea?

Kwa hiyo, Serikali inatambua na Wizara yangu inatambua, ndiyo maana nataka tukae chini na Wizara ya Fedha ilipe madeni yote haya nchi nzima, ni Shilingi bilioni 20.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata sisi Mamlaka ya Majisafi Iringa Mjini, inadai. Tunaomba na sisi tulipwe.

Waheshimiwa muda wa maswali umeisha na maswali yote yameisha. Sasa naomba nitambue wageni waliopo hapa Bungeni asubuhi hii. Kwanza kuna wageni kwenye ukumbi wa Spika, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ambao ni familia yake; Bi Mariam Abdul-Aziz, ni mke wake. Yuko wapi mke wa Mheshimiwa? Karibu, ahsante sana, tunakushukuru; na Shekha Seif Selemani, ni mtoto wake. Asimame! Ahsante sana. Karibu!

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ni Dkt. Donald Mbando - Katibu Mkuu wa Wizara; ahsante, karibu! Dkt. Margret Mhando - Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, karibu! Ndugu Rabikra Mushi - Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii; Ndugu Rufaro Chotora - Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani – *WHO;* karibu, ahsante kwa kazi nzuri. Profesa Idris Mtuliya - Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa *MSD* na Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Rufiji. Karibuni sana Mheshimiwa Profesa. *(Makofi)*

Ndugu Augen Vuruga kutoka Wizara ya Afya Hospitali ya Rufaa Mbeya, karibu; Ndugu Ramadhani Ngayonga - Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Rufiji, karibu sana. Wakurugenzi na Wakuu wa Idara, wadau wa maendeleo; yupo Mwakilisho kutoka *UNICEF,* Wakurugenzi na Makamishna Wasaidizi. Meneja wa Miradi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Wawakilishi kutoka *UNICEF*, karibuni sana.

Vile vile tunao wanafunzi 78 wa Stashahada ya Uuguzi kutoka Chuo cha Uuguzi Milembe wakiongozwa na Rais wa Wanafunzi Ndugu Geofrey Warioba. Wanafunzi wamekosa mahali pa kukaa.

Wanafunzi 83 wa mwaka wa nne kutoka Chuo cha Udaktari cha Kumbukumbu ya Herbert Kairuki wakiongozwa na Ndugu Romana Malikusema. Kutoka *Kairuki Universtiy*, karibuni sana. Ahsanteni kwa kuja, tunawategemeeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ambao ni viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVAMATA) Mkoa wa Dodoma. Karibuni!

Wanafunzi wanaosomea Famasia na Uuguzi katika Chuo Kikuu cha *St. John's,* hawapo wamekosa mahali pa kukaa.

Mgeni wa Mheshimiwa Angella Kairuki, Mbunge na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni Dkt. Joselyne Kaganda - Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi Chakula na Lishe. Yuko wapi? Karibu!

Tunaye pia Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa ambaye ni Bi. Ginai Benedicta Justian, mke wa Mheshimiwa Mbassa, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge ambaye ni Mchungaji Sylvester Msengi wa kanisa la K.K.K.T Sanyaranda Itigi. Karibu! Wengine ni Wageni 48 wa Mheshimiwa Maria Hewa (Mbunge) ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Uhasibu Mwanza. Karibuni! *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge ambao wametoka Simiyu wakiongozwa na Ndugu Musa Elias. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Philemon Ndesamburo (Mbunge), wakiongozwa na Ndugu Evans Peter Massawe. Wako wapi?  Hawapo.

Pia tuna wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kutoka Nungwe Vijibweni wakiongozwa na Mheshimiwa Selemani Mathew. Wageni wa kutoka Jimbo la Kigamboni karibuni! *(Makofi)*

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni ni wanafunzi 30 na Walimu wawili kutoka *Theresia English Medium School* Morogoro, wamekosa mahali pa kukaa.

Wanafunzi 77 na Walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Maria De Mathias Dodoma. Karibuni sana, msome kwa bidii.

Wataalamu wa Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ambao ni Dkt. Caroline Nombo, Dkt. Fadhia Massawe na Bi. Judice Kahamba. Karibuni, utafiti tunauhitaji na hasa kwenye masuala ya Kilimo Kwanza. *(Makofi)*

Watawa 12 wa *Missionary* wa Fransisco wa Kapuchini kutoka Dodoma. Watawa karibuni sana.

Tunao Viongozi sita wa jukwaa la tiba asilia wakiongozwa na Bwana Benevitula Mwalongo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Tiba asilia Tanzania. Karibuni sana!

Wageni saba kutoka *Population Services International (PSI)* wakiongozwa na Bi. Fauzia Ismail Abood. Karibuni sana. Karibuni sana wageni kutoka *PSI! (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mheshimiwa Richard Ndassa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa leo mchana saa nane kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa 'B.'

Kuna tangazo ambalo Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Madhehebu ya Kiprotestant, kwamba leo Jumanne tarehe 2, kutakuwa na ibada ukumbi wa Msekwa ghorofa ya pili Kanisani saa nane mchana. Katibu!

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2014/2015 na mipango ya utekelezaji katika bajeti ya mwaka 2015/2016.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na mpango wa maendeleo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara na maelekezo yake ambayo yametupa mwongozo katika utendaji na kuimarisha huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Rais ameiunganisha Wizara na Taasisi za Kimataifa ambazo zinachangia katika jitihada za Serikali za kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2014 Mheshimiwa Rais amewezesha uboreshaji wa afya ya mama na mtoto kupitia mpango wa *Global Financing Facility* unaoratibiwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa nchi mojawapo katika nchi zitakazofadhiliwa katika mzunguko wa kwanza. Aidha, Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele…,

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, utulivu! Tokeni taratibu mnaotoka! Utulivu tafadhali!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** katika kuhimiza juhudi za kupambana na saratani ya tezi dume. Kwa jinsi hiyo, Wizara itaendesha kampeni maalum ili kuendeleza juhudi hizo za kuelimisha jamii kuhusu kupima mapema kwa lengo la kutambua tatizo mapema na kulidhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukurani kwa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Tanzania kwa miongozo na ushauri wake katika kuboresha huduma za afya hapa nchini. Miongozo na maelekezo yake yamesaidia kuimarisha na kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii nchini.

Vilevile nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongoza, kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma za afya na ustawi wa jamii. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake ambayo ni dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya na ustawi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii nchini, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margret Simwanza Sitta, Mbunge, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya bajeti hii.

Aidha, namshukuru Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, Mbunge, kwa kuendelea kutupatia ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Naahidi kuzingatia ushauri wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Pwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Sebba ambao wametuliwa kuwa Wabunge. Nawapongeza kwa uteuzi wao na ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendelee kuwatumikia wananchi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kifo cha Mheshimiwa Capt. Damian Komba aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali.

Vilevile natoa pole kwa waathirika wa mvua ya mawe iliyoambatana na mafuriko, yalitokea Wilaya wa Kahama katika Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Kusini Magharibi pamoja na mafuriko mengine yalitokea sehemu mbalimbali nchini. Pia natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali mbalimbali waliopo hospitalini na majumbani. Namwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Sekta ya Afya imeingia rasmi katika mpango wa matokeo makubwa sasa, yaani *BRN* kuanzia mwaka 2015/2016.

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeshafanya maandalizi ya awali ya kutekeleza mpango huu. Vipaumbele vilivyoibuliwa kwa ajili ya utekelezaji, vimeanishwa katika aya ya tisa, sehemu ya kwanza hadi ya nne, ukurasa wa tano wa hotuba yangu ambayo naomba ichukuliwe yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya Wizara vya Afya na Ustawi wa Jamii katika bajeti ya mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha huduma za kinga, tiba, kuongeza usawa katika utoaji wa huduma za afya ili kupunguza vifo vya kina mama wajawazito;

(ii) Kuimarisha miundombinu kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Afya na Vyuo vya Ustawi wa Jamii kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji rasilimali watu;

(iii) Kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa *(MOI),* hospitali maalum kama vile Taasisi ya Saratani; *Ocean Road*, Mirembe na Kibong'oto. Pia hospitali za Rufaa za Kanda zikiwemo zile za Mbeya na Mtwara;

(iv) Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya;

(v) Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea huduma za afya;

(vi) Uimarishaji wa huduma za teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA);

(vii) Kutekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa; na

(viii) Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojiunga na mifuko ya Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kutekeleza majukumu yake, inazingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama nilivyoeleza kwa kirefu katika hotuba yangu aya ya 11 ukurasa wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hukusanya mapato yake kutoka Bodi na Mabaraza mbalimbali ya Wizara, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji huduma katika taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara imekusanya jumla ya Sh. 80,629,245,000/= ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 87,671,519,016/= yaliyoidhinishwa mwaka 2014/2015. Hii ni sawa na asilimia 102.5 ya makadirio ya makusanyo ambayo yamevuka lengo kutokana na usimamizi thabiti na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya Sh. 122,309,541,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 jumla ya Sh. 659,743,825,000/= ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Kati ya fedha hizo, Sh. 354,014,333,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 305,729,492,000/= za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya Sh. 525,273,499,325/= zilipokelewa. Kati ya fedha zilizopokelewa Sh. 273,232,217,789/= ni fedha za matumizi ya kawaida na Sh. 250,041,281,536/= ni fedha za miradi ya maendeleo.

Kati ya fedha zilizopokelewa Sh. 352,399,186,592/= zilitoka Hazina na zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara. Vilevile dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya Sh. 170,874,312,731/= vilipokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo ambao ni Mfuko wa Pamoja wa kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina Sh. 273,232,217,789/= zilitumika kwa matumizi ya kawaida na Sh. 79,166,968,805/= kwa matumizi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya imekuwa ikikabaliwa na upungufu wa watumishi kwa muda mrefu. Kwa mwaka 2011/2012 sekta ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa wastani wa asilimia 58 ikilinganishwa na mahitaji halisi. Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2011 - 2015 Wizara yangu imetekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kutatua changamoto hiyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kudahili wanafunzi 35,973 katika Vyuo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuhitimu masomo yao, Serikali ilihakikisha wanaajiriwa katika mamlaka mbalimbali za ajira ambapo jumla ya watumishi 35,574 waliajiriwa. Haya ni mafanikio makubwa kwa Serikali kwani ajira hizo zimepunguza uhaba wa watumishi kama nilivyoeleza awali, yaani kutoka asilimia 58 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 52 mwaka 2014 wakati kukiwa kuna ongezeko la majengo na upanuzi wa hospitali mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika Vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii kutoka wanafunzi 8,582 mwaka 2013/2014 hadi wanafunzi 11,192 mwaka 2014/2015. Hivyo Serikali imevuka lengo la mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi la kudahili wanafunzi 10,000 waliotarajiwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeendelea kufadhili anafunzi 241 wanaochukua mafunzo ya Uzamili katika Vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kupunguza uhaba wa Watalaam wanaotoa huduma za kibingwa nchini. Tangu mwaka 2010 hadi sasa jumla ya wanafunzi 768 wamepata utaalam wa kibingwa katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wataalam wanaoajiriwa wanabaki maeneo waliyopangiwa kwa kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara inaendelea na ujenzi wa nyumba 90 za watumishi wa Vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri za Mikoa ya Arusha, Manyara, Pwani na Morogoro. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya nyumba 220 zitajengwa katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Tanga, Geita, Pwani, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Serikali imetoa kibali cha ajira za wataalam 8,589 wa kada mbalimbali za afya. Wizara imewapangia vituo vya kazi jumla ya wataalam 8,345 katika vituo vya kutolea huduma ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Mkoa; na wataalam 244 katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mgawanyo wa wataalam hawa umezingatia uwiano ili kupunguza changamoto za watumishi wa kada ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha utendaji kazi, kupima, kufanya ufuatiliaji na kupanga vipaumbele vya sekta vikao vya pamoja vya wadau wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii vimefanyika.

Aidha, katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Afya, Wizara ilianzisha utaratibu wa kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii *(Community Score Card)*. Lengo ni kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini hiyo ilifanyika katika Zahanati na Vituo vya Afya vya Serikali vya Halmashauri za Wilaya 11 za Bagamoyo, Mvomero, Morogoro, Mpwapwa, Chamwino, Karatu, Monduli, Arusha, Hai, Rombo na Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imehakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa kwa Halmashauri mpya 29 ambazo zilipatiwa mafunzo ya kuunda Bodi za Halmashauri za Huduma za Afya. Hadi kufikia Aprili, 2015 Halmashauri 21 kati ya zilizopatiwa mafunzo ziliunda Bodi**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeboresha upatikanaji wa takwimu za utoaji wa huduma za afya kutoka vituo vya kutolea huduma nchini kwa kutumia programu ya *District Health Information Systems* Na. 2. Kwa sasa upatikananji wa taarifa umekuwa rahisi na wa kuaminika kwa wastani wa asilimia 90 kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkatati wa TEHAMA (*e'Health*) 2013 - 2018, lengo ni kutumia TEHAMA katika kuboresha huduma za afya. Aidha, *TEHAMA* imesaidia kupata takwimu sahihi kwa wakati, kudhibiti mapato, dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba. Mpango huu unajumuisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki, tiba mtandao na matumizi ya simu za kiganjani (*mHealth*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeziunganisha hospitali za rufaa za kanda za Bugando, *KCMC* na Hospitali Maalum ya *Ocean Road* katika mfumo wa tiba mtandao *(telemedicine)*. Utaratibu huu umerahisisha upatikanaji wa huduma za ushauri wa tiba kwa wagonjwa wengi kwa kutumia wataalam wachache na gharama nafuu. Pia, Wizara imekamilisha kuunganisha Hospitali zote za Rufaa za Mikoa katika mkongo wa Taifa na kuzifanya kuwa na uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaunganisha Hospitali Maalum za *MOI* na Mirembe; Hospitali za Rufaa za Mkoa za Morogoro na Lindi; Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa ya Nyangao; Hospitali za Halmashauri za Mafia, Nachingwea na Kilosa; na Hospitali Teule ya Turiani kwenye tiba mtandao. Aidha, Wizara itafunga mifumo ya kielektroniki katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Amana, Temeke, Mount Meru, Manyara, Morogoro, Kagera, Iringa na Mtwara.

Vilevile, itafunga katika Hospitali za Ndanda na Hospitali Maalum ya Kibong'oto. Vilevile, Wizara inaboresha mfumo wa kielekroniki wa kutayarisha mipango *(PlanRep)* ili kuwezesha Halmashauri kuandaa mpango na bajeti kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa wananchi wote wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha wala kujali hali yao ya kiuchumi katika jamii, *(socio – economic status)*. Hadi Machi, 2015, wafaidika walio chini ya bima mbalimbali za afya nchini ni asilimia 22.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala ya mwaka 2010 ilidhamiria kufikia asilimia 30 ya wananchi wote. Ili kuhakikisha mafanikio haya yanaendelezwa na kuboreshwa, Wizara imeandaa Mkakati wa Ugharamiaji Huduma za Afya Nchini unaoainisha njia madhubuti za kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata hifadhi ya jamii katika eneo la afya. Utekelezaji wa mkakati huo utaanza baada kuridhiwa na Serikali kwa mujibu wa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeanza kutumia mfumo wa malipo wa kieletroniki kwa vituo 228 kati ya vituo 250 vilivyokusudiwa. Mfumo huu utawezesha malipo kufanyika ndani ya siku 60 zilizowekwa kisheria tangu watoa huduma wanapowasilisha madai.

Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Mfuko chini ya Mpango wa Bima ya Afya na Mfuko wa Jamii ulikuwa na wanufaika ambao ni asilimia 20 ya Watanzania wote. Kati ya hao, asilimia 7.2 ni wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na asilimia 12.8 ni wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii. Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali zikiwemo, mabadiliko ya Sheria ambayo yameuwezesha Mfuko kuongeza uandikishaji wa makundi mbalimbali kama: vikundi vya wajasiriamali na ushirika, wanafunzi, Taasisi za kidini, Madiwani na Mashirika Binafsi ambayo awali yalikuwa hayaruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya mapitio ya viwango vya tozo za uchangiaji za huduma za tiba nchini na kupendekeza viwango vipya ambavyo vitaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2015. Kamati maalum imeundwa inayojumuisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Afya ambayo ina jukumu la kupokea mapendekezo na maboresho ya tozo hizo, lengo likiwa ni kulinda haki ya wananchi, watoa huduma za afya na watoa huduma za Bima za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa Kitaifa na Kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Kama unavyofahamu, siku za hivi karibuni nchi yetu imepokea idadi kubwa ya wakimbizi kutoka nchi ya Burundi. Hadi tarehe 25 Mei, 2015 jumla ya wakimbizi 50,829 wameingia nchini. Pamoja na hali hiyo, kumetokea mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambapo hadi tarehe 31 Mei, 2015 jumla ya wagonjwa 4,510 waliripotiwa kuwa na ugonjwa huo na vifo 31 vimetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu, imetoa dawa zenye thamani ya Shilingi milioni 309 ambazo zinatumika kudhibiti ugonjwa huo katika Makambi ya Wakimbizi hao. Aidha, Wataalam wa Afya 91 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamepelekwa katika Kambi hizo ili kuimarisha utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria, 2014 - 2020 kwa kutekeleza afua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa Malaria nchini. Kupitia afua hizo, kiwango cha maambukizi ya Malaria kimeshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 9.2 mwaka 2011/2012. Lengo ni kufikia asilimia tano ifikapo mwaka 2016.

Mhesimiwa Mwenyekiti, aidha, utekelezaji wa afua mbalimbali umechangia katika kufikia kwa malengo ya milenia ambapo matumizi bora ya vyandarua pamoja na upatikanaji wa dawa umesaidia kuokoa maisha ya watoto 60,000 ambao wangefariki kwa ugonjwa wa Malaria kila mwaka. Kupungua kwa idadi ya wagonjwa kutoka wagonjwa 326 kwa kila watu 1,000 mwaka 2009 hadi kufikia wagonjwa 161 kwa kila watu 1,000 mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilisambaza dozi 12,911,100 za dawa mseto za kutibu Malaria na vitendanishi vyenye jumla ya vipimo milioni 28 vya kupima Malaria katika vituo ili kudhibi uwepo wa vimelea kabla ya matibabu. Aidha, Wizara iligawa vyandarua 500,000 katika Shule za Msingi na Sekondari za Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kupitia Programu ya Wanafunzi Shuleni.

Vilevile, Wizara iliendelea na zoezi la kunyunyizia dawa ya Ukoko ndani ya nyumba katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kufikia nyumba 400,000 ambapo takriban wananchi 2,000,000 walikingwa dhidi ya Malaria katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwa kutumia viuadudu vya kibailojia katika Kata za Jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji sita iliyofanyiwa maandalizi ya mpango huu. Miji hiyo ni Kibaha, Mwanza, Musoma, Bukoba, Shinyanga na Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa matibabu ya Kifua Kikuu na Ukoma bila malipo kwa wagonjwa wote wanaogundulika kuwa na Kifua Kikuu na Ukoma. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 90 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walioanza matibabu wanapona ikilinganishwa na kiwango cha uponyaji kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani cha asilimia 85.

Aidha, Wizara imeandaa mkakati na miongozo ya kuboresha huduma za Kifua Kikuu kwa watoto nchini. Huduma hizo zimesambazwa katika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Simiyu, Singida, Tabora, Njombe, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mwanza, Kilimanjaro, Pwani na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa wastani wa utambuzi wa maambukizi ya Kifua Kikuu kwa watoto Kitaifa umeongezeka kutoka asilimia 8.6 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 10.6 mwaka 2013, ikilinganishwa na kiwango kinachopendekezwa na Shirika la Afya Duniani cha utambuzi kuwa kati ya asilimia 10 hadi 15. Baada ya utambuzi huo, watoto hao waliingizwa katika mfumo wa matibabu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya, Wizara iliweka kipaumbele katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Kutokana na jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka asilimia 5.8 mwaka 2008 hadi asilimia 5.3 mwaka 2012. Aidha, kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama wajawazito kwenda kwa watoto kimepungua kutoka asilimia 26 mwaka 2010 hadi asilimia 15 mwaka 2012. Vilevile, idadi ya watu wanaopima VVU kwa hiyari imeongezeka kutoka watu 11,640 mwaka 2009 na kufikia 20,469,241 mwaka 2013.

Pia, Wizara imeongeza wigo wa kuwahudumia na kuwapatia dawa za UKIMWI kutoka wagonjwa 335,292 mwaka 2010 hadi kufikia watu 640,084 ilipofika mwezi Aprili, 2014. Aidha, Wizara imeweka kipaumbele katika afua ya tohara kwa wanaume. Kutokana na tafiti zilizopo afua hii ina matokeo makubwa ya kupunguza maambukizo ya UKIMWI kwa asilimia 60. Tangu kuanza kwa utekelezaji wa afua hii mwaka 2010, jumla ya wanaume 1,138,000 wamefanyiwa tohara ikilinganishwa na lengo la kufikia wanaume 2,102,252 ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya ya Kupambana na UKIMWI ya 2013 - 2017, kwa kutoa ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa hiari. Hadi kufikia Desemba, 2014, idadi ya watu waliopima VVU ilikuwa 25,468,564 na kufanya ongezeko la watu karibu milioni tano, ikilinganishwa na takwimu za Desemba, 2013.

Aidha, Wizara imeziwezesha Kliniki 109 zinazotoa *ARV* kwa wanawake wajawazito wenye *VVU (Option B+)* ziweze pia kutoa huduma ya kupambana na UKIMWI kwa watoto wanaoishi na VVU. Pia, huduma za wagonjwa majumbani zimepanuliwa na kufikia watu 338,547 kati ya lengo la watu 424,298 mwaka 2014. Vilevile, Wizara itaendelea kupanua huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kufikia ongezeko la watu milioni saba na kutoa dawa za *ARV* kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI 880,681.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefikia lengo la kuwa na mashine ndogo 525 za kupima *CD4* kwa ajili ya Vituo vya Afya na Zahanati. Vilevile, mashine ndogo 383 zimefungwa kifaa maalum kinachowezesha taarifa za upimaji wa *CD4* na matumizi ya vitendanishi kutumwa moja kwa moja kwa njia ya mtandao kwa mfumo wa kielektroniki wa *CD4 Logistic Information System,* hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwenye kanzidata *(Database)* ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti *UKIMWI.* Vilevile, Wizara iliendelea kutekeleza afua ya tohara kwa wanaume kama nilivyokwisha ieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala, Serikali imefanikiwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 454 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2010 hadi kufikia vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2012.

Aidha, vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka 81 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2010 hadi kufikia 54 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2013, hivyo kufikia lengo la Maendeleo ya Milenia namba nne la kupunguza vifo vya watoto kwa theluthi mbili ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Matatizo ya Uzazi na Vifo vya Watoto mwaka 2008/2015. Katika eneo la afua za huduma za watoto, Wizara iliwajengea uwezo jumla ya watoa huduma 9,997 katika maeneo ya stadi za kuokoa maisha ya mama na mtoto mchanga, kumhudumia mtoto mgonjwa chini ya miaka mitano, kumsaidia mtoto mchanga kupumua, huduma za afya ya rafiki kwa vijana katika vituo vya kutolea huduma. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza *Ambu bags/masks* 3,314 na *Penguin suckers* 5,567 kwa ajili ya kuwahudumia watoto wachanga wanaopata tatizo la kupumua na madoli ya kufundishia 1,571 katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la saratani limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka. Ili kukabiliana na tatizo hilo, katika mwaka 2014/2015, Wizara imefungua vituo vipya 64 vya kutolea huduma ya uchunguzi na tiba za awali za saratani ya shingo ya kizazi katika Mikoa kama ilivyoainishwa. Aidha, Wizara imenunua vifaa vinavyohitajika kuchunguza saratani ya shingo ya kizazi kwa kila kituo na kuwafundisha watoa huduma za afya 213 kuhusu matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya mafanikio ya chanjo vimeendelea kupanda hadi kufikia asilimia 97 kwa mwaka 2014/2015. Katika kuhakikisha chanjo zinatolewa kwa ubora unaotakiwa, Wizara ilinunua vichupa 9,340,790 vya chanjo za *BCG, OPV, Penta, PCV13, Rota,* Surua na Rubella pamoja na Pepopunda vyenye jumla ya dozi 67,393,750 na majokofu 437 na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini.

Aidha, Wizara imeanzisha chanjo mpya yenye muungano wa chanjo mbili za Surua na Rubella kwa watoto wenye umri wa miezi tisa na miezi 18 ili kuwakinga dhidi ya magonjwa hayo. Katika kufikia lengo la kutekeleza mkakati wa kutokomeza magonjwa hayo hapa nchini, Kampeni ya Chanjo ya Surua, Rubella ilifanyika kwa watoto wenye umri kati ya miezi tisa hadi miaka 15. Kampeni hiyo ilijumuisha afua nyingine muhimu zikiwemo utoaji wa Vitamini A na dawa za kukinga magonjwa yasiyopewa kipaumbele ambayo ni minyoo ya tumbo, matende

na mabusha. Pia, Kampeni hiyo ilipata mafanikio makubwa ambapo walengwa walikuwa ni watoto milioni 21 na waliochanjwa walikuwa watoto milioni 20.5 sawa na asilimia 97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha walengwa wote wa chanjo wanafanikiwa nchini, Wizara ilianzisha Mkakati wa *Reach Every District Reach Every Child* mwaka 2009 ukiwa na lengo la kuondoa vikwazo vyote na changamoto za utoaji wa chanjo; Mkakati huu umesaidia kupunguza idadi ya Halmashauri zilizokuwa nyuma kwenye kiwango cha chanjo kutoka 29 mwaka 2013/2014 hadi Wilaya 19 mwaka 2014/2015. Kutokana na umuhimu wa huduma hii, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri hizo ambazo hazifanyi vizuri, waongeze juhudi za kumfikia kila mtoto, aweze kupata haki yake ya msingi ya chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanya utafiti wa hali ya lishe nchini kwa kutumia mbinu ijulikanayo kama *SMART*. Utafiti huo ulijumuisha Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Matokeo ya utafiti huo ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwaka 2010 yalibainisha kupungua kwa wastani wa viwango vya Kitaifa vya utapiamlo kwa watoto kwa viashiria vya udumavu, ukondefu na uzito pungufu. Aidha, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa udumavu umepungua kutoka asilimia 42 hadi 35; ukondefu umepungua kutoka asilimia tano hadi nne; na uzito pungufu kutoka asilimia 16 hadi 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI* imeendelea kuboresha huduma za tiba kwa kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi. Katika utekelezaji wa Mpango huo, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 6,260 mwaka 2010 hadi 7,014 mwaka 2015.

Aidha, katika kipindi hiki Serikali imefanikiwa kuanzisha huduma mpya za kibingwa na uchunguzi hapa nchini na kuwawezesha wananchi kupata huduma za kibingwa ambazo awali zilikuwa hazitolewi hapa nchini. Huduma hizo ni pamoja na upasuaji mkubwa wa moyo, upasuaji wa mgongo na ubongo, kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo na uanzishaji wa huduma za dharura pamoja na ununuzi wa mashine za kisasa za matibabu mbalimbali ikiwemo tiba ya saratani kwa kutumia mionzi. Ongezeko hilo la vituo na uanzishwaji wa huduma hizi za kibingwa limeongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Saratani *Ocean Road* iliendelea kutoa huduma za kinga, uchunguzi na tiba ambapo jumla ya wagonjwa 15,972 walihudumiwa na kati yao, wapya walikuwa 3,267. Jumla ya wanawake 6,452 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti ambapo 516 walibainika kuwa na dalili za awali za saratani ya shingo ya kizazi na 129 walibainika kuwa na dalili za saratani ya matiti na kuendelea na uchunguzi. Aidha, huduma za kinga, uchunguzi na matibabu ya saratani na tiba shufaa zimeendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 1,897 wamepata huduma katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma za uchunguzi na tiba ya saratani, Wizara imenunua mtambo wa uchunguzi na tiba ya saratani ya aina ya *Linear Accelerator* yaani *(LINAC)* na ufungwaji wa mtambo huu unaendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea na ujenzi wa jengo la kusimika mashine mbili mpya na za kisasa za *LINAC* na *CT Simulator* na kubadilisha chanzo cha mionzi katika mashine ya mionzi ya *Equinox* 80 na kununua mashine za tiba kwa mionzi *(LINAC)* kwa ajili ya huduma ya matibabu ya saratani katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuimarisha huduma za tiba za kibingwa katika Hospitali ya Taifa, Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda ili kupunguza idadi ya vifo na gharama za kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa uchunguzi na matibabu.

Jumla ya wagonjwa 164 walifanyiwa upasuaji wa moyo; katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili 61 na Hospitali ya Rufaa ya Bugando 41. Pia, *Cath lab procedures* 62 zilifanyika katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Vilevile, wagonjwa 98 walifanyiwa upasuaji maalum kwa kutumia tundu dogo *(Laparascopic surgery)* na Hospitali ilipata tuzo ya upasuaji bora iliyotolewa na *British Medical Award*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wanapata huduma za kibingwa, Wizara inaendelea na mpango wa kuleta Madaktari Bingwa nchini. Mwaka 2014/2015 wataalam bingwa 28 kutoka Marekani na India waliletwa na kutoa huduma za mishipa ya damu iliyoziba ambapo wagonjwa 19 walihudumiwa, ambapo huduma hii ilitolewa kwa mara ya kwanza Afrika ya Mashariki.

Aidha, wataalam bingwa wa upasuaji wa moyo kutoka India walitoa huduma kwa watoto 12 wenye magonjwa ya moyo kwa kuwafanyia upasuaji mkubwa. Wataalam hao walitoa huduma hizo kwa kushirikiana na Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Vilevile, Wataalam 33 kutoka Saudi Arabia chini ya ufadhili wa *DHI Nurevn Islamic Foundation* wakishirikiana na Madaktari bingwa wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 66 ambapo kati yao wagonjwa 23 walifanyiwa upasuaji mkubwa na *Cathetarization* kwa wagonjwa 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo umeokoa jumla ya Shilingi bilioni 1.3 ambazo zingetumika kugharamia wagonjwa ambao wangepelekwa nje ya nchi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za upasuaji wa moyo na kuanzisha Taasisi ya Moyo Muhimbili inayojitegemea badala ya utaratibu wa sasa wa kituo hicho kuwa chini ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine mpya tano za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo zimenunuliwa na kufanya idadi ya mashine zilizopo kuwa 16. Aidha, wagonjwa 76 walipata huduma za tiba ya figo kupitia huduma ya kuchuja damu kwa mizunguko 6,066 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Wagonjwa 35 walihudumiwa katika Kituo cha kutoa huduma za afya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuboresha huduma hizi ili wagonjwa wengi zaidi wanufaike na huduma za kusafisha damu na kuweka juhudi za kufikia lengo la kupandikiza figo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Mifupa Muhimbili ilifanya upasuaji wa nyonga na kuweka viungo bandia kwa wagonjwa 250 na goti kwa wagonjwa 60. Aidha, upasuaji ulifanyika kwa watoto 558 wenye vichwa vikubwa, wagonjwa 165 wa ubongo na wagonjwa 312 wa uti wa mgongo na mishipa ya fahamu.

Vilevile, ujenzi wa Awamu ya Tatu wa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2015. Ujenzi huu utakapokamilika na huduma kuanza kutolewa, utaratibu wa kushirikiana na kuwaleta Madaktari Bingwa kutoka nje ya nchi utaendelea ili kujenga uwezo wetu wa ndani. Aidha, Hospitali ya Mirembe ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili 1,800 waliolazwa na 13,500 walihudumiwa na kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile jumla ya wagonjwa wa akili wahalifu wapya 194 walihudumiwa na Taasisi ya Isanga na 40 walipata ruhusa kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria na kurudishwa makwao.

Pia, Wizara iliendelea kutoa huduma ya *Methadone* kwa waathirika wa kujidunga dawa za kulevya. Jumla ya waathirika 2,297 walihudumiwa ambapo kati ya hao 946 walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, 440 Hospitali ya Temeke na 911 Hospitali ya Mwananyamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisambaza na kufunga mashine za kutibia meno katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Manyara, Tabora, Temeke na Tumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji halisi ya damu nchini ni wastani wa chupa 450,000 kwa mwaka. Mikakati ya kufikia lengo hili ni pamoja na kujenga vituo vya ukusanyaji wa damu kwa kila mkoa na kila Halmashauri. Hivyo natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutenga bajeti ya ukusanyaji wa damu katika bajeti zao. Wizara iliendelea kuratibu upatikanaji wa damu salama ambapo jumla ya chupa 162,367 za damu zilikusanywa ikilinganishwa na chupa 160,000 zilizopangwa kukusanywa.

Aidha, asilimia 35 ya damu iliyopatikana ilitokana na wachangiaji wa kudumu. Pamoja na kufikia lengo, kiasi kilichokusanywa ni asilimia 40 ya mahitaji ya nchi. Natoa wito kwa wadau wote, tushirikiane kuchangia damu kwa hiari. Kwa mwaka 2015/2016, Wizara imetenga jumla ya Shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya kununulia vitendanishi na mahitaji muhimu ya Mpango wa Damu Salama. Hapo awali mpango huo ulikuwa ukipata uhisani wa Wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuwezesha utekelezaji na uboreshaji wa ushirikiano na Sekta Binafsi ambapo kufikia sasa asilimia 73 ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini vinamilikiwa na Serikali na asilimia 27 ni vya Sekta Binafsi. Aidha, Halmashauri nyingine nne zimeingia mkataba wa utoaji huduma za afya na vituo vya kutolea huduma na kufanya jumla ya Halmashauri 67 kuwa na mikataba na vituo 68 vya binafsi vingi vikiwa vya Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya Sh. 228,720,505,813/= zimetumika kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa Sh. 47,346,193,082/= ambapo kati ya fedha hizo Sh. 24,617,026,082/= zilitumika kununua na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi na kiasi kilichobaki cha Sh. 22,729,167,000/= kilitumika kulipia deni la *MSD*.

Aidha, Wadau wa Maendeleo walitoa kiasi cha Sh. 181,374,312,731/= ambapo kati ya fedha hizo Sh. 10,500,000,000/= zilitoka kwa wadau wa mfuko wa pamoja na Sh. 170,874,312,731/= zilitoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ambao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na *UKIMWI*, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 jumla ya Sh. 336,002,706,847/= zimetengwa kwa ajili ya kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma. Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa Sh. 85,380,393,000/= na Sh. 18,662,343,250/= zitatokana na asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uchangiaji wa huduma za afya katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, Sh. 231,959,970,597/= zitatolewa na Wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imeendelea kudhibiti upotevu wa dawa ambapo Bohari ya Dawa imeweza kuweka nembo ya *GOT* kwenye aina 65 za dawa ambayo ni sawa na asilimia 50 ya utekelezaji wa lengo lililopangwa.

Aidha, Bohari ya Dawa imekamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika Mikoa ya Tanga na Tabora yenye ukubwa wa mita za mraba 4,500 ambayo ni asilimia 60 ya lengo.

Wizara imeanza kushirikisha Sekta Binafsi kwa ajili ya ununuzi wa dawa pale ambapo bidhaa hizo zitakosekana Bohari ya Dawa. Jumla ya Washitiri binafsi 18 katika mikoa tisa wamepatikana ili kuwezesha upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Bohari ya Dawa itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa karibu na wananchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara hii ilifanya usimamizi shirikishi katika Hospitali 50 zilizopata mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo.

Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa Wajumbe 538 wa Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri, Timu za Menejimenti za Hospitali na Timu za Uimarishaji Ubora katika Hospitali za Halmashauri kwenye Mikoa mipya minne ambayo ni Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya utoaji salama wa sampuli za damu kwa wataalam 549 katika Hospitali ya *MOI*, Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, *KCMC* na Bugando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa kwa kuanza kufanya tathimini kwa vituo vyote vinavyotoa huduma za afya ya msingi kwa awamu kwa kuanza na Mikoa 12 ya Dar es Salaam, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora. Vituo vitapewa hadhi ya nyota moja hadi nyota tano kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Mipango ya uboreshaji huduma itaandaliwa na vituo kuitekeleza kwa kupatiwa msaada wa kitaalamu kutoka Timu ya Uendeshaji Afya za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Wizara yangu kwamba asilimia 80 ya vituo vyote vifikie nyota tatu angalau katika kipindi cha miaka miwili inayofuata. Wizara kwa kupitia Mabaraza ya Taaluma ilisimamia maadili ya kusimamia wataalam waliokidhi viwango vya kutoa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2015, jumla ya wataalam 9,123 walisajiliwa kupitia Mabaraza yao ya Kitaaluma. Mabaraza haya ni pamoja na Madaktari na Madaktari wa Meno, Uuguzi na Ukunga, Famasia, Maabara, Upeo wa Macho Kuona na Afya ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisajili vituo binafsi vya kutolea huduma za afya 98; vituo vya kutolea huduma ya *Optometria* na maduka yanayosambaza na kuuza vifaa vya *Optometria* tisa; vituo vya tiba asili na tiba mbadala 74; Maabara binafsi za afya 117; na taasisi zinazotoa huduma za afya ya mazingira 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kupitia Baraza la Famasia imesajili vyuo vinne vinavyotoa kozi katika ngazi ya cheti na vyuo vitatu vinavyotoa kozi ya mwaka mmoja *(pharmaceutical dispensers)* ambavyo ni vya wamiliki binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Baraza la Famasi limetoa mafunzo kwa watoa dawa 692 wa maduka ya dawa muhimu na wamiliki wa maduka ya dawa muhimu 886. Pia, Baraza la

Famasia limesajili maduka mapya 106 ya dawa moto, maduka 490 ya dawa muhimu na maghala matatu ya kuhifadhia dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Dawa za Asili Muhimbili lilitoa mafunzo kwa waganga wa tiba asili 54 kuhusu lishe bora, usafi, kuandaa dawa za asili na namna bora ya kumhudumia mgonjwa. Aidha, Baraza liliondoa mabango 1128 ya waganga wa tiba asili katika maeneo mbalimbali yanayokizana na Sheria Namba 23 ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ustawi wa jamii, huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu: Serikali inaendelea kutoa huduma za msingi zikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu na unasihi kwa wazee na watu wenye ulemavu, wasiojiweza 869 wanaotunzwa na kulelewa katika makazi 17 ya Serikali, kati yao wanaume 408 na wanawaka 461. Aidha, Wizara iliratibu huduma za matunzo katika makazi 24 yanayoendeshwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Katika kufanikisha utengamao wa wazee na watu wenye ulemavu, Wizara imewezesha kujengwa kwa nyumba 42 za bei nafuu kwa kushirikisha jamii na kuwatengamanisha wakazi 110 katika jamii kwenye makazi ya Nandanga (Wilaya ya Lindi) na Mkaseka (Wilaya ya Masasi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pamoja na baadhi ya halmashauri zimechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha inaboresha huduma za wazee. Hivyo, napenda kuzipongeza halmashauri za Kilindi, Pangani, Iramba, Songea, Tarime na Kaliua ambazo zimechukua jukumu la kuwalipia Wazee kadi za *CHF* ili kuhakikisha wanapata huduma za afya wanapozihitaji bila kikwazo cha fedha. Naomba kuchukua nafasi hii kuwakumbusha kuwa jukumu la kuwahudumia wazee ni la halmashauri, hivyo ni vyema halmashuri zikajipanga kwa kuwalipia au kutoa huduma bila malipo kwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa mafunzo jumuishi kwa watu wenye ulemavu katika vyuo vya Yombo, Dar es Salaam na Chuo cha Wasioona Singida ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Jumla ya vijana 63 wamehitimu; kati yao wanawake ni 34 na wanaume 29. Aidha, jumla ya vijana 110 wanaendelea na mafunzo ikiwa wanawake ni 51 na wanaume 59. Vilevile, Wizara imekarabati miundombinu ya vyoo na mabweni katika Chuo cha Wasioona Singida na kukifanya kuwa rafiki zaidi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ustawi wa familia, watoto, malezi na maendeleo ya awali ya watoto wadogo: Katika kuimarisha huduma za ulinzi na usalama kwa watoto, Wizara ilitoa mafunzo ya ulinzi na usalama wa watoto kwa Maafisa Ustawi wa Jamii na Timu za Ulinzi na Usalama. Mafunzo hayo yalitolewa katika halmashauri za Shinyanga, Mkuranga, Kibaha, Same, Muleba, Karatu, Bagamoyo, Kisarawe, Kahama na Manispaa ya Shinyanga na Iringa na Jiji la Arusha na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 jumla ya halmashauri 30 zimewezeshwa kuanzisha mfumo wa ulinzi na usalama wa mtoto. Aidha, Wizara imesambaza na kutoa mafunzo ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (2013 – 2017) na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009 na Kanuni zake kwa watendaji wakuu katika halmashauri 37. Jumla ya matukio 3,449 ya unyanyasaji, ukatili, udhalilishaji na unyonyaji wa watoto yameripotiwa katika halmashauri za Manispaa za Temeke, Ilemela, Ilala, Kinondoni na Nyamagana, ukilinganisha na matukio 2,250 yaliyoripotiwa katika mwaka 2013/2014. Vilevile, jumla ya matukio 3,206 yameripotiwa kwa njia ya simu maalum, ukilinganisha na matukio 2,362 kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za haki za mtoto na marekebisho ya tabia: Wizara iliendelea kusimamia na kuratibu huduma zitolewazo kwa watoto walio katika mkinzano na

sheria. Wizara imehudumia jumla ya watoto 337 wakiwemo wavulana 304 na wasichana 33 waliohifadhiwa katika mahabusu za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es Salaam na shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Aidha, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wanaohudumia watoto walio katika mkinzano na sheria, ambapo watumishi 133 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, na mahabusu za watoto Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es Salaam na shule ya Maadilisho Irambo walipatiwa mafunzo kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya utoaji huduma. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itatoa mafunzo kwa wawezeshaji 20 katika Jiji la Mbeya na Manispaa ya Temeke ambao watatumika kutoa mafunzo kwa wasaidizi 67 wa watoto walio katika mkinzano na sheria wawapo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa kemikali nchini**:** Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya sampuli 10,974. Sampuli 3,260 zilikuwa za vyakula, dawa, kemikali, maji na maji taka, bidhaa za viwandani na mazingira. Kati ya sampuli hizo, sampuli 2,658 ambazo ni sawa na asilimia 82 zilichunguzwa na kutolewa matokeo. Sampuli nyingine 7,714 zilikuwa za makosa ya jinai, kati ya hizo sampuli 6,318 ambazo ni sawa na asilimia 82 zilichunguzwa na kutolewa matokeo. Aidha, Wakala ulitoa mafunzo kuhusu Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura 182 juu ya matumizi na usafirishaji salama wa kemikali kwa wadau 655.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba: Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua maeneo 6,484 yanayohusika na uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na ya kusindika chakula 1,484, sehemu za kuuzia chakula 2,630, maduka ya dawa 1,582, vituo vya afya 328, maduka ya vipodozi 1,992, maduka ya vifaa tiba 42, viwanda vya dawa nje ya nchi 76, viwanda vya dawa vya ndani vinne na viwanda vya vipodozi nane. Kati ya maeneo 6,484 yaliyokaguliwa, maeneo 5,624 yalikidhi vigezo sawa na asilimia 87. Maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya sheria, wamiliki walielekezwa kufanya marekibisho husika ndani ya muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu; hii ni pamoja na tani 60 za chakula zenye thamani ya Shilingi 120,998,636, tani 73 za dawa zenye thamani ya Shilingi 1,339,724,344 na tani 8.82 za vipodozi zenye thamani ya Shilingi 46,407,304. Aidha, Wizara itakamilisha Sera ya Chakula Salama na kuisambaza kwenye mikoa na halmashauri zote nchini. Sera hiyo itasaidia kuweka mkazo kwenye ukaguzi wa maeneo ya kutayarisha, kusafirisha, kuhifadhi au kuuzia chakula kwa kuyakagua na kuyaboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mamlaka ilichunguza sampuli 4,714 ambapo 1,854 zilikuwa za dawa, 2,676 za chakula, 106 za vifaa tiba na 78 za vipodozi. Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli 4,573 zilikidhi viwango sawa na asilimia 97. Bidhaa ambazo hazikukidhi vigezo ziliondolewa katika soko na baadhi zilikataliwa au kufutiwa usajili. Baadhi ya dawa hizo ni pamoja na dawa ya kutibu fangasi ya *Ketoconazole,* dawa ya malaria ya maji na vidonge aina ya *Amodiaquine.* Dawa zote za kikohozi zenye kiambato hai cha *Phemlypopanolamine,* dawa ya sindano ya *Chloromphemicol* inayotengenezwa na Kiwanda cha *Lincolin Pharmaceutical Limited* India na dawa ya maji *(capsule) aina ya Cloxacillin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa magonjwa ya binadamu: Wizara kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu imekamilisha ufuatiliaji kuhusu njia bora za kutibu maji katika Wilaya za Geita na Kisarawe. Matokeo ya utafiti huo yamewezesha kuandaa mpango wa kuhamasisha kuhusu usalama wa maji ngazi ya kaya kitaifa ikiwa ni moja ya kinga muhimu dhidi ya magonjwa ya kuhara. Aidha, taasisi kwa kushirikiana na Mpango wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele ilifanya utafiti wa ufuatiliaji wa ugonjwa wa

matende na mabusha katika Wilaya za Lushoto, Muheza, Mkuranga, Newala na Tandahimba. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa katika wilaya hizo maambukizi yamepungua chini ya asilimia moja na hivyo ugawaji wa dawa utasitishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utafiti wa matende na mabusha ulifanyika katika wilaya 35 za Mikoa ya Iringa, Rukwa, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Singida, Ruvuma na Njombe. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa maambukizi ya ugonjwa yamepungua chini ya asilimia mbili. Vilevile, utafiti wa ugonjwa wa vikope uliendelea katika wilaya 19 ambapo matokeo yameonesha wilaya saba za Kilindi, Tunduru, Kongwa, Mpwapwa, Chemba, Meatu na Bahi bado zitahitaji umezeshaji dawa kwa kinga-tiba. Pia, utafiti wa awali katika wilaya 19 umeonyesha kuwa ni wilaya moja tu ya Chunya itahitaji kuanza zoezi la ugawaji wa dawa za ugonjwa wa vikope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukrani: Katika mwaka 2015/16, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii. Aidha, napenda kuzishukuru nchi zinazochangia Mfuko wa Pamoja na zinazochangia nje ya Mfuko wa Pamoja ambapo mchango wao umesaidia kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Vilevile, napenda kuyashukuru mashirika ya kimataifa kwa ushirikiano wao katika kuboresha huduma za afya nchini. Pia, nazishukuru asasi za kiraia, sekta binafsi, vyuo vikuu, taasisi za kitafiti na vyama vya kitaaluma tunaoshirikiana nao. Wadau wote hao wameainishwa katika hotuba yangu kuanzia aya ya 144, ukurasa wa 78 hadi aya ya 148, ukurasa wa 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi katika Wizara hii, nimepata ushirikiano mkubwa toka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe (Mb), Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu Dokta Donan William Mmbando kwa kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu katika kipindi hiki. Vilevile, nawashukuru wafuatao:- Dokta Margaret Evelyne Mhando – Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Bwana Rabikira Onaufoo Mushi – Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Wakurugenzi wa Idara zote katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nawashukuru pia, watendaji wakuu na watumishi wote wa sekta ya afya na ya ustawi wa jamii. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu. Kipekee namshukuru mke wangu mpenzi, Mariam Abdulaziz na watoto wetu Tariq, Meyye, Shekhan na Amour kwa uvumilivu na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wa Jimbo la Rufiji, nawashukuru kwa ushirikiano mnaoendelea kunipatia katika kuendeleza Jimbo na naahidi nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo letu la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato na maombi ya fedha kwa Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya Shilingi 122,309,541,000, kati ya fedha hizo Shilingi 114,830,753,000 zitakusanywa katika mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara na Shilingi 7,478,788,000 ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa

huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na mabaraza ya kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2015/2016: Ili kuiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka 2015/2016, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na taasisi zake yenye jumla ya Shilingi 813,976,870,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 369,358,418,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 444,618,452,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; www.moh.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII MHE. DKT. SEIF SELEMANI RASHID (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2014/15 na Mipango ya Utekelezaji katika Bajeti ya mwaka 2015/16. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2015/16.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara na maelekezo yake ambayo yametupa mwongozo katika utendaji na kuimarisha huduma za afya na ustawi wa jamii. Mheshimiwa Rais ameendelea kuiunganisha Wizara na Taasisi za kitaifa na kimataifa ambazo zinachangia katika jitihada za Serikali za 2 kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Kwa Mwaka 2014, Mheshimiwa Rais amewezesha uboreshaji wa huduma za afya ya Mama na Mtoto kupitia Mpango wa "Global Financing Facility (GFF)" unaoratibiwa na Benki ya Dunia. Tanzania imekuwa nchi mojawapo kati ya nchi zitakazofadhiliwa katika mzunguko wa kwanza. Aidha, Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza juhudi za kupambana na saratani ya tezi dume. Kwa jinsi hiyo Wizara itaendesha kampeni maalum ili kuendeleza juhudi hizo za kuelimisha jamii kuhusu kupima mapema kwa lengo la kutambua tatizo mapema na kulidhibiti. Kampeni hii itafanywa na Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau wake.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati katika kuboresha huduma za Afya hapa nchini. Miongozo na maelekezo yake yamesaidia kuimarisha na kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii nchini.

4. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma za afya na

ustawi wa jamii. 3 Aidha, naomba nimpongeze kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge hili ambayo ni dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2015/16.

5. Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Pia, nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii.

6. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta (Mb), kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, namshukuru Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Dkt. Anthony Gervas Mbassa (Mb) kwa kuendelea kutupatia ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Naahidi kuzingatia ushauri wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hotuba zilizotangulia. Michango yao imesaidia kuboresha hotuba yangu. Nawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na ninaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.

7. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali. Aidha, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba ambao wameteuliwa kuwa Wabunge. Nawapongeza kwa uteuzi wao na ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendelee kuwatumikia wananchi kwa pamoja.

8. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kifo cha Mheshimiwa Kapteni John Damian Komba aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali. Vilevile, natoa pole kwa waathirika wa mvua ya mawe iliyoambatana na mafuriko yaliyotokea Wilaya ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Kusini Magharibi pamoja na mafuriko mengine yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini. Pia, natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali mbalimbali waliopo hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

9. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Sekta ya Afya imeingia rasmi katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* kuanzia mwaka 2015/16. Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeishafanya maandalizi ya awali ya kutekeleza mpango huu. Vipaumbele vilivyoibuliwa kwa ajili ya utekelezaji ni:- (i) Utendaji wa kufikia malengo *(Performance Management)* wa vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi za Halmashauri yaani Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, (ii) Kuwepo watumishi wa afya na ustawi wa jamii wa kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya, (iii) Upatikanaji wa dawa muhimu, vitendanishi, vifaa tiba na vifaa vingine vya matumizi katika hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati kwa nchi nzima na (iv) Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto.

**VIPAUMBELE VYA WIZARA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2015/16**

10. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika bajeti ya mwaka 2015/16 ni kama ifuatavyo:- (i) Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, kuongeza usawa katika utoaji wa huduma za afya ili kupunguza vifo vya kinamama wajawazito, (ii) Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya na vyuo vya ustawi wa jamii kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu, (iii) Kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali Maalum kama vile Taasisi ya Saratani Ocean Road, Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda zikiwemo zile za Mbeya na Mtwara, (iv) Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya (PPP), (v) Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya, (vi) Uimarishaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), (vii) Kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*, (viii) Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojiunga na Mifuko ya Bima za Afya.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/15**
**NA MWELEKEO WA KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA**
**KATIKA MWAKA 2015/16**

11. Mheshimiwa Spika, Wizara katika kutekeleza majukumu yake inazingatia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa II wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (2010), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya (2009 -2015), Mpango Kazi wa II wa Taifa wa Huduma na Matunzo kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi (2013 – 2017), Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007– 2017), Sera ya Taifa ya Wazee (2003) na Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu (2004). Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010.

**Mwenendo wa Mapato, Matumizi ya Kawaida**
**na Miradi ya Maendeleo**

12. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hukusanya mapato yake kutoka Bodi na Mabaraza mbalimbali ya Wizara, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 80,629,245,000.00 ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi 78,671,519,016.00 yaliyoidhinishwa kwa mwaka 2014/15. Hii ni asilimia 102.5 ya makadirio ya makusanyo ambayo yamevuka lengo kutokana na usimamizi thabiti na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka 2015/16, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 122,309,541,000.00.

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, jumla ya Shilingi 659,743,825,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi 354,014,333,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 305,729,492,000.00 za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2015 jumla ya Shilingi 523,273,499,325.00 zilipokelewa. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi 273,232,217,789.00 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 250,041,281,536.00 ni fedha za Miradi ya Maendeleo. 9 Kati ya fedha zilizopokelewa jumla ya Shilingi 352,399,186,594.00 zilitoka Hazina na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara. Vilevile, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya Shilingi

170,874,312,731.00 vilipokelewa kutoka kwa Wadau wa Maendeleo ambao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kati ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina, Shilingi 273,232,217,789.00 zilitumika kwa Matumizi ya Kawaida na Shilingi 79,166,968,805.00 kwa matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

14. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa watumishi kwa muda mrefu. Kwa mwaka 2011/12 sekta ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 58 ikilinganishwa na mahitaji halisi. Katika kipindi cha miaka mitano 2011- 2015, Wizara yangu imetekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kutatua changamoto hiyo. Mikakati hiyo ni pamoja ni kudahili wanafunzi 35,973 katika vyuo vya afya (Kiambatisho Na. 1a). Baada ya kuhitimu masomo yao Serikali ilihakikisha wanaajiriwa katika Mamlaka mbalimbali za ajira ambapo jumla ya watumishi wapya 35,574 waliajiriwa (Kiambatisho Na. 1b). Haya ni mafanikio makubwa kwa Serikali kwani ajira hizo zimepunguza uhaba wa watumishi kama nilivyoeleza awali yaani kutoka asilimia 58 mwaka 2011/12 hadi asilimia 52 mwaka 2014.

15. Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano eneo la rasilimali watu, naomba sasa nitoe taarifa utekelezaji wa kazi zilizofanyika katika eneo hili kwa mwaka 2014/15. Katika kipindi hicho, Wizara imeendelea kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya na ustawi wa jamii kutoka wanafunzi 8,582 mwaka 2013/14 hadi 11,192 mwaka 2014/15. Hivyo, Serikali imevuka lengo la Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) la kudahili wanafunzi 10,000 waliotarajiwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017. Aidha, Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi 241, wanaochukua mafunzo ya uzamili katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kupunguza uhaba wa wataalam wanaotoa huduma za kibingwa nchini. Tangu mwaka 2010 hadi sasa jumla ya wanafunzi 768 wamepata utaalam wa kibingwa katika fani mbalimbali.

16. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza Mkakati wa TEHAMA katika Sekta ya Afya kwa kuwianisha na majukumu mbalimbali ya Wizara. Katika kuwianisha Mkakati huo na upatikanaji wa rasilimali watu, Wizara imeanzisha mafunzo kwa njia ya kielektroniki kwa wanafunzi wauguzi wanaojiendeleza 11 kutoka ngazi ya cheti kwenda stashahada. Hadi sasa jumla ya wanafunzi 154 walidahiliwa katika mafunzo hayo. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza vyuoni vifaa vya kufundishia vikiwemo kompyuta za mezani 400, printa 24 na mashine kubwa 8 za kudurufu. Vilevile, Wizara imeboresha vyuo vya kufundishia Tabibu Meno vya Tanga na Mbeya kwa kuvinunulia mashine mbili za X-ray zinazohamishika kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma, kuongeza idadi ya ajira za watumishi wa Sekta ya Afya na udahili wa wanafunzi watarajali.

17. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itakamilisha mtaala wa Mafundi Sanifu Meno kwa kufuata mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Aidha, Wizara itaratibu uanzishwaji wa mafunzo ya Shahada katika Fani za Tiba na Uuguzi katika Chuo cha Madaktari Wasaidizi Mbeya na Chuo cha Uuguzi Bagamoyo. Kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Chuo cha Mtakatifu Joseph cha Songea na Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba cha Kilimanjaro, kwa kufuata Mfumo wa Tuzo za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

18. Mheshimiwa Spika, Wizara, imeendelea kuboresha huduma za mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Bagamoyo na Chuo Kikuu cha Hurbert Kairuki kwa kuvipatia vifaa mbalimbali vya kufundishia. Aidha, Wizara imekarabati chuo cha Newala na kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Vilevile, katika kuhakikisha tija na ufanisi kazini, Wizara inaendelea kutathmini utendaji wa watumishi wake kwa kutumia mfumo wa wazi wa upimaji wa watumishi (OPRAS).

19. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wataalam wanaoajiriwa wanabaki maeneo waliyopangiwa kwa kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Kwa mwaka 2014/15, Wizara inaendelea na ujenzi wa nyumba 90 za watumishi wa vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri za Mikoa ya Arusha (20), Manyara (30), Pwani (20) na Morogoro (20). Katika mwaka 2015/16 jumla ya nyumba 220 zitajengwa katika Mikoa ya Kigoma (30), Mwanza (20), Shinyanga (40), Simiyu (48), Kagera (10), Tanga (10), Geita (10), Pwani (12), Arusha (20) na Manyara (20).

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15 Serikali imetoa kibali cha ajira za wataalam 8,589 wa kada mbalimbali za afya. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imewapangia vituo vya kazi jumla ya wataalam 8,345 katika vituo vya kutolea huduma ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Mkoa na wataalam 244 katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Kiambatisho Na. 2). Mgawanyo wa wataalam hawa umezingatia uwiano ili kupunguza changamoto za watumishi wa kada ya afya.

21. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itahakikisha kuna uwiano wa wafanyakazi wa kutoa huduma hasa katika ngazi ya afya ya msingi nchini na kutoa kipaumbele kwenye mikoa 12 yenye upungufu mkubwa wa watumishi. Mikoa hiyo ni Simiyu, Geita, Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Tabora, Katavi, Singida, Dar es salaam na Pwani.

**URATIBU, UFUATILIAJI NA UGHARAMIAJI HUDUMA ZA AFYA**

**Uratibu na Ufuatiliaji Huduma za Afya**

22. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu mahusiano ya kiutendaji, ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wadau wa Maendeleo. Vikao vya pamoja vya wadau wa sekta ya afya vimefanyika ili kupima na kuboresha utendaji katika Sekta. Kwa kupitia vikao hivyo, wadau mbali mbali wameshiriki katika kufanya ufuatiliaji wa utoaji huduma za afya na kupanga vipaumbele vya sekta kwa pamoja vikiwemo vipaumbele vya Tekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

23. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya sekta ya afya, Wizara ilianzisha utaratibu wa kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card). Nyenzo hii ina viashiria vyenye vigezo maalum vinavyoshirikisha pande zote mbili wakiwemo watoa huduma na watumia huduma. Lengo ni kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Tathmini hiyo ilifanyika katika zahanati na vituo vya afya vya Serikali vya Halmashauri za Wilaya 11 za Bagamoyo, Mvomero, Morogoro, Mpwapwa, Chamwino, Karatu, Monduli, Arusha, Hai, Rombo na Moshi. Aidha, Wizara imehakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa, kwa Halmashauri mpya 29 ambazo zilipatiwa mafunzo ya kuunda Bodi za Halmashauri za Huduma za Afya. Hadi kufikia Aprili, 2015 Halmashauri 21 kati ya zilizopatiwa mafunzo ziliunda Bodi (Kiambatisho Na.3).

24. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeboresha upatikanaji wa takwimu za utoaji wa huduma za afya kutoka vituo vya kutolea huduma nchini kwa kutumia programu ya DHIS2. Kwa sasa upatikananji wa taarifa umekuwa rahisi na wa kuaminika kwa wastani wa asilimia 90 kwa kila mwezi.

25. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkatati wa TEHAMA (eHealth) 2013-2018, lengo ni kutumia TEHAMA katika kuboresha huduma za afya. Aidha, TEHAMA imesaidia kupata takwimu sahihi kwa wakati, kudhibiti mapato, dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba. Mpango huo unajumuisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki, tiba mtandao na matumizi ya simu za kiganjani (mHealth). Aidha, Wizara imeziunganisha hospitali za rufaa za kanda za Bugando, KCMC na Hospitali Maalum ya Ocean Road katika mfumo wa tiba mtandao (telemedicine). Utaratibu huu umerahisisha upatikanaji wa huduma za ushauri na tiba kwa wagonjwa wengi kwa kutumia wataalam wachache na gharama nafuu. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Ufungaji wa Mfumo wa Kieletroniki katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Nchini. Pia, Wizara imekamilisha kuunganisha Hospitali zote za Rufaa za Mikoa katika mkongo wa Taifa na kuzifanya kuwa na uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa urahisi.

26. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaunganisha Hospitali Maalum za MOI na Mirembe; Hospitali za Rufaa za Mkoa za Morogoro na Lindi, Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa ya Nyangao; Hospitali za Halmashauri za Mafia, Nachingwea na Kilosa; na Hospitali Teule ya Turiani kwenye tiba mtandao. Aidha, Wizara itafunga mifumo ya kielektroniki (HoMIS) katika hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Amana, Temeke, Mount Meru, Manyara, Morogoro, Kagera, Iringa na Mtwara. Vilevile, itafunga katika hospitali za Ndanda na hospitali maalum ya Kibong'oto. Wizara pia, itawezesha hospitali kuunda kamati za kusimamia utekelezaji ili kuhakikisha uendelevu na ufanisi wa mifumo hiyo. Vilevile, Wizara inaboresha mfumo wa kielekroniki wa kutayarisha mipango (PlanRep) ili kuwezesha Halmashauri kuandaa mpango na bajeti kwa urahisi.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya upanuzi wa mfumo wa matumizi ya simu kwa ajili ya kutolea taarifa mbalimbali za sekta ya afya (m-Health) katika Halmashauri za Mikoa ya Kagera na Kilimanjaro. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendeleza mfumo huo katika Halmashauri za Mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Kigoma, Arusha, Rukwa, Mbeya na Dar es Salaam (Kinondoni na Ilala).

**Ugharamiaji wa Huduma za Afya**

28. Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa wananchi wote wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha wala kujali hali yao ya kiuchumi katika jamii (socio – economic status). Aidha, Sera imesisitiza uwepo wa vyanzo vya fedha vinavyoaminika pamoja na kuhakikisha sekta ya afya inapata raslimali za kutosha za kugharamia huduma za afya. Mkakati mkubwa umekuwa katika kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. Hadi Machi 2015, wafaidika walio chini ya bima mbali mbali za afya nchini ni asilimia 22.82 (Kiambatisho Na.4). Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya 2010 ilidhamiria kufikia asilimia 30 ya wananchi wote. Ili kuhakikisha mafanikio haya yanaendelezwa na kuboreshwa, Wizara imeandaa Mkakati wa Ugharamiaji Huduma za Afya Nchini unaoainisha njia madhubuti za kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata hifadhi ya jamii katika eneo la afya. Utekelezaji wa mkakati huo utaanza baada kuridhiwa na Serikali kwa mujibu wa utaratibu.

29. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeanza kutumia Mfumo wa malipo wa kieletroniki kwa vituo 228 kati ya vituo 250 vilivyokusudiwa. Mfumo huu utawezesha malipo kufanyika ndani ya siku 60 zilizowekwa kisheria tangu watoa huduma wanapowasilisha madai. Aidha, ili kupeleka huduma karibu na jamii, Mfuko umeanza ujenzi wa ofisi za Mikoa ya Dodoma na Mbeya. Vilevile, Mfuko umejenga miundo mbinu ya kielektroniki yenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi taarifa mbalimbali za Mfuko ikiwemo taarifa za wanachama. Kuanzia tarehe 27/10/2014 hadi 28/02/2015, Mfuko ulikusanya taarifa za wanachama kupitia fomu

maalum na unaendelea na uhakiki wa taarifa hizo. Mara baada ya zoezi kukamilika taarifa zitaingizwa kwenye mfumo mpya wa Mfuko na hivyo kuweza kutoa vitambulisho vipya vitakavyosaidia kurahisisha huduma kwa wanachama na kudhibiti matumizi ya huduma kwa wasiostahili.

30. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Mfuko chini ya Mpango wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Jamii (CHF) ulikuwa unahudumia jumla ya wanufaika 8,729,389 ambao ni sawa na asilimia 20 ya watanzania wote kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Kati ya hao idadi ya wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilikuwa 3,144,115 ambao ni sawa na asilimia 7.2 na kwa Mfuko wa Afya ya Jamii ilikuwa na jumla ya wanufaika 5,585,274 ambao ni sawa na asilimia 12.8 ikilinganishwa na idadi ya watanzania wote. Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali zikiwemo, mabadiliko ya Sheria ambayo yameuwezesha Mfuko kuongeza uandikishaji wa makundi mbalimbali kama; vikundi vya wajasiriamali na ushirika, wanafunzi, Taasisi za kidini, Madiwani, na mashirika binafsi ambayo awali yalikuwa hayaruhusiwi.

31. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya viwango vya tozo za uchangiaji za huduma za tiba nchini na kupendekeza viwango vipya ambavo vitaanza kutumika kuanzia 1 Julai, 2015. Kamati Maalum imeundwa inayojumuisha wadau mbali mbali wa sekta ya afya ambayo ina jukumu la kupokea mapendekezo na maboresho ya tozo hizo. Lengo likiwa ni kulinda haki ya Wananchi, Watoa Huduma Afya na Watoa Huduma za Bima za Afya.

32. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii Mijini-Tiba kwa Kadi, halmashauri za Mikoa ya Pwani (Mji mdogo wa Kibaha), Tabora (Manispaa), Kigoma (Ujiji), Geita (Mji wa Geita), Katavi (Mji wa Mpanda), Njombe (Mji wa Njombe na Makambako), Manyara (Mji wa Babati) na Morogoro (Manispaa) wameanzisha huduma za Tiba kwa Kadi. Aidha, Manispaa na Miji katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Lindi, Singida zipo katika hatua mbalimbali za kutunga Sheria ndogo. Katika kufanikisha uanzishwaji wa Mpango wa Tiba kwa Kadi, Wizara inawakumbusha Watendaji wa Halmashauri za Manispaa au Miji kuzingatia uanzishwaji na utekelezaji wa mpango wa Tiba kwa Kadi.

**HUDUMA ZA KINGA - Udhibiti wa Magonjwa**

33. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Aidha, utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki umeimarishwa sambamba na kutoa mafunzo kwa wataalam (1,036) wa ngazi zote katika Mikoa ya Kilimanjaro (385), Mwanza (361) na Kagera (290). Teknolojia hiyo imerahisisha upatikanaji wa taarifa za magonjwa kwa haraka na hivyo kuwezesha kudhibiti magonjwa ya milipuko. Mpango huo utaendelezwa katika mikoa mingine mwaka 2015/16.

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Aidha, Serikali itaendelea kupanua utekelezaji wa Mkakati wa TEHAMA wa Wizara ili kuhakikisha taarifa za magonjwa zinapatikana kwa wakati na kwa uhakika zaidi. Vilevile, Wizara itaimarisha utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (eIDSR) kwa kuendesha mafunzo kwa wataalam 1,928 wa afya kutoka vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Pia, Serikali itaendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa pamoja na matukio mbalimbali ya kiafya kwa kutekeleza mpango kazi uliopo unaozingatia Kanuni za Afya za Kimataifa za mwaka 2005.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara imefuatilia na kuchukua tahadhari za kudhibiti magonjwa katika mipaka ya nchi yetu yanayoweza kuingia kutokana na wasafiri wanaoingia nchini kwa kuzingatia kanuni za afya za kimataifa (International Health Regulations -IHR). Hatua hizo zimefanikisha kuzuia ugonjwa hatari wa Ebola kutokuingia nchini. Aidha, Wizara ilipeleka Wataalam watano nchini Sierra Leone na Liberia kusaidia kukabiliana na ugonjwa wa Ebola na pia kutoa fursa ya wataalam wetu kujifunza na kupata uzoefu wa kukabiliana na ugonjwa huo ambao haujawahi kutokea hapa nchini. Napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuwa wataalam wetu wote wamerudi na wapo salama na wanaendelea kushirikiana na wataalam wengine ili kuimarisha uthibiti wa ugonjwa wa Ebola na magonjwa mengine ya mlipuko nchini.

36. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa mapya yanayojitokeza ikiwemo mafua yanayosababishwa na virusi mbalimbali. Vituo maalum vitano vilianzishwa kwa ajili ya ufuatiliaji huo katika hospitali za Kibondo (Kigoma), Sekou Toure (Mwanza), Haydom (Manyara), Mwananyamala na Kliniki ya International School of Tanganyika za Dar es Salaam. Aidha, Wataalam 280 kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa na Mbeya na sita kutoka Zanzibar walipatiwa elimu ya namna ya kujikinga na magonjwa hayo ikiwemo ugonjwa wa Ebola. Vilevile, Wizara imeboresha Maabara Kuu ya Taifa na Maabara ya Mbeya ili magonjwa hayo yaweze kuthibitishwa hapa nchini, na taratibu za kupata ithibati toka Shirika la Afya Duniani zinaendelea.

37. Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, siku za hivi karibuni nchi yetu imepokea idadi kubwa ya wakimbizi kutoka nchi ya Burundi. Hadi tarehe 25 Mei, 2015 jumla ya wakimbizi 50,829 wameingia nchini. Pamoja na hali hiyo kumetokea mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambapo hadi tarehe 25 Mei, 2015 jumla ya wagonjwa 4,435 waliripotiwa kuwa na ugonjwa huo na vifo 31 vimetokea. Serikali kupitia Wizara yangu imetoa dawa zenye thamani ya Shilingi milioni 309 ambazo zinatumika kudhibiti ugonjwa huo katika makambi ya wakimbizi hao. Aidha, wataalam wa afya 91 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamepelekwa katika kambi hizo ili kuimarisha utoaji huduma.

38. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa ya mafua ikiwemo mafua makali ya ndege katika vituo vitano maalum vilivyoanzishwa kwa ajili ya ufuatiliaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa na kudhibiti yale yanayojitokeza, kwa kuwatumia watumishi wa afya ngazi ya jamii (Community Health Workers).

39. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia programu ya Field Epidemiology Laboratory Training imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya Epidemiolojia ambapo jumla ya wanafunzi 10 walihitimu mafunzo ya miaka miwili katika ngazi ya uzamili mwaka 2014. Aidha, Wizara iliendelea kutoa na kusambaza chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa kwa kununua jumla ya chanjo 7,000 ambapo 2,000 zilisambazwa katika eneo la mradi wa majaribio wa kutokomeza kichaa cha mbwa unaotekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Morogoro na Pwani. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ilihakikisha kuwa chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa inapatikana wakati wote kupitia Bohari ya Dawa (MSD).

**Udhibiti wa Malaria**

40. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria 2014 – 2020 kwa kutekeleza afua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa malaria nchini. Kupitia afua hizo kiwango cha maambukizi ya malaria kimeshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 9.2 mwaka 2011/12. Lengo ni kufikia asilimia tano mwaka 2016. Aidha, utekelezaji wa afua mbalimbali umechangia katika kufikia kwa malengo ya milenia ambapo matumizi bora ya vyandarua pamoja na upatikanaji wa dawa umesaidia kuokoa

maisha ya watoto 60,000 ambao wangefariki kwa ugonjwa wa malaria kila mwaka. Kupungua kwa idadi ya wagonjwa kutoka wagonjwa 326 kwa kila watu 1,000 mwaka 2009 hadi kufikia wagonjwa 161 kwa kila watu 1,000 mwaka 2014.

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara ilisambaza dozi 12,911,100 za dawa mseto ya kutibu malaria na vitendanishi vyenye jumla ya vipimo 28,130,736 vya kupima malaria (mRDT), katika vituo ili kuthibitisha uwepo wa vimelea kabla ya matibabu. Aidha, Wizara iligawa vyandarua 500,000 katika shule za msingi na Sekondari za Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kupitia Programu ya Wanafunzi Shuleni. Vilevile, Wizara iliendelea na zoezi la kunyunyizia dawa ukoko ndani ya nyumba katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kufikia nyumba 400,000 ambapo takriban wananchi 2,000,000 walikingwa dhidi ya malaria katika maeneo hayo. Katika mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwa kutumia viuadudu vya kibailojia katika kata za Jiji la Dar es Salaam pamoja na miji sita iliyofanyiwa maandalizi ya Mpango huo. Miji hiyo ni Kibaha, Mwanza, Musoma, Bukoba, Shinyanga na Geita.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

42. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za kifua kikuu sugu ikiwa ni pamoja na kufanya ugatuzi wa matibabu yake, kwa kuanzisha vituo vitano vya kutoa huduma hizo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Geita na Mwanza pamoja na Zanzibar. Aidha, Wizara imekamilisha zoezi la tathmini katika migodi mitatu ya Mererani, Geita na Mwadui kwa hatua za awali za kuanzisha huduma za kuthibiti kifua kikuu katika maeneo ya migodi na machimbo. Vilevile, maabara za kifua kikuu nchini zimeboreshwa kwa kupatiwa mashine 40 za Gene-Xpert (Kiambatisho Na. 5).

43. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa matibabu ya kifua kikuu na ukoma bila malipo kwa wagonjwa wote wanaogundulika kuwa na kifua kikuu na ukoma. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 90 ya wagonjwa wa kifua kikuu walioanza matibabu wanapona, ikilinganishwa na kiwango cha uponyaji kilichowekwa na Shirika la Afya Dunia cha asilimia 85. Aidha, Wizara imeandaa mkakati na miongozo ya kuboresha huduma za kifua kikuu kwa watoto nchini. Huduma hizo zimesambazwa katika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Simiyu, Singida, Tabora, Njombe, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mwanza, Kilimanjaro, Pwani na Arusha. Kwa hivi sasa, wastani wa utambuzi wa maambukizi ya kifua kikuu kwa watoto kitaifa umeongezeka kutoka asilimia 8.6 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 10.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na kiwango kinachopendekezwa na Shirika la Afya Duniani cha utambuzi kuwa kati ya asilimia 10 hadi 15. Baada ya utambuzi huo, watoto hao waliingizwa katika mfumo wa matibabu nchini.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kupanua huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Wizara ilifanya kampeni maalum ya kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa ukoma na utambuzi wa wagonjwa wa ukoma katika Wilaya za Mkinga na Muheza Mkoani Tanga. Vilevile, Mpango Mkakati wa Tano wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (2015 – 2020) umeandaliwa. Ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana kwa urahisi, Wizara itaongeza vituo vya kutolea huduma za kifua kikuu sugu na kupanua utoaji wa huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI chini ya mfumo mmoja katika mikoa yote. Aidha, Wizara itaendelea kufanya kampeni maalum ya kuelimisha jamii kuhusu utokomezaji wa ugonjwa wa ukoma na utambuzi wa wagonjwa wa ukoma katika wilaya zenye viwango vya juu vya maambukizi zikiwemo Wilaya za Kilombero, Nanyumbu, Chato, Kisarawe na Liwale.

**Udhibiti wa UKIMWI**

45. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya, Wizara iliweka kipaumbele katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Kutokana na jitihada hizo Wizara imefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka asilimia 5.8 mwaka 2008 hadi 5.3 mwaka 2012. Aidha, kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama wajawazito kwenda kwa watoto kimepungua kutoka asilimia 26 mwaka 2010 hadi asilimia 15 mwaka 2012. Vilevile, idadi ya watu wanaopima VVU kwa hiyari imeongezeka kutoka watu 11,640 mwaka 2009 na kufikia 20,469,241 mwaka 2013. Pia, Wizara imeongeza wigo wa kuwahudumia na kuwapatia dawa za UKIMWI kutoka wagonjwa 335,292 mwaka 2010 hadi kufikia 640,084 Aprili, 2014. Aidha, Wizara imeweka kipaumbele katika afua ya tohara kwa wanaume. Kutokana na tafiti zilizopo afua hii ina matokeo makubwa ya kupunguza maambukizo ya UKIMWI kwa asilimia 60. Tangu kuanza kwa utekelezaji wa afua hii mwaka 2010, jumla ya wanaume 1,138,000 wamefanyiwa tohara ikilinganishwa na lengo la kufikia wanaume 2,102,252 ifikapo mwaka 2017.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya wa Kupambana na UKIMWI (2013-2017) kwa kutoa ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa hiari. Hadi kufikia Desemba 2014, idadi ya watu waliopima VVU ilikuwa 25,468,564 na kufanya ongezeko la watu 4,999,323 ikilinganishwa na takwimu za Desemba 2013. Aidha, Wizara imeziwezesha Kliniki 109 zinazotoa ARV kwa wanawake wajawazito wenye VVU (Option B+) ziweze pia kutoa huduma ya kupambana na UKIMWI kwa watoto wanaoishi na VVU (Kiambatisho Na. 6). Pia, huduma za wagonjwa nyumbani zimepanuliwa na kufikia watu 338,547 kati ya lengo la watu 424,298 mwaka 2014. Vilevile, Wizara itaendelea kupanua huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kufikia ongezeko la watu 7,411,619 na kutoa dawa za ARV kwa WAVIU 880,681.

47. Mheshimiwa Spika, Wizara imefikia lengo la kuwa na mashine ndogo 525 za kupima CD4 kwa ajili ya Vituo vya Afya na Zahanati. Vilevile, mashine ndogo 383 zimefungwa kifaa maalum kinachowezesha taarifa za upimaji wa CD4 na matumizi ya vitendanishi kutumwa moja kwa moja kwa njia ya mtandao kwa mfumo wa kielektroniki wa CD4LIS hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwenye kanzidata (Database) ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Katika mwaka 2015/16, wagonjwa wanaotumia dawa za ARVs wanatarajiwa kupimwa uwingi wa virusi vya UKIMWI kwa kutumia mashine maalum ambazo zitawekwa kwenye vituo vya kutolea huduma zikisaidiana na mashine kubwa zilizo katika Hospitali za Rufaa za Kanda.

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara iliendelea kutekeleza afua ya tohara kwa wanaume kama mojawapo ya afua ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI. Jumla ya wanaume 450,898 kutoka mikoa 12 yenye maambukizi ya juu ya VVU na kiwango cha chini cha tohara walitahiriwa. Mikoa hiyo ni ya Katavi, Rukwa, Mbeya, Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Geita, Mwanza, Kagera na Mara – (Wilaya ya Rorya). Kwa mwaka 2015/16 jumla ya wanaume 492,842 watafikiwa.

**Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele**

49. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kugawa dawa za kinga-tiba za magonjwa ya matende na mabusha, vikope, usubi, kichocho na minyoo ya tumbo kwa watu 22,309,588 walio na umri kati ya miaka mitano na kuendelea katika jumla ya mikoa 16 na halmashauri 101. Aidha, dawa za kinga tiba ya ugonjwa wa vikope zilisambazwa katika Halmashauri 33. Pia, Wizara ilifanya tathmini ya ugonjwa wa matende katika Wilaya za Muheza, Lushoto, Newala na Mkuranga. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha

kupungua kwa maambukizi kuwa chini ya asilimia moja na hivyo Wizara itasitisha ugawaji wa kinga-tiba ya Matende katika Wilaya hizo kuanzia mwaka 2015/16. Vilevile, huduma za udhibiti wa magonjwa hayo zilianzishwa katika Halmashauri zote za Mikoa ya Geita, Simiyu, Arusha na Kilimanjaro.

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele kwa kugawa dawa za kinga-tiba katika mikoa 20. Aidha, Wizara itaanzisha huduma ya udhibiti wa magonjwa hayo hususan kichocho na minyoo ya tumbo katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Shinyanga na Mara. Vilevile, Halmashauri 34 za Mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Tanga zilizofanikiwa kupunguza maambukizi ya matende kufikia chini ya asilimia mbili zitafanyiwa utafiti wa mwisho utakaowezesha maamuzi ya kuendelea au kusitisha kinga-tiba ya ugonjwa huo.

**Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto**

51. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya chama Tawala, Serikali imefanikiwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 454 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2010 hadi kufikia vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2012. Aidha, vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano vimepungua toka 81 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2010 hadi kufikia 54 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2013 hivyo kufikia Lengo la Maendeleo ya Milenia namba nne la kupunguza vifo vya watoto kwa theluthi mbili ifikapo mwaka 2015.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Matatizo ya Uzazi na Vifo vya Watoto (2008-2015). Katika eneo la afua za huduma za watoto, Wizara iliwajengea uwezo jumla ya watoa huduma 9,997 katika maeneo yafuatayo: stadi za kuokoa maisha ya mama na mtoto mchanga (1,391), kumhudumia mtoto mgonjwa chini ya miaka mitano (3,512), kumsaidia mtoto mchanga kupumua (4,977) na huduma za afya rafiki kwa vijana katika vituo vya kutolea huduma za afya (117). Aidha, Wizara ilipanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa waliofanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto kwa kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya 316. Vilevile, Wizara ilikamilisha mapitio ya mwongozo wa ufuatiliaji vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga katika ngazi zote na ufuatiliaji unaendelea nchi nzima.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara ilinunua na kusambaza Ambu bag/masks 3,314 na Penguin suckers 5,567 kwa ajili ya kuwahudumia watoto wachanga wanaopata tatizo la kupumua na madoli ya kufundishia 1,571 katika vituo vya kutolea huduma za afya. Vilevile, watoa huduma 3,512 walipatiwa mafunzo ya matibabu ya magonjwa ya watoto kwa uwiano katika Mikoa ya Mwanza (Magu, Misungwi, Ukerewe na Nyamagana), Kagera (Kyerwa), Kigoma (Kigoma-Ujiji, Uvinza, Kibondo, Kasulu, Buhigwe, Kakonko na Kigoma), Tabora (Tabora, Uyui, Sikonge, Kaliua, Urambo, Nzega na Igunga), Mbeya (Mbeya na Mbarali), Iringa (Iringa na Mufindi), Njombe (Njombe na Makete), Dar es Salaam (Kinondoni na Temeke) na Geita (Bukombe na Mbogwe).

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itawajengea uwezo watoa huduma jinsi ya kumhudumia mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu kwa njia ya mwambatano wa ngozi kwa ngozi ya mama na ya mtoto (Kangaroo Mother Care) katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi, pamoja na Mikoa ya Mbeya na Njombe pamoja na jinsi ya kumhudumia mtoto chini ya mwezi mmoja katika mikoa hiyo.

55. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za afya ya uzazi, Wizara imekamilisha ujenzi wa majengo ya upasuaji na wodi tatu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora

(Kitete), Hospitali za Halmashauri za Igunga, Nzega na Serengeti. Aidha, ujenzi wa nyumba nne za watumishi, majengo 12 kwa ajili ya Kliniki za Afya ya Mtoto na Uzazi na majengo sita ya wagonjwa wa nje umekamilika. Vilevile, Wizara imekamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Nyasho, Murangi, Kiagata, Ikizu, Kasahunga, Nasa, Iramba, Kinesi, Muriba, Nyarwana katika Mkoa wa Mara; Likombe, Kitere, Nanguruwe, Mahurungwa, Mahuta, Namikupa, Chihangu, Chiwale na Michiga katika Mkoa wa Mtwara; Upuge, Kitunda, Igurubi, Choma, Simbo, Nanga, Busondo, Itobo, Zogolo, Bukene, Ulyankulu na Usoke katika mkoa wa Tabora.

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Uzazi wa Mpango Uliothaminiwa (National Family Planning Costed Implementation Plan 2010 to 2015). Wizara ilinunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango nchini kote. Kiasi kipatacho Shilingi 5,000,000,000.00 zilitumika kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba vya uzazi wa mpango zikiwemo njia za vidonge vya kumeza 2,167,272; sindano vichupa 4,058,482; kondomu za kiume 27,000,000, vipandikizi 921,568 na vitanzi 349,224.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Uzazi wa Mpango Uliothaminiwa kwa kununua na kusambaza vifaa na dawa za uzazi wa mpango nchini kote. Vifaa hivyo ni kondomu za kiume 27,937,867 vitanzi 405,413, cyclebeads (shanga) 481,733 dawa za sindano vichupa 7,829,500 vipandikizi 1,767,729 na vidonge vya kumeza 3,499,667. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma 780 kutoka mikoa yote nchini kuhusu njia za kisasa za uzazi wa mpango; kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma mchanganyiko za uzazi wa mpango na afya ya uzazi kwa vijana; na kupanua wigo wa utoaji wa huduma za mkoba za uzazi wa mpango kwenye maeneo ya vijijini.

58. Mheshimiwa Spika, tatizo la saratani limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwa ka. Ili kukabiliana na tatizo hilo, katika mwaka 2014/15, Wizara imefungua vituo vipya 64 vya kutolea huduma ya uchunguzi na tiba za awali za saratani ya shingo ya kizazi katika Mikoa ya Lindi (3), Mtwara (6), Ruvuma (3), Mara (4), Tanga (2), Mbeya (10), Mwanza (5), Tabora (5), Njombe (1), Dar es Salaam (11), Arusha (1), Singida (2), Dodoma (3), Morogoro (1), Iringa (3), Shinyanga (2), na vituo viwili vipo Zanzibar. Aidha, Wizara imenunua vifaa vinavyohitajika kuchunguza saratani ya shingo ya kizazi kwa kila kituo na kuwafundisha watoa huduma za afya 213 kuhusu matumizi yake.

59. Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo (2012 - 2015) Wizara imekuwa ikitekeleza Mpango wa Kutokomeza Maambukizi ya VVU toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto 2012 - 2015. Jumla ya watoa huduma 9,896 walipatiwa mafunzo ya kutoa dawa za ARV kwa wanawake wajawazito kutoka katika mikoa yote. Kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa mwisho wa utelekezaji wa Mpango uliopo, Wizara itafanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango huo. Aidha, itahakikisha Mpango mpya wa kutokomeza maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto unatayarishwa, na kwamba huduma hii itaendelea kutolewa nchini.

60. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya, ambapo watoa huduma 300 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Mbeya, Mara na Shinyanga wamepatiwa mafunzo ili kuwawezesha kuhudumia waliofanyiwa ukatili wa kijinsia. Vituo vya kutoa huduma toshelezi (one stop centres) viliongezwa katika Mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro. Aidha, mafunzo ya namna ya ukusanyaji wa sampuli za ushahidi wa kimahakama kwa waliofanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yalitolewa kwa watoa huduma 138 wakiwemo Maafisa wa Afya, Ustawi wa Jamii, Polisi na Waendesha Mashitaka. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaongeza vituo vya kutoa huduma toshelezi katika Mkoa wa Mara, Mbeya na Dar es Salaam (Hospitali ya Taifa Muhimbili). Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu, ukusanyaji wa ushahidi wa kimahakama na rufaa kwa waliofanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

**Huduma za Chanjo**

61. Mheshimiwa Spika, viwango vya mafanikio ya chanjo vimeendelea kupanda hadi kufikia asilimia 97 kwa mwaka 2014/15. Katika kuhakikisha chanjo zinatolewa kwa ubora unaotakiwa, Wizara ilinunua vichupa vya chanjo 9,340,790 za BCG, OPV, Penta, PCV13, Rota, MR na TT vyenye jumla ya dozi 67,393,750 na majokofu 437 na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Mafunzo ya kuboresha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za chanjo yalifanyika kwa waratibu wa chanjo kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Pwani, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Morogoro. Vilevile, vituo 37 katika Mikoa ya Geita, Njombe, Tabora, Iringa, Mwanza, Arusha, Dodoma, Lindi na Manyara vilifungiwa majokofu ya umeme-jua sambamba na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa majokofu, utunzaji wa chanjo na vifaa vya kutolea chanjo.

62. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha walengwa wote wa chanjo wanafikiwa nchini, Wizara ilianzisha Mkakati wa RED/REC (Reach Every District/Reach Every Child) mwaka 2009 ukiwa na lengo la kuondoa vikwazo vyote na changamoto za utoaji wa chanjo. Mkakati huu umesaidia kupunguza idadi ya Halmashauri zilizokuwa nyuma kwenye kiwango cha chanjo kutoka 29 mwaka 2013/14 hadi 19 mwaka 2014/15. Kutokana na umuhimu wa huduma hii, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri hizo ambazo hazifanyi vizuri, waongeze juhudi za kumfikia kila mtoto, aweze kupata haki yake ya msingi ya chanjo. Aidha, mafunzo ya kuboresha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za chanjo yalifanyika kwa waratibu wa chanjo kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Pwani, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Dar es salaam na Morogoro.

63. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha chanjo mpya yenye muungano wa chanjo mbili za surua na rubella, kwa watoto wenye umri wa miezi 9 na miezi 18 ili kuwakinga dhidi ya magonjwa hayo. Katika kufikia lengo na kutekeleza mkakati wa kutokomeza magonjwa hayo hapa nchini, kampeni ya chanjo ya surua rubella ilifanyika kwa watoto wenye umri kati ya miezi 9 hadi miaka 15. Kampeni hiyo ilijumuisha afua zingine muhimu zikiwemo utoaji wa Vitamini A na dawa za kukinga magonjwa yasiyopewa kipaumbele ambayo ni minyoo ya utumbo, matende na mabusha. Pia, Kampeni hiyo ilipata mafanikio makubwa ambapo walengwa walikuwa ni watoto 21,159,130 na waliochanjwa walikuwa 20,543,364 sawa na asilimia 97.

Aidha, Wizara imeanzisha Chanjo ya HPV Mkoani Kilimanjaro kwa watoto wenye umri kati ya miaka 9 hadi 13. Chanjo hiyo ni kinga ya virusi vya HPV vinavyosababisha saratani ya shingo ya uzazi. Uanzishwaji wa chanjo hiyo umetoa mafanikio makubwa Mkoani Kilimanjaro kwa kuwafikia walengwa kwa asilimia 93. Chanjo hiyo inatarajiwa kufanyika nchi nzima ifikapo mwaka 2017. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaanza kutoa chanjo mpya ya polio kwa njia ya sindano ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Dunia wa Kutokomeza Ugonjwa wa Polio. 37 Vilevile, Wizara itabadili chanjo ya Polio kutoka Trial and Oral Polio Vaccine (tOPV) kwenda Bio Oral Polio Vaccine (bOPV) ili kutokomeza ugonjwa wa polio nchini.

**Usafi wa Mazingira**

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira. Kupitia kampeni hizo, Wizara imehamasisha jamii kujenga vyoo bora, ambapo hadi Januari 2015 jumla ya vyoo 551,806 katika kaya vimejengwa sawa na asilimia 81 ya lengo na vyoo 113 vya shule vimejengwa. Aidha, vyoo 58 vimekarabatiwa. Wizara imekamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji wa kampeni hiyo inayopanuka kutoka ngazi za kaya na shule pekee, kuelekea ngazi za vituo vya tiba, maeneo ya umma na vituo vya wasafiri. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu udhibiti wa taka ngumu na maji taka, usafi wa mifereji ya

maji ya mvua na usalama wa maji ya kunywa katika kaya. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za usafi wa mazingira katika ngazi za mikoa, halmashauri na mitaa au vijiji. Kila halmashauri nchini zitapewa usafiri wa pikipiki moja kwa ajili ya kazi hiyo.

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa taarifa utaanzishwa ili kuwezesha Sekretariati za Mikoa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati sambamba na kuhimiza ujenzi wa vichomea taka (incinerators) kwenye vituo vya tiba. Aidha, uhamasishaji wa ujenzi wa matundu ya vyoo bora shuleni yanayotosheleza mahitaji utaimarishwa.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya Semina maalum ya uhamasishaji kwa Makatibu Tawala wa Mikoa 23 ya Tanzania Bara kuhusu udhibiti wa taka ngumu, pamoja na mafunzo kwa Maafisa Afya wa Manispaa 16 na Majiji matano juu ya matumizi ya kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009. Aidha, Wizara imehamasisha waratibu wa afua ya afya kazini katika mikoa 10 na halmashauri 85 kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU, kifua kikuu na homa ya ini. Vilevile, imesambaza nakala 470 za Mkakati wa Pili wa Kuzuia Maambukizi ya magonjwa hayo. Pia, Wizara, imetoa mafunzo kwa waratibu na waelimishaji rika 50 katika ngazi ya Wizara na Mikoa minne ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Pwani kuhusu kuzuia na kudhibiti maambukizi ya VVU, kifua kikuu, pamoja na magonjwa mengine katika sehemu za kazi kwa watumishi wa sekta ya afya.

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kutoa huduma na kuimarisha vituo vya afya katika bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi kavu kwa madhumuni ya kujikinga na magonjwa yanayotolewa taarifa kimataifa na athari nyingine za kiafya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Wizara ya Maji inatarajia kutekeleza mradi wa majaribio juu ya kuhimili athari za kiafya zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma kwa kufanya uhamasishaji wa viongozi wa ngazi ya mkoa na halmashauri. Vilevile, machapisho ya vielelezo yanayolenga kutoa elimu ya jinsi ya kuhimili athari za kiafya zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi yataandaliwa na kugawiwa katika maeneo ya miradi.

**Elimu ya Afya kwa Umma**

68. Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa Mwongozo wa Kisera (2015) na Mkakati wa Huduma za Uelimishaji (2015 – 2020) pamoja na mafunzo elekezi kwa timu za uelimishaji wa huduma za afya katika halmashauri na mikoa. Mafunzo hayo yalihusu jinsi ya kupanga, kuratibu, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini huduma za elimu ya afya yalihusisha Mkoa wa Iringa, Halmashauri za wilaya za Iringa na Mufindi; Mkoa wa Mbeya, Halmashauri za Wilaya za Mbarali na Mbeya na mkoa wa Njombe, Halmashauri za Wilaya za Makete na Njombe Vijijini. Aidha, Wizara iliendelea kuboresha huduma za afya ngazi ya jamii kwa kuwasilisha Mwongozo wa Kisera wa Huduma za Afya (2014) na Mkakati wa Huduma za Afya ngazi ya Jamii (2015 – 2020) kwa wadau na Timu za Uendeshaji za Huduma za Afya za Halmashauri zote za Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Vilevile, machapisho ya uelimishaji jamii kuhusu magonjwa mbalimbali ikiwemo Ebola yalitayarishwa na kusambazwa nchi nzima ikijumuisha vituo vya afya mipakani, bandari na viwanja vya ndege. Pia, Wizara imekuwa ikitoa matamko wakati wa maadhimisho na sherehe mbalimbali kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya hali ya utoaji wa huduma za afya nchini pamoja na mikakati iliyopo ya kuimarisha afya za wananchi.

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao na kufanya uchunguzi wa afya ikiwemo saratani ya tezi dume. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu matibabu ya nimonia na kuharisha kwa watoto wadogo kulingana na ushauri wa watoa huduma. Vilevile, njia mbalimbali zikiwemo

uraghibishi, kampeni, kusambaza vipeperushi, ujumbe mfupi wa simu, matangazo ya televisheni na radio, vijarida, mabango na njia za mawasiliano za asili zitatumika. Pia, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za afya za Mikoa na Halmashauri katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Simiyu, Kagera na Geita iliyolengwa katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

**Huduma za Lishe**

70. Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Taifa wa Lishe ambao ulizinduliwa mwaka 2011 umekuwa ukitekelezwa kwa njia ya ushirikishwaji wadau mbalimbali, ndani na nje ya sekta ya afya. Aidha, tathmini ya mkakati huo umeonyesha mafanikio yakiwemo kuajiri Maafisa Lishe katika wilaya 157 na kuingiza masuala ya lishe katika Sekta ya kilimo hususan kwenye korido ya Kusini ya kilimo (SAGCOT) kwa kutumia sekta binafsi. Pia, Taasisi imeendelea kutekeleza mpango wa ugatuaji wa majukumu kwenda ngazi ya halmashauri.

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara na wadau wake ilipanua wigo wa kutoa huduma za lishe kwa kuongeza virutubishi hasa kwa watoto chini ya miaka mitano na wanawake walio kwenye umri wa kuzaa maeneo ya vijijini. Aidha, Wizara ilisimamia Mradi wa Majaribio wa Kuongeza Virutubishi unaoendelea kutekelezwa katika Halmashauri sita za Iringa vijijini, Kilolo, Njombe Mji, Karatu, Monduli na Meru kuanzia mwezi wa Desemba, 2014 hadi Machi, 2015. Katika mradi huo, Wizara ilifanya uhakiki wa kuangalia usindikaji na njia zinazotumika kuongeza virutubishi. Pia, iliwajengea uwezo waratibu wote wa Lishe na wasindikaji unga wa mahindi ngazi ya vijiji namna ya kufanya tathmini na uhakiki kama viwango vimefikiwa.

72. Mheshimiwa Spika, Wizara imehamasisha na kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya virutubishi nyongeza ambapo jumla ya watu 13,341 kutoka vijiji 55 vya Halmashauri hizo walifaidika na uhamasishaji huo. Kati ya hao, 2,120 ni wanawake wenye watoto ambao walifundishwa namna ya kuongeza virutubishi kwenye chakula cha watoto na kuwalisha. Pia, Wizara itaendelea kupanua wigo wa upatakanaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwa maeneo mengine nchini hususani yale yenye utapiamlo mkali. Vilevile, Wizara itawaongezea utaalam wamiliki wa viwanda na vinu vya kusagia mahindi ili waongeze virutubishi katika vyakula.

73. Mheshimiwa Spika, kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe, Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa 875 wakiwemo maafisa Lishe na Mipango pamoja na waratibu wa chanjo katika halmashauri 164 na mikoa yote kuhusu uingizaji wa afua za lishe katika mipango na bajeti zao. Vilevile, Taasisi iliratibu programu maalum ya mafunzo kwa waratibu wa lishe 168 katika ngazi za mikoa na halmashauri. Programu hiyo ililenga kuwajengea uwezo wa kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini shughuli za lishe kwa ufanisi zaidi. Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe ilitoa mafunzo ya ulishaji wa watoto wachanga na watoto wadogo kwa watoa huduma za afya 239 katika vituo vya afya na jamii kutoka katika Halmashauri za Mbarali, Makete, Njombe, Mufindi, Iringa, Mbeya, Karagwe, Kyerwa na Misenyi. Katika mwaka 2015/16, Taasisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya mafunzo kwa kuwahusisha wataalam wa kada za lishe 250 katika ngazi za mikoa na halmashauri ambao hawakupata mafunzo hayo.

74. Mheshimiwa Spika, Taasisi imepanua wigo wa mradi wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula ngazi ya Taifa kwa kuongeza viwanda vinavyoongeza virutubishi kwenye vyakula kutoka tisa hadi 13. Viwanda vyenye mitambo ya kuongeza virutubishi kwa sasa ni pamoja na Coast Millers; S.S. Bakhressa Co Ltd (Buguruni); S.S. Bakhressa Co Ltd (Kipawa); S.S. Bakhressa Co Ltd (Mzizima); Azania Wheat Flour (Kipawa); Azania Wheat Flour (Ubungo); 21 st Century (Kurasini, Sinza); Pembe Flour Mills (Tanga); Monaban Farming and Trading Ltd (Arusha); East Coast Oil, Fats and Soaps Ltd; BIDCO na Murzah Oil Mills (DSM). Aidha, Taasisi ilifanya ufuatiliaji

wa uwekaji madini joto kwenye chumvi kwenye mashamba 78 katika Halmashauri za Singida, Iramba, Manyoni, Meatu, Babati, Hanang, Uvinza, Rufiji, Bagamoyo, Mkuranga, Bahi, Chamwino, Manispaa za Singida, Temeke, Kinondoni na Dodoma. Jumla ya wazalishaji chumvi 288 walipata mafunzo kuhusu uwekaji wa madini joto kwenye chumvi. Katika mwaka 2015/16, viwanda 16 zaidi vya vyakula vitaanza utekelezaji wa mpango huo.

75. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa ushirikiano na Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanya utafiti wa hali ya lishe nchini kwa kutumia mbinu ijulikanayo kama "SMART". Utafiti huo ulijumuisha mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar ukihusisha watoto 16,984 wenye umri chini ya miaka mitano na wanawake zaidi ya 16,000 walio katika umri wa kuzaa kutoka katika kaya 20,799. Matokeo ya utafiti huo ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwaka 2010 yalibainisha kupungua kwa wastani wa viwango vya kitaifa vya utapiamlo kwa watoto kwa viashiria vya udumavu, ukondefu na uzito pungufu.

Aidha, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa udumavu umepungua kutoka asilimia 42 hadi 35, ukondefu kutoka asilimia tano hadi nne na uzito pungufu kutoka asilimia 16 hadi 13. Kwa upande wa wanawake walio katika umri wa kuzaa, utafiti huo umeonesha tatizo la uzito uliokithiri (kiribatumbo) ni kubwa katika Mikoa ya Kilimanjaro (asilimia 22) na Dar es Salaam (asilimia 21) (Kiambatisho Na. 7).

76. Mheshimiwa Spika, pamoja na kupungua kwa viwango hivyo bado kuna zaidi ya watoto milioni 2.7 wamedumaa, 446,000 wana ukondefu na 106,000 wanaokabiliwa na utapiamlo mkali. Aidha, viwango vya udumavu katika Mikoa tisa ni vya juu sana kwa mujibu wa vigezo vya Shirika la Afya Duniani. Mikoa hiyo ni Kagera (52%), Njombe (52%), Iringa (51%), Ruvuma (49%), Kigoma (49%), Rukwa (48%), Geita (46%), Dodoma (45%) na Katavi (43%). Vilevile, Mikoa 10 imebainika kuwa na kaya nyingi ambazo hazitumii chumvi yenye madini joto huku Mikoa ya Lindi (5.9%) na Mtwara (12.6%) ikionesha kiwango kidogo zaidi cha matumizi ya chumvi yenye madini joto. Mikoa mingine ni Tabora (19.5%), Rukwa (21.2%), Geita (22.2%), Ruvuma (25%), Shinyanga (29.8%), Singida (32.0%), Simiyu (34.3%) na Kagera (49.6%). Mikoa saba tu ndiyo ilionesha kuwa na viwango vya zaidi ya asilimia 90 ya kaya zinazotumia chumvi yenye madini joto ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Dar-es-Salaam, Mbeya, Kigoma na Mwanza.

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe na kwa kushirikiana na wadau itafanya ufuatiliaji wa kina kubaini sababu za viwango vya udumavu kuendelea kuwa ni vya juu sana hususan katika mikoa ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini. Aidha, kwa kuwa lishe ni suala mtambuka Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Chakula na Lishe Tanzania ya mwaka 1992 kwa lengo la kutoa mwongozo wa kitaifa kuhusu masuala ya lishe kwenye hatua za makuzi katika maisha na magonjwa pamoja na kuimarisha uratibu wa shughuli zinazotekelezwa na wadau mbalimbali wa lishe. Wizara pia itaandaa Mpango wa Taifa kuhusu masuala ya Lishe kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo.

78. Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe kuwa, jukumu la kuhakikisha kuwa jamii inapata lishe bora ni letu sote, hivyo kila mdau ashiriki katika kutimiza azma hii. Napenda kutoa pongezi kwa Wabunge wanaopigania haki za watoto, lishe na uhakika wa chakula, kwani wamekuwa mstari wa mbele katika kuleta ushawishi wa kutokomeza utapiamlo nchini.

**HUDUMA ZA TIBA**

79. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI imeendelea kuboresha huduma za tiba kwa kutekeleza MMAM. Katika utekelezaji wa Mpango huo vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 6,260 mwaka 2010 hadi 7,014 mwaka 2015

(Kiambatisho Na.8). Aidha, katika kipindi hiki Serikali imefanikiwa kuanzisha huduma mpya za kibingwa na uchunguzi hapa nchini na kuwawezesha wananchi kupata huduma za kibingwa ambazo awali zilikuwa hazitolewi hapa nchini. Huduma hizo ni pamoja na upasuaji mkubwa wa moyo, upasuaji wa mgongo na ubongo, kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo na uanzishaji wa huduma za dharura pamoja na ununuzi wa mashine za kisasa za matibabu mbalimbali ikiwemo tiba ya saratani kwa kutumia mionzi. Ongezeko hilo la vituo na uanzishwaji wa huduma hizi za kibingwa limeongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**Huduma za Tiba katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda**

80. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Ibara ya 86(g) Wizara imeendelea kuboresha huduma za rufaa katika Hospitali ya Taifa, Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda. Maboresho hayo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo pamoja na usimikaji wa mitambo kwa ajili ya kuimarisha huduma mbalimbali za tiba.

81. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani Ocean Road iliendelea kutoa huduma za kinga, uchunguzi na tiba ambapo jumla ya wagonjwa 15,976 walihudumiwa na kati yao wapya walikuwa 3,267. Jumla ya wanawake 6,452 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti ambapo 516 walibainika kuwa na dalili za awali za saratani ya shingo ya kizazi na 129 walibainika kuwa na dalili za saratani ya matiti na kuendelea na uchunguzi. Aidha, huduma za kinga, uchunguzi na matibabu ya saratani na tiba shufaa zimeendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 1,897 wamepata huduma katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015. Katika kuboresha huduma za uchunguzi na tiba ya saratani, Wizara imenunua mtambo wa uchunguzi na tiba ya saratani aina ya Linear Accelerator (LINAC) na ufungaji wa mtambo huo unaendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea na ujenzi wa jengo la kusimika mashine mbili mpya na za kisasa za LINAC na CT Simulator na kubadilisha chanzo cha mionzi katika mashine ya mionzi ya Equinox 80 na kununua mashine za tiba kwa mionzi (LINAC) kwa ajili ya huduma ya matibabu ya saratani katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

82. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kujenga uwezo wa kutoa huduma za kibingwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya uchunguzi na tiba ya saratani na upasuaji mifupa kwa kuanzisha program za mafunzo kwa masomo ya Shahada ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi na Shahada ya Uzamili katika Tiba ya Sayansi ya Saratani kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Jumla ya wanafunzi 33 wa shahada ya kwanza na nane wa Shahada ya Uzamili wamepata mafunzo ya kuchunguza na kutibu saratani.

83. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuimarisha huduma za tiba za kibingwa katika Hospitali ya Taifa, Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda ili kupunguza idadi ya vifo, na gharama za kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa uchunguzi na matibabu. Jumla ya wagonjwa 164 walifanyiwa upasuaji wa moyo katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando (41) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (61). Pia, Cath lab procedures 62 zilifanyika katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Vilevile, wagonjwa 98 walifanyiwa upasuaji maalum kwa kutumia tundu dogo (Laparascopic surgery) na Hospitali ilipata tuzo ya upasuaji bora iliyotolewa na British Medical Award.

84. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wanapata huduma za kibingwa, Wizara inaendelea na mpango wa kuleta Madaktari Bingwa nchini. Mwaka 2014/15 wataalam bingwa 28 kutoka Marekani na India waliletwa na kutoa huduma za mishipa ya damu iliyoziba ambapo wagonjwa 19 walihudumiwa; ambapo huduma hii ilitolewa kwa mara ya kwanza Afrika ya Mashariki. Aidha, wataalam bingwa wa upasuaji wa moyo kutoka India walitoa huduma kwa watoto 12 wenye magonjwa ya moyo kwa kuwafanyia

upasuaji mkubwa. Wataalam hao walitoa huduma hizo kwa kushirikiana na Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Taifa Muhimbili. Vilevile, Wataalam 33 kutoka Saudi Arabia chini ya ufadhili wa DHI Nurevn Islamic Foundation wakishirikiana na madaktari bingwa wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 66 ambapo kati yao wagonjwa 23 walifanyiwa upasuaji mkubwa na Cathetarization kwa wagonjwa 43. Utaratibu huo umeokoa jumla ya Shilingi bilioni 1.3 ambazo zingetumika kugharamia matibabu ya wagonjwa ambao wangepelekwa nje ya nchi. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za upasuaji wa moyo na kuanzisha Taasisi ya Moyo Muhimbili inayojitegemea badala ya utaratibu wa sasa wa kituo hicho kuwa chini ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

85. Mheshimiwa Spika, mashine mpya tano za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo zimenunuliwa na kufanya idadi ya mashine zilizopo kuwa 16. Aidha, wagonjwa 76 walipata huduma za tiba ya figo kupitia huduma ya kuchuja damu kwa mizunguko 6,066 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Pia, wagonjwa 35 walihudumiwa katika Kituo cha kutolea huduma za afya Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuboresha huduma hizi ili wagonjwa wengi zaidi wanufaike na huduma za kusafisha damu na kuweka juhudi za kufikia lengo la kupandikiza figo hapa nchini.

86. Mheshimiwa Spika, jengo la mradi wa awamu ya tatu la Taasisi ya Mifupa Muhimbili limekamilika kwa kiwango cha asilimia 95. Matarajio ni kukamilisha jengo hilo kwa asilimia 100 ifikapo Julai 2015. Kukamilika kwa jengo hilo kutaboresha huduma katika maeneo ya kufanyia vipimo, matibabu ya upasuaji wa ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Aidha, huduma hizo zitapunguza idadi ya wagonjwa wa mifupa, tiba za ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo wanaopewa rufaa kwenda kupata matibabu hayo nje ya nchi.

87. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mifupa Muhimbili ilifanya upasuaji wa nyonga na kuweka viungo bandia kwa wagonjwa 250 na goti kwa wagonjwa 60. Aidha, upasuaji ulifanyika kwa watoto 558 wenye vichwa vikubwa, wagonjwa 165 wa ubongo na wagonjwa 312 wa uti wa mgongo na mishipa ya fahamu. Vilevile, Taasisi ya Mifupa Muhimbili ilitoa huduma za kibingwa za mkoba katika Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando na Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro, ambapo jumla ya wagonjwa 513 walihudumiwa na kati yao 116 walifanyiwa upasuaji.

88. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mirembe ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili 1,848 waliolazwa na 13,500 walihudumiwa na kurudi nyumbani. Aidha, jumla ya wagonjwa wa akili wahalifu wapya 194 walihudumiwa na Taasisi ya Isanga na 40 walipata ruhusa kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria na kurudishwa makwao. Vilevile, Hospitali ya Mirembe imehudumia wagonjwa wa magonjwa ya kawaida 47,640. Pia, Wizara iliendelea kutoa huduma ya Methadone kwa waathirika wa kujidunga dawa za kulevya. Jumla ya waathirika 2,297 walihudumiwa ambapo kati ya hao 946 walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, 440 Hospitali ya Temeke na 911 Hospitali ya Mwananyamala. Aidha, Wizara itatoa elimu ya huduma ya Methadone kwa wafanyakazi na kuanzisha huduma ya Methadone katika Hospitali ya Mirembe.

89. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15 Wizara iliboresha maabara za Hospitali za Kanda KCMC na Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Maboresho hayo yamewezesha maabara za Muhimbili na KCMC zimepewa Ithibati ya Ubora wa huduma za maabara kwa viwango vya kimataifa. Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, ukarabati wa maabara ya uchunguzi wa vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa Ebola umekamilika. Vilevile, katika hospitali ya KCMC ujenzi wa jengo la huduma za dharura umekamilika kwa asilimia 52. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar itahakikisha kuwa Maabara ya

Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja Zanzibar inapata ithibati ya ubora wa huduma za maabara kwa viwango vya kimataifa.

90. Mheshimiwa Spika, Wizara ilisambaza na kufunga mashine za kutibia meno katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Manyara, Tabora, Temeke na Tumbi. Pia, mashine za X- Ray zilisambazwa katika Hospitali ya KCMC, Vyuo vya Tabibu meno vya Tanga na Mbeya. Aidha, Wizara ilisambaza dawa za ganzi kwa tiba ya magonjwa ya kinywa kwa mikoa yote 25. Vilevile Wizara ilifanya matengenezo kinga ya vifaa vya kutibia meno katika kliniki za meno katika Mikoa ya Tanga (Hospitali ya Mkoa), Chuo cha Meno Tanga, Njombe (Vituo vya Afya vya Wanging'ombe na Lupembe na Zahanati ya Mtwango), Temeke (Hospitali ya Vijibweni, Kituo cha Afya Zakhem, Kituo cha Afya Kitunda na Zahanati ya Yombo) na Hospitali ya Mwananyamala. Katika mwaka 2015/16, Wizara itanunua na kusambaza viti na mashine za kutibia meno katika Hospitali za Rufaa za Mikoa za Mtwara, Kagera, Dar es Salaam - Amana na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Aidha, Wizara itanunua na kusambaza dawa za tiba ya meno katika vituo vyote vya umma vyenye kliniki za meno. Pia, Wizara itafanya matengenezo kinga na tiba ya vifaa vya kutibia meno vya kliniki za meno katika Mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Tabora na Mtwara.

91. Mheshimiwa Spika, Wizara imendelea kufanya maboresho ya uhakiki wa maabara ili kupata matokeo sahihi ya vipimo vya maabara kwa kuzingatia utaratibu wa ithibati kwa viwango vya kimataifa. Jumla ya maabara 48 zilijumuishwa katika utaratibu wa kuhakikiwa ambapo maabara 26 zilitunukiwa nyota kati ya moja hadi tatu za ubora wa huduma. Mafundi wanne wa vifaa tiba walipata mafunzo na kupatiwa vifaa kwa ajili ya matengezo ya BioSafety Cabinets za maabara. Katika mwaka 2015/16 jumla ya maabara 18 zitaingia katika mchakato wa uhakiki.

92. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Kibong'oto iliendelea kutoa huduma za tiba ambapo wagonjwa 19,234 walihudumiwa. Kati yao 840 ni wagonjwa wa kifua kikuu na UKIMWI na 120 wa kifua kikuu sugu. Aidha, hospitali iliendelea na mafunzo maalum kwa wataalam 25 wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini. Mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa watoa huduma hizo nchini kote. Katika mwaka 2015/16, Hospitali itaendelea kuhudumia wagonjwa wanaougua kifua kikuu, kifua kikuu sugu, UKIMWI na wagonjwa wengineo.

93. Mheshimiwa Spika, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Mtambo mkubwa wa Oksjeni kwa ajili ya huduma za tiba umenunuliwa na ufungaji wa mtambo huo unaendelea. Aidha, katika udhibiti wa taka hatarishi, kichomea taka kilinunuliwa na kusimikwa. Pia, ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti umekamilika sambamba na kununua majokofu ya kuhifadhia maiti yenye uwezo wa kulaza maiti 60 kwa mara moja.

94. Mheshimiwa Spika, mahitaji halisi ya damu nchini ni wastani wa chupa 450,000 kwa mwaka. Mikakati ya kufikia lengo hili ni pamoja na kujenga vituo vya ukusanyaji wa damu kwa kila mkoa na kila Halmashauri; hivyo natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutenga bajeti ya ukusanyaji wa damu katika bajeti zao. Wizara iliendelea kuratibu upatikanaji wa damu salama ambapo jumla ya chupa 162,367 za damu zilikusanywa ikilinganishwa na chupa 160,000 zilizopangwa kukusanywa. Aidha, asilimia 35 ya damu iliyopatikana ilitokana na wachangiaji wa kudumu. Pamoja na kufikia lengo, kiasi kilichokusanywa ni asilimia 40 ya mahitaji ya nchi.

Natoa wito kwa wadau wote tushirikiane kuchangia damu kwa hiari. Vilevile, klabu za kuchangia damu zilizo ndani na nje ya shule zitaendelea kuimarishwa. Kwa mwaka 2015/16, Wizara imetenga Shilingi 4,776,011,200.00 kwa ajili ya kununulia vitendanishi na mahitaji muhimu ya Mpango wa Damu Salama, hapo awali mpango huo ulikuwa ukipata uhisani wa Wadau wa Maendeleo.

95. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuwezesha utekelezaji na uboreshaji wa ushirikiano na Sekta Binafsi ambapo kufikia sasa asilimia 73 ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini vinamilikiwa na Serikali na asilimia 27 ni vya Sekta Binafsi. Aidha, halmashauri nyingine nne zimeingia mikataba ya utoaji huduma za afya na vituo vya kutolea huduma na kufanya jumla ya halmashauri 65 kuwa na mikataba na vituo 68 vya binafsi vingi vikiwa vya mashirika ya dini.

96. Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuboresha huduma za afya kwa wazee katika Halmashauri zote. Juhudi hizo, zimeiwezesha Tanzania kushika nafasi ya pili baada ya Mauritius katika nchi 11 za bara la Afrika zilizofanyiwa tathmini ya utoaji wa huduma bora za afya kwa wazee ya mwaka 2014 (Global AgeWatch Index Report). Nchi nyingine za Bara la Afrika zilizoshiriki ni pamoja na Afrika Kusini, Morocco, Ghana, Nigeria, Rwanda, Zambia, Uganda, Malawi na Msumbiji. Tathmini hii hufanywa kila mwaka na Shirika la Kimataifa linaloitwa Help Age International.

97. Mheshimiwa Spika, mikutano minne kati ya Wizara na vyama vya waganga wa tiba asili na waganga wa tiba mbadala ilifanyika kwa lengo la kuwaelimisha juu ya Sheria, Kanuni, Miongozo na namna bora ya kutoa huduma ya tiba asili. Mikutano hiyo iliwezesha kuanzishwa kwa Shirikisho la Vyama vya Waganga wa Tiba Asili na Chama cha Waganga wa Tiba Mbadala ili kurahisisha usimamizi na uratibu wa huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini. Aidha, elimu juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya tiba asili na tiba mbadala ilitolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari mbali mbali. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Tiba Asili na Tiba Mbadala.

**Huduma za Dawa**

98. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya Shilingi 228,720,505,813.00 zimetumika kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa Shilingi 47,346,193,082.00 ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 24,617,026,082.00 zilitumika kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kiasi kilichobaki cha Shilingi 22,729,167,000.00 kilitumika kulipa deni la MSD. Aidha, Wadau wa Maendeleo walitoa kiasi cha Shilingi 181,374,312,731.00 ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 10,500,000,000.00 zilitoka kwa wadau wa Mfuko wa Pamoja na Shilingi 170,874,312,731.00 zilitoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ambao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

99. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 jumla ya Shilingi 336,002,706,847.00 zimetengwa kwa ajili ya kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa Shilingi 85,380,393,000.00 na Shilingi 18,662,343,250.00 zitatokana na asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uchangiaji wa huduma za afya katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, Shilingi 231,959,970,597.00 zitatolewa na Wadau wa Maendeleo.

100. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Serikali imeendelea kudhibiti upotevu wa dawa ambapo Bohari ya Dawa imeweza kuweka nembo ya GOT kwenye aina 65 za dawa ambayo ni sawa na asilimia 50 ya utekelezaji wa lengo lililopangwa. Aidha, Bohari ya Dawa imekamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika Mikoa ya Tanga na Tabora yenye ukubwa wa mita za mraba 4,500 ambayo ni asilimia 60 ya lengo. Ujenzi wa maghala hayo umepunguza gharama za ukodishwaji wa maghala katika mikoa hiyo.

101. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha upatikanaji wa dawa, Wizara imeanza kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya ununuzi wa dawa pale ambapo bidhaa hizo zitakosekana

Bohari ya Dawa. Jumla ya Washitiri binafsi 18 katika mikoa tisa wamepatikana ili kuwezesha upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Bohari ya Dawa itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa karibu na wananchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Mpango huo utahusisha kutumia waagizaji wa dawa binafsi 18 nchi nzima ili kutoa dawa kwa vituo vya afya pale ambapo zinakosekana Bohari ya Dawa. Aidha, ili kulinda ubora wa dawa kabla ya kumfikia mwananchi, dawa hizo zitapitia mfumo wa ubora wa Bohari ya Dawa ambao unaendana na viwango vya kimataifa vya ISO 9001:2008.

102. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Bohari ya Dawa itakamilisha taratibu za kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya uzalishaji wa dawa na vifaa tiba ambavyo malighafi zake zinapatikana hapa nchini kama vile pamba kwa ajili ya uzalishaji wa Gauze na Cotton wool. Ukamilishwaji wa utaratibu huo utaipunguzia Serikali matumizi ya fedha za kigeni kununulia dawa na vifaa tiba nje ya nchi na hivyo kufupisha muda wa kupatikana kwa dawa na vifaa tiba. Bohari ya Dawa itaboresha mfumo wa usambazaji wa dawa hadi vituo vya kutolea huduma za afya kwa madhumuni ya kupunguza gharama. Ili kufanikisha hilo, Bohari itatekeleza mfumo wa kufupisha mzunguko wa usambazaji kwa kutumia mfumo wa Supply Chain Guru unaobainisha mzunguko ulio mfupi katika kugawa dawa ndani ya Halmashauri.

103. Mheshimiwa Spika, Wizara imeboresha taarifa za ugavi na usambazaji wa dawa kwa njia ya kielektroniki na kufanya uhamasishaji wa utumiaji wa mfumo huo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zote nchini. Aidha, mafunzo ya ugavi na usambazaji wa shehena za dawa kwa njia ya mtandao umefanyika katika Halmashauri zote nchini na hivyo uagizaji wa dawa unafanyika kwa njia ya mtandao. Mfumo huo umeboresha uwasilishwaji wa taarifa na mahitaji ya vituo kwa wakati na uwazi zaidi. Vilevile, Wizara itaendelea na utoaji wa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo katika ngazi ya hospitali.

**UBORA WA HUDUMA ZA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

104. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara ilifanya usimamizi shirikishi katika Hospitali 50 zilizopata mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wajumbe 538 wa Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri, Timu za Menejimenti za Hospitali na Timu za Uimarishaji Ubora katika Hospitali za Halmashauri kwenye Mikoa mipya minne ambayo ni Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Vilevile, Timu za Menejimenti za Hospitali katika ngazi ya Halmashauri katika Mkoa wa Lindi zimepata mafunzo kuhusu kukinga na kudhibiti maambukizo ya magonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya utoaji salama wa sampuli za damu kwa wataalam 549 katika Hospitali ya MOI, Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, KCMC na Bugando. Pia, mafunzo hayo yalitolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mtwara (Ligula), Pwani (Tumbi), Dar es Salaam (Amana na Mwananyamala), Ruvuma (Songea), Lindi (Sokoine), Kigoma (Maweni), Arusha (Mount Meru), Mwanza (Sekou Toure), Shinyanga, Tabora (Kitete), Singida, Kilimanjaro (Mawenzi), Tanga (Bombo), Mbeya na Iringa. Vilevile, Wizara iliendelea kupanua shughuli za Utoaji Cheti Hatua-kwa-Hatua kuelekea Ithibati katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Iringa na Njombe ili kuimarisha huduma za afya. Jumla ya vituo 28 vimefikiwa Hospitali za Rufaa ngazi ya Mkoa vinne, Hospitali ngazi ya Halmashauri 18 na Vituo vya Afya sita, na vyote viko kwenye ngazi ya kwanza.

105. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa kwa kuanza kufanya tathimini kwa vituo vyote vinavyotoa huduma za afya ya msingi kwa kuanzia na Mikoa 12 ya Dar es Salaam, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Singida, na Tabora. Vituo vitapewa hadhi ya nyota

moja hadi tano kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Mipango ya uboreshaji huduma itaandaliwa na vituo kuitekeleza kwa kupatiwa msaada wa kitaalamu kutoka Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri.

106. Mheshimiwa Spika, Wizara itatoa mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo kwa wajumbe 300 wa Timu za Uimarishaji Ubora wa huduma za afya katika Mikoa mitano ya Pwani, Tanga, Ruvuma, Shinyanga na Mtwara. Aidha, Wizara itafanya tathimini ya utekelezaji wa viwango vya kukinga na kudhibiti maambukizo katika hospitali zote zilizopata mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo na itatoa mafunzo ya utoaji salama wa sampuli za damu kwa watoa huduma za afya 300 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa za Maweni, Ligula, Mawenzi, Mbeya, Mount Meru, Shinyanga, Sekou Toure, Ruvuma, Mwananyamala na Tumbi. Pia, Wizara itafanya usimamizi shirikishi kwenye Mikoa 12 ya Dodoma, Katavi, Geita, Kilimanjaro, Simiyu, Njombe, Morogoro, Mbeya, Iringa, Rukwa, Tabora na Shinyanga.

107. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza jitihada za kuimarisha huduma za afya zinazotolewa na kuhakikisha kuwa zinakidhi viwango vya kimataifa kwa kuendelea kutekeleza mpango wa Utoaji Cheti Hatua-kwa-Hatua kuelekea Ithibati. Mpango huu unaotumia viwango vya SafeCare kwa vituo vya afya ya msingi ambavyo vimepatiwa hadhi ya nyota tatu na kuendelea wakati wa tathimini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itakamilisha mwongozo utakaoelekeza namna ya kumsimamia mwanafunzi wa Uuguzi na Ukunga anapokuwa akijifunza kwa vitendo katika maeneo ya kutolea huduma. Aidha, Wizara itakamilisha mwongozo wa kisera unaoelekeza uanzishwaji wa maabara maalum (skills lab) za kufundishia Wauguzi na Wakunga. Lengo la uanzishwaji wa miongozo hiyo ni kutoa fursa kwa wanafunzi kusimamiwa kwa umakini wanapokuwa katika mazoezi kwa vitendo.

109. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa Timu za Maafa za Mikoa katika Mikoa ya Njombe na Iringa. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya namna ya kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola ambao umezikumba nchi za Afrika Magharibi. Vilevile, Wizara imeratibu shughuli za kukabiliana na maafa ya mafuriko yaliyo zikumba sehemu mbalimbali ikiwemo Mikoa ya Shinyanga na Morogoro. Katika mwaka wa 2015/16, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na maafa na dharura mbalimbali nchini ikiwemo kutoa mafunzo kwa Timu za Maafa za Mikoa na Halmashauri.

110. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia mabaraza ya taaluma ilisimamia maadili na kusajili wataalam waliokidhi viwango vya kutoa huduma za afya nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2015, jumla ya wataalam 9,123 walisajiliwa kupitia mabaraza yao ya kitaaluma (Kiambatisho Na 9). Mabaraza hayo ni pamoja na Madaktari na Madaktari wa Meno, Uuguzi na Ukunga, Famasia, Maabara, Upeo wa Macho Kuona na Afya ya Mazingira. Aidha, katika mwaka 2015/16 Wizara itawasilisha mapendekezo ya sheria mpya ya Madaktari ambapo sheria inayotumika sasa ni ya mwaka 1959 ambayo ni ya muda mrefu.

111. Mheshimiwa Spika, Wizara ilisajili vituo binafsi vya kutolea huduma za afya 98, vituo vya kutolea huduma ya Optometria na maduka yanayosambaza na kuuza vifaa vya Optometria tisa, vituo vya tiba asili na tiba mbadala 74, maabara binafsi za afya 117, taasisi zinazotoa huduma za afya ya mazingira 23. Aidha, Wizara kupitia Baraza la Famasi imesajili vyuo vinne vinavyotoa kozi katika ngazi ya cheti na vyuo vitatu vinavyotoa kozi ya mwaka mmoja (pharmaceutical dispensers) ambavyo ni vya wamiliki binafsi. Vilevile, Baraza la Famasi limetoa mafunzo kwa watoa dawa 692 wa maduka ya dawa muhimu na wamiliki wa maduka ya dawa muhimu 886. Pia, Baraza la Famasi limesajili maduka mapya 106 ya dawa moto, maduka 490 ya dawa muhimu na maghala matatu ya kuhifadhia dawa. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa

vituo vipya vinaanza kutoa huduma kwa wananchi mapema mara baada ya kukamilika ili kuendelea kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Hivyo, Wizara inafanyia kazi taratibu zinazotumika ili kuondoa changamoto zinazochelewesha usajili wa vituo vya kutolea huduma. Kwa kuwa taratibu za usajili zinaanzia katika Halmashauri husika, ninatoa wito kwa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha wanakamilisha tararibu zote zinazotakiwa mapema ili kukamilisha usajili kwa wakati.

112. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Dawa za Asili Muhimbili lilitoa mafunzo kwa waganga wa Tiba Asili 54 kuhusu lishe bora, usafi, kuandaa dawa za asili na namna bora ya kumhudumia mgonjwa. Aidha, Baraza liliondoa mabango 1,128 ya waganga wa tiba asili katika maeneo mbalimbali yanayokinzana na Sheria; Na. 23 ya mwaka 2012 iliyoanzisha Tiba Asili na Tiba Mbadala ambayo inakataza matangazo yanayopotosha wananchi kuhusu matibabu ya magojwa. Kati ya hayo mabango hayo yaliondolewa katika Manispaa za Temeke (248), Ilala (580) na Kinondoni (300). Vilevile, zoezi hilo pia, lilifanyika katika Jiji la Mbeya kwa mafanikio makubwa. Zoezi hilo ni endelevu na litatekelezwa katika mikoa yote nchini. Pia, Baraza lilifanya ufuatiliaji wa huduma za tiba asili katika Mikoa ya Njombe, Singida na Dar es Salaam na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo mbalimbali kwa waratibu 17 wa mikoa hiyo pamoja na baadhi ya waganga 290 wa tiba asili.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Baraza la Madaktari ilipitisha Hospitali za Rufaa za Mkoa za St. Gaspar (Itigi), Tumbi (Pwani) na Songea (Ruvuma) kutoa mafunzo kwa vitendo kwa madaktari wapya na hivyo kufanya hospitali zinazotoa mafunzo kwa vitendo kufikia 20. Aidha, Baraza liliandaa Mwongozo wa mafunzo kwa vitendo kwa Madaktari na Madaktari wa meno na kusambaza jumla ya nakala 1800 za mwongozo huo.

114. Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 4/2014 la Itifaki ya kuanzisha Tume ya Utafiti wa Afya ya Afrika Mashariki lilipitishwa na Bunge na kuidhinishwa na Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara iliandaa Kanuni ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto, marekebisho ya Kanuni ya Makao ya Watoto, Kanuni za Sheria ya Udhibiti wa Kemikali za Viwandani, Kanuni za Afya ya Jamii Kuhusu Usimamizi wa Uchafu na utunzaji wa Mabaki ya Binadamu, Kanuni za Usimamizi wa Bidhaa za Tumbaku na Kanuni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwenye mahabusi za watoto.

115. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utaratibu wa kufanya mabadiliko ya Sheria iliyoanzisha Bohari ya Dawa ili kuiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka 2015/16, Wizara itawasilisha Muswada wa Sheria ya Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali na Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Kemia ili usomwe Bungeni kwa mara ya pili. Aidha, Wizara itawasilisha Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219. Vilevile, itaandaa Kanuni chini ya Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kanuni chini ya Sheria ya Usimamizi wa Hospitali Binafsi na Kanuni nyingine za Sheria za Afya na Ustawi wa Jamii.

**HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

116. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu, kutoa na kusimamia huduma za ustawi wa jamii kwa makundi maalum ambayo ni wazee, watu wenye ulemavu, watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto walio katika mkinzano na sheria, familia zenye migogoro ya ndoa na familia zenye dhiki.

**Huduma kwa Wazee na Watu Wenye Ulemavu**

117. Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi zikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu na unasihi kwa wazee na watu wenye ulemavu wasiojiweza 869 wanaotunzwa na kulelewa katika makazi 17 ya Serikali. Kati yao wanaume ni 408 na wanawake 461. Aidha, Wizara iliratibu huduma za matunzo katika makazi 24 yanayoendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika kufanikisha utengamao wa wazee na watu wenye ulemavu, Wizara imewezesha kujengwa kwa nyumba 42 za bei nafuu kwa kushirikisha jamii na kuwatengamanisha wakazi 110 katika jamii kwenye makazi ya Nandanga (Wilaya ya Lindi) na Mkaseka (Wilaya ya Masasi).

118. Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha inaboresha huduma za wazee, ikiwemo kuanzisha taaluma maalum za wazee (Geatric care) katika Chuo Kikuu cha Sayansi Shirikishi cha Muhimbili. Awali taaluma hii ya kibingwa ilikuwa haipo nchini, hivyo kwa kutambua umuhimu wa wazee tumeanzisha ili kuboresha huduma za matibabu kwa wazee. Aidha, napenda kuzipongeza Halmashauri za Kilindi, Pangani, Iramba, Songea, Tarime na Kaliua ambazo zimechukua jukumu la kuwalipia Wazee kadi za CHF ili kuhakikisha wanapata huduma za afya wanapozihitaji bila kikwazo cha fedha. Naomba kuchukua nafasi hii kuwakumbusha kuwa jukumu la kuwahudumia wazee ni la Halmashauri, Hivyo ni vyema Halmashuri zikajipanga kwa kuwalipia au kutoa huduma bila malipo kwa wazee.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba kudhoofika kwa mfumo wa kinga ya jamii kumechangia mmomonyoko wa maadili na kupungua kwa huduma ya matunzo, na hadhi ya wazee katika jamii. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaimarisha na kurahisisha upatikanaji wa haki na huduma kwa wazee na matunzo stahiki katika makazi kwa ajili ya wazee waliokosa ndugu na jamaa wa kuwatunza.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wazee, Watu wenye ulemavu, fimbo nyeupe na watu wenye ualbino. Maadhimisho yanaweka msisitizo kwa jamii kuachana na mila potofu zinazowanyima haki watu wenye ulemavu ikiwemo haki ya kuishi, kushiriki katika masuala ya kijamii na kupewa ulinzi. Haki hizo zitapatikana kwa kujenga mazingira yasiyokuwa na vikwazo katika jamii. Aidha, hivi karibuni kumejitokeza tena wimbi la mauaji ya watu wenye ualbino, vitendo vinavyofanywa kwa imani zinazohusishwa na ushirikina. Vitendo hivyo ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na ni fedheha kwa Taifa letu. Nachukua fursa hii kulaani desturi hiyo na kuiasa jamii na wananchi kwa ujumla kuachana na imani hizo potofu zinazohatarisha maisha ya watanzania wenzetu. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wake itaandaa mkakati madhubuti wa uelimishaji wa Jamii dhidi ya vitendo viovu kwa watu wenye ualbino.

121. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo ya marekebisho na utengamao kwa Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka katika Halmashauri za Wilaya za Mvomero, Kilombero, Ruangwa, Dodoma, Nkasi, Masasi, Manyoni, Biharamulo na Sumbawanga (Hospitali ya Mkoa wa Rukwa). Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa kuandaa na kuratibu mipango ya kuwahudumia watu wenye ulemavu. Vilevile, mafunzo hayo yatazijengea Halmashauri uwezo wa kupanga mipango inayozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika jamii. Wizara imeweka suala la marekebisho na utengamao katika Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015-2020) ili kuweka misingi ya kiutekelezaji katika halmashauri.

122. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo jumuishi kwa watu wenye ulemavu katika vyuo vya Yombo Dar es Salaam na Chuo cha Wasioona Singida ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Jumla ya vijana 63 wamehitimu; kati yao wanawake ni 34 na wanaume 29. Aidha, jumla ya vijana 110 wanaendelea na mafunzo ikiwa wanawake ni 51 na

wanaume 59. Vilevile, Wizara imekarabati miundombinu ya vyoo, na mabweni katika Chuo cha Wasioona Singida na kukifanya kuwa rafiki zaidi kwa watu wenye ulemavu.

**Huduma za Ustawi wa Familia, Watoto, Malezi na Maendeleo ya Awali ya Watoto Wadogo**

123. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ulinzi na usalama kwa watoto, Wizara ilitoa mafunzo ya ulinzi na usalama wa watoto kwa maafisa ustawi wa jamii na Timu za Ulinzi na Usalama. Mafunzo hayo yalitolewa katika Halmashauri za Shinyanga, Mkuranga, Kibaha, Same, Muleba, Karatu, Bagamoyo, Kisarawe, Kahama na Manispaa ya Shinyanga na Iringa, na Jiji la Arusha na Mbeya. Hadi kufikia mwezi Machi 2015 jumla ya halmashauri 30 zimewezeshwa kuanzisha Mfumo wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto. Aidha, Wizara imesambaza na kutoa mafunzo ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi (2013-2017) na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009 na kanuni zake kwa watendaji wakuu katika halmashauri 37 (Kiambatisho Na.10).

124. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto umesaidia kuongeza uelewa wa jamii kuhusu haki ya kupata ulinzi na matunzo kutoka kwa Jamii. Mafanikio hayo yanaonekana kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaojitokeza kufichua vitendo vya unyanyasaji, ukatili, udhalilishaji na unyonyaji kwa watoto. Aidha, jumla ya matukio 3,449 yameripotiwa katika Halmashauri za Manispaa za Temeke, Ilemela, Ilala, Kinondoni na Nyamagana ukilinganisha na matukio 2,250 yaliyoripotiwa katika mwaka 2013/14. Vilevile, jumla ya matukio 3,206 yameripotiwa kwa njia ya simu maalum ukilinganisha na matukio 2,362 kwa mwaka 2013/14.

125. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto, Wizara ilifanya kongamano la watoto walio katika mazingira hatarishi. Washiriki 172 walitoka Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali, 119 walitoka Mashirika yasiyo ya kiserikali na 47 wawakilishi wa watoto walitoka Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mwanza, Dar es salaam, Mara, Pwani, Kigoma na Iringa inayotekeleza mpango huo. Aidha, kongamano hilo lilitanguliwa na maadhimisho ya wiki ya ulinzi na usalama wa mtoto katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa, Hai, Bukoba, Kisarawe, Kibaha, Magu, Shinyanga, Kasulu, Tandahimba, Nanyumbu, Masasi, Newala na Mtwara; Manispaa za Kinondoni, Ilala, Temeke, Musoma, Ilemela, Nyamagana, Shinyanga na Mtwara; na Miji ya Njombe na Masasi.

126. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu, kutoa na kusimamia huduma ya malezi ya kambo na kuasili ambapo jumla ya mashauri 105 yalipokelewa na jumla ya watoto 80 wapo katika malezi ya kambo na watoto 25 waliasiliwa. Katika kuimarisha na kuboresha mahusiano katika familia, Wizara imeendelea kuratibu huduma za unasihi, usuluhishi na upatanishi katika mashauri ya ndoa zenye mifarakano na migogoro katika Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii. Jumla ya mashauri 150 yalipokelewa, 30 yalisuluhishwa, 45 yalipelekwa mahakamani na 75 yanaendelea kusikilizwa.

127. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walezi 600 wanaotoa huduma katika makao ya watoto na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na vyuo vya malezi ya watoto vinavyoendeshwa na watu binafsi pamoja na mashirika. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo vya malezi ya watoto. Pia, jumla ya vituo 51 vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo viwili vya malezi vilisajiliwa.

128. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuanzisha mifumo ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika halmashauri 13 na kuendesha mafunzo kwa Timu za Ulinzi na

Usalama za Mtoto na maafisa ustawi wa jamii. Aidha, Wizara itaendelea kusambaza na kutoa mafunzo kwa watendaji wakuu katika halmashauri zilizobaki kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa II wa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi (2013 - 2017). Aidha, Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009 na kanuni zake zitasambazwa ili kuboresha utoaji wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.

**Huduma za Haki za Mtoto na Marekebisho ya Tabia**

129. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia na kuratibu huduma zitolewazo kwa watoto walio katika mkinzano na sheria. Wizara imehudumia jumla ya watoto 337 wakiwemo wavulana 304 na wasichana 33 waliohifadhiwa katika mahabusu za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es salaam na shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Aidha, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wanaohudumia watoto walio katika mkinzano na sheria, ambapo watumishi 133 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, na mahabusu za watoto Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es salaam na shule ya Maadilisho Irambo walipatiwa mafunzo kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya utoaji huduma. Katika mwaka 2015/16, Wizara itatoa mafunzo kwa wawezeshaji 20 katika Jiji la Mbeya na Manispaa ya Temeke ambao watatumika kutoa mafunzo kwa wasaidizi 67 wa watoto walio katika mkinzano na sheria wawapo mahakamani.

**UDHIBITI WA KEMIKALI NCHINI**

130. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya Sampuli 10,974. Sampuli 3,260 zilikuwa za vyakula, dawa, kemikali, maji na maji taka, bidhaa za viwandani na mazingira. Kati ya hizo sampuli 2,658 ambazo ni sawa na asilimia 82 zilichunguzwa na kutolewa matokeo. Sampuli nyingine 7,714 zilikuwa za makosa ya jinai, kati ya hizo sampuli 6,318 ambazo ni sawa na asilimia 82 zilichunguzwa na kutolewa matokeo.

131. Mheshimiwa Spika, Wakala ulitoa mafunzo kuhusu Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Sura 182 juu ya matumizi na usafirishaji salama wa kemikali kwa wadau 655. Aidha, mafunzo kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Teknolojia ya Vinasaba vya Binadamu Sura 73 yalitolewa kwa wadau 703. Mafunzo hayo yalihusu uelewa wa taratibu za uchukuaji, ufungaji, uhifadhi na usafirishaji wa sampuli na vielelezo vinavyohitaji uchunguzi wa kimaabara wa Sayansi Jinai. Vilevile, vyombo vya habari na njia mbalimbali za mawasiliano zilitumika kuelimisha jamii kuhusu Sheria hizo.

132. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ulitekeleza mradi wa kuzuia na kudhibiti ajali zinazohusisha kemikali ili kuepusha madhara kwa binadamu na uharibifu wa mazingira na mali. Aidha, jumla ya vituo 20 vya mipakani vilikaguliwa na jumla ya mizigo 9,683 ya kemikali iliruhusiwa kuingizwa nchini baada ya kukidhi matakwa ya sheria.

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wakala itaendelea na hatua za mwisho za kupata ithibati kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Aidha, Wakala utajenga jengo kwa ajili ya Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya na kufanya ukarabati wa jengo la Maabara ya Vinasaba vya Binadamu. Vilevile, jengo la Maabara ya Kanda ya Mashariki Makao Makuu Dar es Salaam litakarabatiwa.

**UDHIBITI WA UBORA WA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA**

134. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua

maeneo 6,484 yanayohusika na uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na ya kusindika chakula 1,484, sehemu za kuuzia chakula 2,630, maduka ya dawa 1,582, vituo vya afya 328, maduka ya vipodozi 1,992, maduka ya vifaa tiba 42, viwanda vya dawa nje ya nchi 76, viwanda vya dawa vya ndani vinne na viwanda vya vipodozi vinane. Kati ya maeneo 6,484 yaliyokaguliwa, maeneo 5,624 yalikidhi vigezo sawa na asilimia 87. Maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya Sheria, wamiliki walielekezwa kufanya marekibisho husika ndani ya muda maalum.

135. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Chakula na Dawa ilisajili na kuhuisha vibali vya maeneo 5,912 ya kufanyia biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Aidha, Mamlaka ilitathmini na kusajili aina 2,608 za chakula, 2,264 za dawa, 914 za vipodozi, 56 vifaa tiba na dawa 16 za majaribio. Vilevile, Mamlaka ilitoa vibali 8,982 vya kuingiza bidhaa nchini na 1,180 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

136. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu; hii ni pamoja na tani 60 za chakula zenye thamani ya Shilingi 120,998,636, tani 73 za dawa zenye thamani ya Shilingi 1,339,724,344 na tani 8.82 za vipodozi zenye thamani ya Shilingi 46,407,304. Ili kuhakikisha kuwa jamii inatumia chakula salama na bora, Wizara itakamilisha Sera ya Chakula Salama na kuisambaza kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini. Sera hiyo itasaidia kuweka mkazo kwenye ukaguzi wa maeneo ya kutayarisha, kusafirisha, kuhifadhi au kuuzia chakula kwa kuyakagua na kuyaboresha zaidi.

Aidha, Mamlaka ilichunguza sampuli 4,714 ambapo 1,854 zilikuwa za dawa, 2,676 za chakula, 106 za vifaa tiba na 78 za vipodozi. Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli 4,573 zilikidhi viwango sawa na asilimia 97. Bidhaa ambazo hazikukidhi vigezo ziliondolewa katika soko na baadhi zilikataliwa au kufutiwa usajili. Baadhi ya dawa hizo ni pamoja na dawa ya kutibu fangasi ya Ketokonagoli, dawa ya malaria ya maji na vidonge aina ya Amodiaquine. Dawa zote za kikohozi zenye kiambato hai cha Phemlypopanolamine, dawa ya sindano ya Chloromphemicol Sodium Succinate inayotengenezwa na Kiwanda cha Lincolin Pharmaceutical Limited India na dawa ya maji kapsulin aina ya Cloxacillin.

137. Mheshimiwa Spika, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa umma kupitia radio, televisheni, magazeti, mikutano na imeanza utaratibu wa kutembelea Taasisi za elimu ambapo shule 16 za msingi na sekondari katika Mkoa wa Dar es Salaam zilipatiwa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipodozi.

Aidha, Mamlaka ilipokea na kutathmini taarifa 206 za madhara yaliyohisiwa kutokana na matumizi ya dawa. Tathmini ilibaini kuwa madhara hayo hayakuwa na uhusiano na matumizi ya dawa. Vilevile, watoa huduma za afya 202 na wajumbe 56 wa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa katika Mikoa ya Kigoma, Tabora, na Singida walipewa mafunzo juu ya kukusanya taarifa za madhara ya dawa. Pia, Mamlaka imeanza ujenzi wa ofisi na maabara ya Kanda ya Ziwa katika Jiji la Mwanza. Ili kuhakikisha kuwa jamii inatumia chakula salama na bora, Wizara itakamilisha Sera ya Chakula Salama na kuisambaza kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini. Sera hiyo itasaidia kuweka mkazo kwenye ukaguzi wa maeneo ya kutayarisha, kusafirisha, kuhifadhi au kuuzia chakula kwa kuyakagua na kuyaboresha zaidi.

138. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa inaendelea kutekeleza Mpango wa Uwianisho wa Taratibu za Udhibiti wa Dawa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliozinduliwa mwaka 2012. Mpango huo ambao ni wa kwanza kutekelezwa katika Bara la Afrika, ulianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu na zilizo bora, salama na fanisi katika nchi wanachama kwa kutumia mifumo ya pamoja. Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Mpango ilimalizika

tarehe 31 Desemba, 2014, ambapo miongozo ya tathmini na usajili wa dawa, utengenezaji bora wa dawa na mifumo ya uhakiki ubora wa huduma zinazotolewa na Mamlaka za Udhibiti wa Dawa za Nchi wanachama iliyowianishwa (harmonized guidelines) na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya mwezi Septemba, 2014. Miongozo hiyo imeanza kutumika na Mamlaka za Udhibiti wa Dawa za nchi wanachama kuanzia tarehe 1 Januari, 2015.

139. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Awamu ya Pili ya Mpango, itazingatia kutoa mafunzo kwa watatalaam wa tathmini na usajili wa dawa (Drug Assessors) pamoja na ukaguzi wa viwanda vya dawa (Drug Inspectors). Vilevile, tathmini za pamoja za dawa na ukaguzi wa viwanda vya dawa kwa lengo la kusajili dawa zilizoombewa usajili kwa utaratibu wa pamoja (joint assessment and inspection procedures) ili kuongeza upatikanaji wa dawa bora, salamu na fanisi katika nchi wanachama. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa kushirikiana na wataalam kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na Taasisi ya Udhibiti Dawa ya Uswisi (SWISSMEDIC). Pia, katika kipindi hiki, Mpango utapanua wigo wake ambapo utekelezaji wa uwianisho wa mifumo ya udhibiti wa madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, ufuatiliaji wa ubora wa dawa katika soko na udhibiti wa vifaa tiba na vitendanishi utaimarishwa. Kwa upande wa Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa itaendelea na utekelezaji wa mpango wa uwianisho wa mifumo ya udhibiti wa dawa kwa nchi za SADC sanjari na ule wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU**

140. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, imekamilisha ufuatiliaji kuhusu njia bora za kutibu maji katika Wilaya za Geita na Kisarawe. Matokeo ya utafiti huo yamewezesha kuandaa mpango wa uhamasishaji kuhusu usalama wa maji ngazi ya kaya kitaifa ikiwa ni moja ya kinga muhimu dhidi ya magonjwa ya kuhara. Aidha, Wizara imeandaa Mpango kazi wa kuhamasisha tiba za maji ngazi ya kaya na kujenga kituo cha mafunzo ya vyoo bora katika kijiji cha Katoma wilayani Geita. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita imekamilisha uhamasishaji katika vitongoji vyote vya kijiji cha Katoma na kuanzisha Kamati za Vitongoji ili kusaidia Kamati ya Kijiji katika udhibiti wa mazingira na tayari wananchi wameshaanza ujenzi wa vyoo bora.

141. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa kushirikiana na Mpango wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele ilifanya utafiti wa ufuatiliaji wa ugonjwa wa matende na mabusha katika Wilaya za Lushoto, Muheza, Mkuranga, Newala na Tandahimba. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa katika wilaya hizo maambukizi yamepungua chini ya asilimia moja na hivyo ugawaji wa dawa utasitishwa katika maeneo hayo. Aidha, utafiti wa matende na mabusha ulifanyika katika wilaya 35 za Mikoa ya Iringa, Rukwa, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Singida, Ruvuma na Njombe. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa maambukizi ya ugonjwa yamepungua chini ya asilimia mbili. Vilevile, utafiti wa ugonjwa wa vikope uliendelea katika wilaya 19 ambapo matokeo yameonesha Wilaya saba za Kilindi, Tunduru, Kongwa, Mpwapwa, Chemba, Meatu na Bahi bado zitahitaji umezeshaji dawa kwa kinga-tiba. Pia, utafiti wa awali katika wilaya 19 umeonesha kuwa ni Wilaya moja tu ya Chunya itahitaji kuanza zoezi la ugawaji wa dawa za ugonjwa wa vikope.

142. Mheshimiwa Spika, Taasisi ilifanya utafiti wa majaribio ya dawa za kudhibiti VVU ili kutathmini ubora wa dawa mpya ijulikanayo kama FOZIVUDINE iliyo katika mseto wa dawa zitakazotumika kwa wagonjwa wanaoanza dawa na wale wanaojenga usugu wa dawa za kundi la kwanza. Utafiti huo umeshakamilika na sasa uchambuzi wa takwimu unaendelea. Katika mwaka 2015/16, Taasisi itaendelea kufanya utafiti wa kufupisha tiba ya kifua kikuu na za kutafuta namna bora ya kugundua vimelea vya kifua kikuu. Katika kipindi hicho utafiti utafanyika kwa kushirikiana na nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Utafiti wa

NC005 utahusisha nchi za Afrika Kusini na Uganda na utafiti wa NC006 utahusisha nchi za Afrika Kusini, Zambia, Kenya na Uganda. Aidha, Taasisi itaendelea kufanya tafiti za dawa za kutibu uti wa mgongo kwa wagonjwa wenye VVU na utafiti wa kubaini kiwango cha maambukizi ya kichocho na minyoo ya tumbo katika Wilaya za Rorya na Butiama mkoani Mara.

**USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI**

143. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini. Aidha, iliratibu na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda za SADC, EAC, ECSA- HC na mashirika mengine ya kitaifa na katika kutekeleza maamuzi ya pamoja yenye manufaa kwa taifa. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, itaimarisha ushirikiano na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya za kitaifa na kimataifa. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, Malaria Afrika, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Wazee, Albino, Watu Wenye Ulemavu, Kutotumia Tumbaku, Tiba Asili ya Mwafrika, Wachangia Damu, Utepe Mweupe, Siku ya Wauguzi na Fimbo Nyeupe.

**SHUKRANI**

144. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), na Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF na UNFPA kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Pia, napenda kuzishukuru nchi nyingine za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa njia mbalimbali.

145. Mheshimiwa Spika, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), GAVI, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine ya Marekani, Canadian Bar Association, CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), JICA, KOICA, KfW, Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF),MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na UNWomen.

146. Mheshimiwa Spika, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorcerciasis Control, Africare, Axios International, Aids Relief Consortium, AIHA, ASCP, ASM, APHL, Balm and Gillead Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief Services (CRS), Citi Bank, Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), Global Fund, General

Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital- London, Save the Children, SightSavers International, Supply Chain Management Systems (SCMS) na University of Columbia, URC, USAPresidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.

147. Mheshimiwa Spika, niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, CCBRT, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, MUKIKUTE, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya.

148. Mheshimiwa Spika, navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na ustawi wa jamii.

149. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa toka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe (Mb.), Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu Dkt. Donan William Mmbando kwa kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu katika kipindi hiki. Vilevile, nawashukuru Dkt. Margaret Evelyn Mhando, Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Bwana Rabikira Onaufoo Mushi, Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nawashukuru pia, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa, na Wakurugenzi wa Hospitali Maalum na za Rufaa za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo ya Afya na Ustawi wa Jamii na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mashirika ya Dini, ya Kujitolea na Binafsi. Natoa shukurani kwa sekta nyingine ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendelee kuzingatia misingi ya afya bora ili hatimaye waweze kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

150. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu. Kipekee namshukuru mke wangu mpenzi Mariam S. Abdulaziz na watoto wetu Tariq, Meyye, Shekhan na Amour kwa uvumilivu na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa

wananchi wa Jimbo la Rufiji nawashukuru kwa ushirikiano mnaoendelea kunipatia katika kuendeleza Jimbo na naahidi nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo letu la Rufiji.

**MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2015/16**
**Mapato**

151. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya Shilingi 122,309,541,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 114,830,753,000.00 zitakusanywa katika mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na Shilingi 7,478,788,000.00 ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na Mabaraza ya Kitaaluma.

**Matumizi ya Kawaida**

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 369,358,418,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 133,003,758,000.00 zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 236,354,660,000.00 zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara Shilingi 43,952,857,000.00 ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii - Makao Makuu na Shilingi 192,401,803,000.00 ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

**Miradi ya Maendeleo**

153. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 444,618,452,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni Shilingi 70,000,000,000.00 na fedha za nje ni Shilingi 374,618,452,000.00. Kati ya fedha hizo za nje, Shilingi 12,567,233,000.00 zitatolewa na wadau wa maendeleo wanaochangia kupitia mfuko wa pamoja na Shilingi 362,051,219,000.00 zitatolewa na wadau walio nje ya mfuko wa pamoja.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2015/16**

154. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka 2015/16, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Taasisi zake yenye jumla ya Shilingi 813,976,870,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 369,358,418,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 444,618,452,000.00 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

155. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; www.moh.go.tz. 156. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii! Mwakilishi wake, Mheshimiwa Martha Umbulla, una nusu saa (dakika 30).

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa edha 2014/2015 na maoni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kama Ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA- (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa taarifa hii, nitoe pole nyingi kwa wananchi wa Mkoa wa Manyara hususan Wilaya ya Mbulu, Kata ya Gehandu kwa kufiwa na Diwani wao kupitia Chama cha Mapinduzi, ndugu Isack Bayo ambaye pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba kutoa taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na maoni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilizuru kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za Wizara na taasisi zake ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na wahusika. Pia Kamati ilikagua miradi ya maendeleo katika taasisi hizo ambayo iliidhinishiwa fedha katika mwaka huu wa fedha. Miongoni mwa taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*, Taasisi ya Saratani *Ocean Road,* Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(MOI)*, Kitengo cha Magonjwa ya Moyo Muhimbili, Kituo cha Mtangamao wa Waathirika wa Dawa za Kulevya cha Itega na Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na Dodoma.

Aidha, mwezi Aprili mwaka huu, Kamati ya Huduma za Jamii ilipata fursa ya kutembelea moja ya Hospitali za Kundi la Apollo iliyopo New Delhi, nchini India kwa lengo la kuangalia huduma za tiba ambazo zinatolewa kwa wagonjwa wa Tanzania wanaopelekwa katika hospitali hizo. Kundi la Hospitali za Apollo lina makubaliano ya kimkataba na Serikali ya Tanzania, yanayowezesha hospitali hizo kupokea wagonjwa kutoka Tanzania ambao wanapata rufaa ya kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 01 Aprili na tarehe 08 Mei, 2015, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahsusi yafuatayo:-

Moja, utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015,

Pili, utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Tatu, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Nne, makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara pamoja na maeneo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekti, utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilibaini kwamba, kwa sehemu kubwa Wizara

imezingatia ushauri uliotolewa jambo ambalo limewezeshwa kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:-

Kwanza, kupungua kwa utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kuongeza tengeo la fedha za ndani. Fedha ya maendeleo inayotokana na vyanzo vya ndani imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 19 katika mwaka wa fedha mwaka 2012/2013 hadi kufikia shilingi bilioni 70 katika mwaka 2015/2016. Kamati inapongeza hatua hii ya kuweza kuongeza bajeti ya ndani ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 350 ndani ya kipindi cha miaka minne ya bajeti (2012/2013 hadi 2015/2016). Ni imani ya Kamati kwamba, iwapo utaratibu huu utaendelea, tutapunguza utegemezi wa fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa.

Pili, kuongezeka kwa ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya taasisi za Wizara kutokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki. Mfumo huu umewezesha baadhi ya taasisi kuvuka lengo la makusanyo. Kwa mfano, Hospitali ya Rufaa Mbeya imeongeza makusanyo kutoka Shilingi milioni 50 kwa mwezi hadi Shilingi milioni 500.

Tatu, kuongezeka kwa tengeo la fedha za mradi wa Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto kutoka Shilingi bilioni 14.5 zilizoombwa hadi kufikia Shilingi bilioni 19.5. Hii ni ishara kwamba, Wizara inatambua umuhimu wa eneo hilo kupewa bajeti ya kutosha.

Nne, kukamilika kwa matengenezo ya mashine mbili za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo, bado kuna maeneo yanayokabiliwa na changamoto na hivyo Kamati inashauri yafanyiwe kazi kama ifuatavyo:-

Kwanza, fedha za uendeshaji kutolewa pungufu, kucheleweshwa ama kutotolewa kabisa na hivyo kuathiri uendeshaji wa hospitali, vyuo vya mafunzo na huduma za ustawi wa jamii.

Pili, ongezeko la idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa kwa ajili ya kugharamia matibabu hayo. Hali hii imesababisha deni la matibabu katika Hospitali za Apollo kufikia Dola za Marekani milioni 9.2 hadi Machi, 2015.

Tatu, bajeti ndogo kwa ajili ya wahitaji wa huduma za ustawi wa jamii wakiwemo wazee, watu wenye ulemavu na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Nne, kupungua kwa fedha za wadau wa maendeleo katika sekta ya afya jambo ambalo limeathiri ununuzi wa dawa, vifaa tiba, vifaa vitendanishi na chanjo.

Tano, fedha ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani kuchelewa au kutolewa kwa kiasi kidogo jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi na kusababisha ongezeko la gharama za miradi hii na baadhi ya wakandarasi kuishitaki Serikali kwa kutowalipa madeni.

Sita, kuendelea kuongezeka kwa deni la Serikali kwa Bohari ya Dawa (*MSD*) ambapo hadi Machi, 2015 lilikuwa limefikia Shilingi bilioni 108.6. Hali hii inaiathiri *MSD* katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Saba, kuboresha huduma za matibabu ya saratani nchini na kuiwezesha Hospitali ya *Ocean Road* kufanya kazi kikamilifu. Upatikanaji wa watumishi katika sekta ya afya hususan

maeneo ya pembezoni, huduma za bima ya afya kwa wananchi wote na utolewaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu nchini ikiwemo wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013/2014: Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 659.8, ambapo kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 354 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida *(recurrent expenditure)* na shilingi milioni 305.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 328 sawa na asilimia 58.4 ya bajeti yote iliyotengwa. Kati ya kiasi hicho kilichotolewa, Shilingi bilioni 254.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 90.9 ya fedha zilizotengwa. Kwa upande mwingine fedha zilizopokelewa katika maendeleo ni Shilingi bilioni 73.8 sawa na asilimia 26.1 ya bajeti yote iliyotengwa katika maendeleo._Kati ya fedha ya maendeleo iliyopokelewa, Shilingi bilioni 8.8 ni kutoka fedha za ndani ikiwa ni asilimia 16.3 tu…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, punguzeni kelele!

**MHE. MARTHA J. UMBULLA- (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA YA JAMII):** ..ya tengeo la ndani la Shilingi bilioni 54.

**MWENYEKITI:** Utulivu!

**MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA YA JAMII):** Fedha za nje zilizopokelewa ni Shilingi bilioni 73.8, sawa na asilimia 26.8 ya fedha za nje kwenye maendeleo ambazo zilikuwa Shilingi bilioni 251.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha iliyopokelewa na Wizara hadi Machi, 2015 ilikuwa asilimia 58.4 tu, Kamati inasikitishwa na mwenendo huo wa fedha. Aidha, inahoji ni kwa vipi Hazina itaweza kutoa asilimia 41.6 iliyosalia katika kipindi cha robo iliyosalia kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha wakati imetoa asilimia 58.4 tu ya bajeti ya Wizara katika robo tatu zilizopita!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukusanyaji wa maduhuli hadi Machi, 2015 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 70.4, sawa na asilimia 74 ya lengo lake ambalo lilikuwa Shilingi bilioni 94.6 na kiwango hicho cha ukusanyaji ni pungufu kwa asilimia 15 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita ambayo yalifikia asilimia 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili sekta ya afya nchini: Kamati ikitathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya afya nchini zikiwamo zifuatazo:-

Moja, kuendelea kukua kwa deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ambapo hadi mwaka 2015 lilikuwa Shilingi bilioni 108.

Pili, bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuendelea kuwa chini ya kiwango kwa asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Azimio la Abuja la Mwaka 2001.

Tatu, utendaji wa *MSD* kuhitaji uimarishwe.

Nne, Wizara kuendelea kudaiwa na wakandarasi ambao wanatoa huduma mbalimbali kwa Wizara na taasisi zake.

Tano, Wizara kuendelea kutegemea sehemu kubwa ya fedha za maendeleo zaidi ya asilimia 82 kutoka vyanzo vya nje.

Sita, ongezeko la wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa.

Saba, kuendelea kukua kwa deni la Serikali kwa Hospitali za Apollo nchini India ambazo zinapokea wagonjwa kutoka Tanzania; na

Nane, fedha za maendeleo kutotolewa kwa wakati ambapo hadi Machi, 2015 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 26.1 ya fedha zilizotengwa. Pia, kusuasua kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), upungufu wa watumishi wa sekta ya afya nchini hasa katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa nchi yetu. Pia, upatikanaji duni wa huduma za Afya ya Mama na Mtoto ikiwemo utoaji wa huduma za uzazi salama na mpango mkakati wa kuzuia vifo vya mama na mtoto. Kutoeleweka hasa ni kiasi gani kinatengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo. Vilevile, gharama kubwa za matibabu kwa wagonjwa wa saratani na Figo na mwisho bajeti finyu kwa Idara ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016: Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekusudia kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi 122,218,398,500/= ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 23 ikilinganishwa na malengo ya mwaka 2014/2015. Aidha, ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 813.9, ambapo kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 444.6 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 369.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujadili taarifa ya makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2015/2016, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Wizara imeongezeka kwa takribani Shilingi bilioni 191 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2014/2015. Kamati inaipongeza hatua hii, hata hivyo bado inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya hadi kufikia lengo la asilimia 15 la bajeti ya Taifa kwa mujibu wa Azimio la Abuja la mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini kwamba, Wizara imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha Idara ya Huduma ya Uuguzi na Ukunga ambayo imetengewa Shilingi bilioni 422.3 na Kitengo cha Huduma za Dawa *(Pharmaceutical Services Unit)* ambacho kimetengewa Shilingi bilioni 36.6 ili kusimamia na kuboresha huduma za upatikanaji wa dawa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ni matumaini ya Kamati kwamba, kuanzishwa kwa maeneo haya mapya ya kibajeti yataleta ufanisi zaidi na kuimarisha huduma katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inasikitishwa na hatua ya baadhi ya vifungu kupunguziwa fedha katika mwaka ujao wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Vifungu hivyo ni pamoja na Huduma za Kinga ambacho bajeti yake imepungua kutoka Shilingi bilioni 275.6 mwaka wa fedha 2014/2015 hadi Shilingi bilioni 246.3 mwaka ujao wa fedha. Kamati inashauri kwamba, ni vyema Wizara ikahakikisha hatua hiyo haileti madhara kwa maeneo yaliyoguswa na hatimaye kuathiri utoaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati: Pamoja na kujadili makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2014/2015, Kamati inatoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya sekta ya sfya na Azimio la Abuja: Itakumbukwa kwamba, nchi yetu ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo ni Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zimeridhia Azimio la Abuja linalozitaka nchi wanachama kuongeza bajeti katika sekta ya afya hadi kufikia asilimia 15 ya bajeti ya Serikali ifikapo mwaka 2015. Huu ukiwa ni mwaka wa mwisho wa kufikia lengo hilo, ni wazi kwamba, hakuna dalili za nchi yetu kufikia kiwango cha asilimia 15 cha bajeti ya Serikali kuelekezwa katika sekta ya afya. Ushahidi unaonyesha kupitia mwenendo wa ongezeko la bajeti ya sekta ya afya katika miaka mitatu iliyopita ambapo ilikuwa ni asilimia 10.4 kwa miaka ya 2012/2013 na 2013/2014 na asilimia 10.5 kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeshindwa kufikia lengo la Azimio la Abuja katika kipindi hiki cha miaka 10, ni vyema ikajitathmini ili kuona kwamba, kushindwa huko kuna athari zozote katika sekta ya afya nchini. Aidha, iendelee kutumia Azimio hilo kama lengo la kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya kwa kadri uwezo wa kiuchumi utakavyoendelea kuruhusu ili kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na watumishi katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* inayo dhamana ya kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kote nchini. Ili *MSD* iweze kutimiza wajibu huo kikamilifu, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Moja*,* Serikali ilipe deni la Shilingi bilioni 108 inalodaiwa na *MSD*, Serikali itoe fedha ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa mkupuo, taarifa za mapokezi ya dawa kutoka *MSD* katika hospitali au vituo vya afya nchini ziweke wazi na kamati za mapokezi ili kuleta uwazi na ushirikishwaji wa wananchi, MSD ihuishe takwimu za usambazaji wa huduma zake mara kwa mara kwa lengo la kujitathmini katika utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo na utegemezi wa wahisani: Bado kwa sehemu kubwa shughuli za maendeleo katika sekta hii zinategemea fedha za wahisani. Kwa mwaka 2014/2015 jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni 305.8, ambapo fedha kutoka vyanzo vya ndani ni Shilingi bilioni 54 tu na fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ni Shilingi bilioni 251.7 sawa na asilimia 82.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huo ndiyo unaojitokeza pia katika mwaka ujao wa fedha, ambapo asilimia 84.2 ya bajeti yote ya maendeleo inategemea fedha za nje. Ni wazi kwamba, utekelezaji wa miradi utaendelea kuathirika kwani fedha hizo za wahisani zimekuwa hazitolewi kwa wakati na hutolewa kwa kiwango kidogo. Pia, wakati mwingine miradi imekwama kabisa baada ya wahisani hao kujitoa katika ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu katika kuimarisha vyanzo vya mapato ya ndani ili viweze kutumika katika ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Moja, ili jengo jipya la *MOI* lianze kutumika, Serikali iwezeshe upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na vifaa tiba kiasi cha Shilingi bilioni 12,5. Aidha, Shilingi bilioni 1.8 zilizotengwa kwa ajili ya kuanza kulipia deni la ujenzi kutoka Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)* zitolewe ili kutoathiri mwenendo wa kifedha wa mfuko huo.

Pili, fedha za ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa tiba katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road*, kiasi cha shilingi bilioni 14 zitolewe kwa wakati.

Tatu, kwa upande wa Hospitali ya Mirembe, Serikali ihakikishe shilingi bilioni 124 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika kituo cha waathrika wa dawa za kulevya zinatolewa ili kuepusha matukio ya wagonjwa hao kutoroka na kufanyia fujo wagonjwa wa matatizo mengine pamoja na wafanyakazi.

Nne, Kamati inapongeza hatua ya kuanza kazi kwa Kitengo cha Tiba ya Magonjwa ya Moyo Muhimbili na inashauri Serikali kukiwezesha kwa rasilimali fedha na watu ili kifanye kazi kwa ufanisi na kusaidia Watanzania na pia kupunguza hitaji la huduma hiyo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli ya Serikali katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii: Kamati imebaini kwamba, zipo taasisi za Wizara ambazo zimeonyesha mafanikio katika eneo la ukusanyaji na udhibiti wa maduhuli kutokana na kuanza kutumia mfumo wa kielektoniki. Mfano ni Hospitali ya Rufaa Kanda Mbeya ambayo imeongeza mapato kutoka Shilingi milioni 50 hadi milioni 500 kwa mwezi. Aidha, Kamati inaipongeza sana Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Wizara kuhakikisha taasisi zake zinaingia katika matumizi ya mfumo huo wa kielektroniki ili kuongeza uwezo wa kukusanya na kudhibiti mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto: Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti katika eneo hili, ambapo katika mwaka uliopita Wizara iliongeza bajeti katika eneo hili kutoka Shilingi bilioni 14.5 hadi bilioni 19.5. Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya upasuaji katika Mkoa wa Tabora, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Kitete na Hospitali ya Igunga ya Nzega na Mkoa wa Mara Hospitali ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iendelee kuboresha eneo hili kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini kwa kuongeza utoaji wa chanjo, dawa za uzazi wa mpango, upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia na motisha kwa watumishi wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa bima ya afya kwa wote: Kamati inashauri yafuatayo:-

Kwanza, kukamilisha Mkakati wa Ugharamiaji wa Afya *(Health Care Financing Strategy)* utakaotoa mfumo mzuri wa ugharamiaji wa huduma ya afya. Pili, kutoa mwongozo wa kujiunga na mfumo wa bima ya afya utakawezesha kupata huduma bila kikwazo cha gharama *(Universal Coverage)*. Elimu ya kutosha itolewe kwa jamii ili iweze kuunga mkono mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii: Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:- Huduma za idara hiyo ziendelee kuboreshwa kwa kutengewa bajeti kubwa ili kuwezesha makundi yenye kuhitaji mahitaji maalum katika jamii kupata huduma stahiki. Pili, Wizara kupitia idara hii iendelee kuhamasisha jamii kuandaa miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kupata huduma na kutekeleza shughuli zao bila vikwazo. Tatu, Serikali iendelee kuboresha vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwa ni pamoja na vituo vya watoto yatima, walemavu, makazi ya wazee na mahabusu ya watoto ili kuwawezesha kuishi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa watu wenye ulemavu wa ngozi: Ni wazi ukatili na mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi (*albinism)* yamekuwa janga linaloisumbua nchi yetu na kuharibu jina zuri la Tanzania. Kamati inaungana na jamii nyingine kulaani na kukemea uendekezaji wa mila potofu za kutafuta mafanikio kwa kutumia viungo vya wenzetu hawa. Aidha, wenzetu hawa wanahitaji kuthaminiwa na kupata huduma stahiki kama makundi mengine katika jamii. Kwa mantiki hiyo Kamati inashauri yafuatayo:-

Kwanza, kesi za watuhumiwa wa mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi zipewe kipaumbele na vyombo vya sheria na hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaotiwa hatiani. Pili, Serikali kupitia Wizara ya Fedha iangalie uwezekano wa kutoa msamaha wa kodi kwa malighafi na vifungashio vya mafuta ya kulainishia ngozi kwa watu wenye *albinism* ili kuzuia mionzi ya jua (*sun skin cream)* ili bidhaa hiyo izalishwe kwa wingi hapa nchini na kwa gharama nafuu. Tatu, kuwe na mkakati maalum wa kutoa elimu kwa jamii dhidi ya imani potofu kwamba wanaweza kufanikiwa katika maisha kwa kutumia viungo vya watu wenye *albinism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madaktari ya Mwaka, 1959 *(The Medical and Dental Practitional Act)*: Kamati inaishauri Serikali kukamilisha Muswada huu wa Sheria na kuwasilisha Bungeni ili kupata sheria ambayo itawawezesha madaktari kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya tiba ya saratani nchini: Tatizo la saratani limeendelea kuongezeka nchini, ambapo wagonjwa wengi wamekuwa wakipokelewa na kupatiwa matibabu katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road.* Hata hivyo, matibabu hayo yamekuwa ya gharama kubwa kiasi cha kuwafanya watu wa kipato cha chini washindwe kumudu. Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Moja, Serikali iongeze ruzuku yake kwa taasisi hii ili kuiwezesha iendelee kutoa huduma kwa gharama nafuu kwa wagonjwa wa saratani;

Pili, Serikali ianzishe vituo katika hospitali za kanda kama vile, Bugando, *KCMC*, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na kadhalika ili ziweze kutoa huduma za awali kwa wananchi wa mikoani kabla hawajalazimika kuja *Ocean Road*.

Tatu, Serikali iangalie namna ya kutumia teknolojia ya wa *Tele - Medicine* kwa kushirikiana na hospitali za nchini India ambazo ziko tayari kwa ushirikiano huo. Utaratibu huo utasaidia wagonjwa wa saratani nchini kupata huduma ya madaktari bingwa kutoka nchini India bila kulazimika kwenda huko; na

Mwisho, Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha ili kuhakikisha ukarabati wa mashine za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali: Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Miswada hiyo inakamilika kabla ya kumalizika kwa muda wa uhai wa Bunge hili ili kuwezesha chombo hicho kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutunza kanzi data *(data base)* ya vinasaba vya binadamu *(DNA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika maeneo ya pembezoni: Ni wazi maeneo ya pembezoni katika nchi yetu yanakabiliwa na uhaba wa watumishi wakiwemo wa sekta ya afya, na ili kupunguza uhaba wa watumishi wa sekta ya afya katika maeneo hayo, Kamati inashauri yafuatayo:- Serikali iandae mkakati maalum wa kupata watumisi walio tayari kufanya kazi katika maeneo hayo.

Pili, Serikali iangalie uwezekano wa kusomesha vijana kutoka maeneo husika na kuingia nao mkataba wa utumishi mara wanapohitimu.

Tatu, Kuingia mkataba na wahitimu wa Sekta ya Afya wa kufanya kazi maeneo ya pembezoni kwa kipindi maalum kabla ya kuhama. Mkataba unaweza kuhusisha pia posho maalum kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la matibabu nchini India: Kamati ilipotembelea moja ya Hospitali za Apollo nchini India, iligundua kwamba, deni inalodaiwa Serikali yetu kutokana na gharama za matibabu ya Watanzania katika hospitali hizo limefikia takribani dola za Marekani milioni 9. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kulipa deni hilo ili kutokiuka mkataba wa makubaliano baina ya Serikali na Hospitali za Apollo wa kuhudumia wagonjwa wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati na pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati na hasa wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati nawapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dokta Seif Suleiman Rashid, Mbunge na Naibu Waziri Dokta Kebwe Steven Kebwe, Mbunge kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati katika kipindi chote hiki. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dokta Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii - Fungu 52, jumla ya Shilingi 813,976,870,000 kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2O15/2016 KAMA ILIVYOWASILSIHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, niaomba kuwasilishaTaarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni, katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilizuru kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za Wizara na taasisi zake ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na wahusika.

Pia Kamati ilikagua miradi ya maendeleo katika taasisi hizo ambayo iliidhinishiwa fedha katika mwaka huu wa fedha. Miongoni mwa taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, (NHIF), Taasisi ya Saratani Ocean Road (Ocean Road Cancer Institute), Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Kitengo cha Magonjwa ya Moyo Muhimbili, Kituo cha Mtangamao wa Waathirika wa dawa za Kulevya cha Itega, na Hospitali za Mikoa Morogoro na Dodoma.

Aidha, mwezi April mwaka huu, Kamati ya Huduma za Jamii, ilipata fursa ya kutembelea moja ya Hospitali za Kundi la Apollo iliyopo New Delhi, nchini India, kwa lengo la kuangalia huduma za tiba ambazo zinatolewa kwa Wagonjwa wa Tanzania wanaopelekwa katika

hospitali hizo. Kundi la Hospitali za Apollo lina makubaliano ya kimkataba na Serikali ya Tanzania, yanayowezesha Hospitali hizo kupokea Wagonjwa kutoka Tanzania ambao wanapata rufaa ya kupelekwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 01, 04 na 08 Mwezi Mei 2015, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Katika kipindi hicho Waziri wa Afya, Dkt. Seif Ali Rashid (Mb) aliwasilisha taarifa kuhusu Fungu 52 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,**uwasilishaji wa Mheshimiwa Waziri ulijikita katika maeneo manne Taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahususi yafuatayo:

i. Utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015,

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2014/15

iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015,

iv. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na maeneo ya vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ilibaini kwamba, kwa sehemu kubwa Wizara imezingatia ushauri uliotolewa jambo ambalo limewezeshwa kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:-

- Kupungua kwa utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kuongeza tengeo la fedha za ndani. Fedha ya maendeleo inayotokana na vyanzo vya ndani imeongezeka kutoka shilingi bilioni 19 katika mwaka wa fedha mwaka 2012/13 hadi kufikia shilingi bilioni 70 katika mwaka 2015/16. Kamati inapongeza hatua hii ya kuweza kuongeza bajeti ya ndani ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 350 ndani ya kipindi cha miaka minne ya bajeti (2012/13 hadi 2015/16) ni imani ya Kamati kwamba iwapo utaratibu huu utaendelea tutapunguza utegemezi wa fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa.
- Kuongezeka kwa ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya taasisi za Wizara kutokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki. Mfumo huu umewezesha baadhi ya taasisi kuvuka lengo la makusanyo. Kwa mfano Hospiali ya Rufaa, Mbeya imeongeza makusanyo kutoka shilingi milioni 50 kwa mwezi hadi shilingi milioni 500.

- Kuongezeka kwa tengeo la fedha za mradi wa huduma ya afya ya Mama na Mtoto kutoka shilingi bilioni 14.5 zilizoombwa hadi kufikia shilingi bilioni 19.5hii ni ishara kwamba Wizara inatambua umuhimu wa eneo hilo kupewa bajeti ya kutosha.

- Kukamilika kwa matengenezo ya mashine 2 za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya Oceand road.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo bado kuna maeneo yanayokabiliwa na changamoto na hivyo Kamati inashauri yafanyiwe kazi kama ifuatavyo:

i) Fedha za uendeshaji kutolewa pungufu, kucheleweshwa ama kutotolewa kabisa na hivyo kuathiri uendeshaji waHospitali, vyuo vya mafunzo na huduma za ustawi wa jamii.

ii) Ongezeko la idadi ya Wagonjwa wanaopelekwa nje kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa kwa ajili ya kugharamia matibabu hayo. Hali hii imesababisha deni la matibabu katika Hospitali za Apollo kufikia Dola za Marekani **milioni 9.2** hadi Mwezi wa Machi, 2015.

iii) Bajeti ndogo kwa ajili ya Wahitaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii wakiwemo Wazee, Watu wenye Ulemavu na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

iv) Kupungua kwa fedha za Wadau wa maendeleo katika sekta ya afya jambo ambalo limeathiri ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo.

v) Fedha ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani kuchelewa au kutolewa kwa kiasi kidogo jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi na kusababisha ongezeko la gharama za miradi hiyo, na baadhi ya Wakandarasi kuishitaki Serikali kwa kutowalipa madeni.

vi) Kuendelea kuongezea kwa deni la Serikali kwa Bohari ya Dawa (MSD) ambapo hadi Machi mwaka huu lilikuwa limefikia Sh. **Bilioni 108.6** Hali hii inaiathiri MSD katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

vii) Kuboresha huduma za Matibabu ya Saratani nchini na kuiwezesha Hospitali ya Ocean Road kufanya kazi kikamilifu,

iv) Upatikanaji wa Watumishi katika sekta ya afya hususan maeneo ya pembezoni,

v) Huduma za Bima ya Afya kwa wananchi wote,

vi) Utolewaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu nchini ikiwemo wenye ulemavu wa ngozi,

**3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitengewa jumla ya shilingi **659,743,825,000/=** ambapo kati ya fedha hizo shilingi**354,014,333,000/=**zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (recurrent expenditure) na shilingi **305, 729, 492,000**/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2015Wizara ilikuwa imepokea **shilingi 328,069,157,000/=**sawa na asilimia **58. 4**ya bajeti yote iliyotengwa.Katika kiasi hicho kilichotolewa shilingi **254,345,933,000/**ni kwa ajili ya matumizi ya kawadia, sawa na asilimia **90.9** ya fedha zilizotengwa. Kwa upande mwingine fedha zilizopokelewa katika maendelea ni shilingi **73,723,224,000** sawa na asilimia **26.1** ya bajeti yote iliyotengwa katika maendeleo.

Katika fedha ya maendeleo iliyopokelewa shilingi **8,800,000,000/=**ni kutoka fedha za ndani ikiwa ni asilimia **16.3** tu ya tengeo la ndani la **shilingi 54,000,000,000/=. Fedha za** nje zilizopokelewa ni**shilingi 73,723,224,000/=** sawa na asilimia **26.8**ya fedha za nje kwenye maendeleo ambazo zilikuwa **shilingi 251,729,492,000/=**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha iliyopokelewa na Wizara hadi Machi, 2015 ilikuwa asilimia 58.4 tu, Kamati inasikitishwa na mwenendo huo wa fedha. Aidha,inahoji ni kwa vipi Hazina itaweza kutoa asilimia 41.6 iliyosalia katika kipindi cha robo iliyosalia kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha wakati imetoa asilimia 58.4 tu ya bajeti ya Wizara katika robo tatu zilizopita.

Mheshimiwa Spika, katika ukusanyaji wa maduhuli hadi Machi, 2015 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi **70,367,588,681** sawa na asilimia 74 ya lengo lake ambalo lilikuwa shilingi **94,585,060,505.** Kiwango hicho cha ukusanyaji ni pungufu kwa asilimia 15 ikilinganishwa na Makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita ambayo yalifikia asilimia 89.

**3.0CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA AFYA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika,**wakati Kamati ikitathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya afya nchini zikiwamo zifuatazo:-

i. Kuendelea kukua kwa Deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ambapo hadi Machi, 2015 lilikuwa shilingi bilioni **108**,

ii. Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuendelea kuwa chini ya kiwango cha asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Azimio la Abuja la Mwaka 2001,

iii. Utendaji wa MSD kuhitaji uimarishwe,

iv. Wizara kuendelea kudaiwa na Wakandarasi ambao wanatoa huduma mbalimbali kwa Wizara na Taasisi zake.

v. Wizara kuendelea kutegemea sehemu kubwa ya fedha za maendeleoa (zaidi ya asilimia 82) kutoka vyanzo vya nje.

vi. Ongezeko la Wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa.

vii. Kuendelea kukua kwa deni la Serikali kwa Hospitali za Apollo nchini India ambazo zinapokea wagonjwa wa Tanzania,

viii. Fedha za maendeleo kutotolewa kwa wakati ambapo hadi Machi 2015 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 26.1 ya fedha zilizotengwa.

ix. Kusuasua kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM),

x. Upungufu wa Watumishi wa sekta ya afya nchini hasa katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa nchi,

xi. Upatikanaji duni wa huduma za Afya ya Mama na Mtoto ikiwemo utoaji wa huduma za uzazi salama na mpango mkakati wa kuzuia vifo vya mama na mtoto.

xii. Kutoeleweka hasa ni kiasi gani kinatengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo,

xiii. Gharama kubwa za matibabu kwa Wagonjwa waSaratani na Figo,

xiv. Bajeti finyu kwa Idara ya Ustawi wa Jamii;

**4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekusudia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 122,218,398,500 ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 23 ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha 2014/15.

Aidha, ili kutekeleza majukumu yake kikamilifuWizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **813,976,870,000/=**ambapo kati ya fedha hizo shilingi **444,618,452,000/=**ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo na shilingi **369,358,418,000**/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujadili Taarifa ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2015/16 Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Wizara imeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 191 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2014/15.Kamati inapongeza hatua hii, hata hivyo bado inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya hadi kufikia lengo la asilimia 15 la bajeti ya taifa kwa mujibu wa Azimio la Abuja, la mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Pia Kamati ilibaini kwamba, Wizara imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha Idara ya Huduma za Uuguzi na Ukunga (Kifungu 2004) ambayo imetengewa shilingi bilioni 422.3 na Kitengo cha "Huduma za Dawa "Pharmaceutical Services Unit" (Kifungu 2005) ambacho kimetengewa shilingi bilioni 36.6,ili kusimamia na kuboresha huduma za upatikanaji wa dawa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ni matumaini ya Kamati kwamba, kuanzishwa kwa maeneo haya mapya ya kibajeti yataleta ufanisi zaidi na kuimarisha huduma katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inasikitishwa na hatua ya baadhi ya vifungu kupunguziwa fedha katika mwaka ujao wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Vifungu hivyo ni pamoja na 2001 (Huduma za Kinga) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 275.6 mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 246.3 mwaka ujao wa fedha.

Vingine ni Kifungu 3001 (Idara ya Kinga) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 34.3 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 33 kwa mwaka wa fedha ujao na, kifungu 3002 (Idara ya Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 732.1 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 661.6 kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba, ni vyema Wizara ikahakikisha hatua hiyo haileti madhara kwa maeneo yaliyoguswa na hatimaye kuathiri utoaji wa huduma za afya nchini.

**5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kujadili makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2014/2015, Kamati inatoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

**5.1 Bajeti ya Sekta ya Afya na Azimio la Abuja**

Mheshimiwa Spika,itakumbukwa kwamba, nchi yetu ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo ni Wanachama Wa Umoja wa Afrika, ambazo zimeridhia Azimio la Abuja linalozitaka nchi wanachama kuongeza bajeti katika Sekta ya Afya hadi kufikia asilimia 15 ya bajeti ya Serikali ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, huu ukiwa ni mwaka wa mwisho wa kufikia lengo hilo ni wazi kwamba, hakuna dalili za nchi yetu kufikia kiwango cha asilimia 15 cha bajeti ya Serikali kuelekezwa katika Sekta ya afya. Ushahidi unajionesha kupitia mwenendo wa ongezeko la bajeti ya sekta ya afya katika miaka mitatu iliyopita ambapo ilikuwa asilimia 10.4 kwa miaka ya 2012/13 na 2013/14 na asilimia 10.5 kwa mwaka 2014/15.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali imeshindwa kufikia lengo la Azimio la Abuja katika kipindi hiki cha miaka 10, ni vyema ikajitathmini ili kuona iwapo kushindwa huko kuna athari zozote katika Sekta ya Afya nchini. Aidha, iendelee kutumia Azimio hilo kama lengo la kuendelea kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya kwa kadri uwezo wa kiuchumi utakavyoendelea kuruhusu ili kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na watumishi katika sekta hiyo.

**5.2 Upatikanaji wa Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi nchini.**

Mheshimiwa Spika, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ndiyo ina dhamana ya kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kote nchini. Ili MSD iweze kutimiza wajibu huo kikamilifu Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

- Serikali ilipe deni inalodaiwa na MSD (shilingi bilioni 108);
- Serikali itoe fedha ya Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa mkupuo;
- Taarifa za mapokezi ya dawa kutoka MSD katika Hospitali au vituo vya afya nchini ziweke wazi na Kamati za mapokezi ili kuleta uwazi na ushirikishwaji wa Wananchi;
- MSD ihuishe takwimu za usambazi wa huduma zake mara kwa mara kwa lengo la kujitathmini katika utendaji wake.

**5.3Bajeti ya Maendeleo na Utegemezi wa Wahisani**

**Mheshimiwa Spika**, bado kwa sehemu kubwa shughuli za maendeleo katika sekta hii zinategemea fedha za Wahisani. Kwa Mwaka 2014/2015, jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni sh. **305,729,492,000/=** ambapo fedha kutoka vyanzo vya ndani ni shilingi **54,000,000,000/=** na fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ni shilingi **251,729,492,000/** sawa na asilimia **82.3**

Mwenendo huo ndiyo unaojitokeza pia katika mwaka ujao wa fedha, ambapo asilimia 84.2 ya bajeti yote ya maendeleo inategemea fedha za nje. Ni wazi kwamba, utekelezaji wa miradi utaendelea kuathirika kwani fedha hizo za Wahisani zimekuwa hazitolewi kwa wakati na

kutolewa kwa kiwango kidogo. Pia wakati mwingine miradi imekwama kabisa baada ya Wahisani hao kujitoa katika ufadhili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu katika kuimarisha vyanzo vya mapato vya ndani ili viweze kutumika katika ya miradi ya maendeleo.

**5.4Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 201/2015**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kutembelea miradi ya maendeleo ukiwemo ujenzi wa jengo la tiba na wodi ya Wagonjwa katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali ya Magonjwa wa Akili Mirembe, na Kitengo cha Tiba ya Moyo Muhimbili, inashauri mambo yafuatayo:

i) Ili jengo jipya la MOI lianze kutumika, Serikali iwezeshe upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na vifaa tiba kiasi cha shilingi bilioni 12.5. Aidha, shilingi bilioni 1.8 zilizotengwa kwa ajili ya kuanza kulipia deni la ujenzi kutoka Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) zitolewe ili kutoathiri mwenendo wa kifedha wa mfuko huo.

ii) Fedha za ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa tiba katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, kiasi cha shilingi bilioni 14 zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miundombinu husika inakuwa katika hali nzuri kwa lengo la kutoathiri utoaji huduma kwa Wagonjwa wa Saratani.

iii) Kwa upande wa Hospitali ya Mirembe, Serikali ihakikishe shilingi bilioni 124 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika kituo cha Waathrika wa dawa za kulevya zinatolewa ili kuepusha matukio ya wagonjwa hao kutoroka na kufanyia fujo wagonjwa wa matatizo mengine pamoja na wafanyakazi.

iv) Kamati inapongeza hatua ya kuanza kazi kwa kitengo cha tiba ya magonjwa ya Moyo Muhimbili, na inashauri Serikali kukiwezesha kwa raslimali fedha na watu ili kifanye kazi kwa ufanisi na kusaidia Watanzania na pia kupunguza hitaji la huduma hiyo nje ya nchi.

**5.5Maduhuli ya Serikali katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, zipo taasisi za Wizara ambazo zimeonesha mafanikio katika eneo la ukusanyaji na udhibiti wa maduhuli kutokana na kuanza kutumia mfumo wa kielektoniki. Mfano ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ambayo imeongeza mapato kutoka shilingi milioni 50 hadi 500 kwa mwezi. Aidha, Kamati inaipongeza sana Hospitali hiyo.

Kamati inashauri Wizara kuhakikisha taasisi zake zinaingia katika matumizi ya mfumo huu wa kielektroniki ili kuongeza uwezo wa kukusanya na kudhibiti mapato.

**5.6Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto**

**Mheshimiwa Spika**, uhakika wa huduma bora ya afya kwa Mama na Mtoto ndiyo msingi wa ustawi wa jamii na ndiyo kipimo cha utoaji wa huduma ya afya katika jamii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti katika eneo hili ambapo katika mwaka uliopita Wizara iliongeza bajeti katika eneo hili kutoka shilingi bilioni 14.5 hadi bilioni 19.5.

Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya upasuaji katika mkoa wa Tabora (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Kitete, na Hospitali za Igunga na Nzega) na mkoa wa Mara (Hospitali ya Serengeti).

Kamati inashauri Serikali iendelee kuboresha eneo hili kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini kwa kuongeza utoaji wa chanjo, dawa za uzazi wa mpango, upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia na motisha kwa watumishi wa sekta ya afya.

**5.7 Mpango wa Bima ya Afya kwa wote**

**Mheshimiwa Spika**, afya nzuri na ya uhakika ni jambo la kwanza la msingi kwa binadamu yoyote. Hilo pia ndiyo hitaji kwa Watanzania na ndiyo maana Kamati imekuwa ikisisitiza juu ya utaratibu wa bima ambao utahusisha makundi yote katika jamii. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa azma ya kuwezesha mpango huu Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kukamilisha Mkakati wa Ugharamiaji wa Afya (Health Care Financing Strategy) utakaotoa mfumo mzuri wa ugharamiaji wa huduma ya afya;
- Kutoa Mwongozo wa kujiunga na mfumo wa Bima ya Afya utakawezesha kupata huduma bila kikwazo cha gharama (Universal Coverage).
- Elimu ya kutosha itolewe kwa jamii ili iweze kuunga mkono mpango huu

**5.8 Idara ya Ustawi wa Jamii**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ustawi wa Jamii ni suala mtambuka linalogusa makundi tofauti katika jamii, Kamati imekuwa ikishauri Idara hii kuweka chini ya mamlaka inayoshughulikia masuala mtambuka, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli za Wizara zote. Hata hivyo, kumekuwa na hali ya kusuasua katika kutekeleza ushauri huo. Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:

- Huduma za Idara hiyo ziendelee kuboreshwa kwa kutengewa bajeti kubwa ili kuwezesha makundi ye mahitaji maalum katika jamii kupata huduma stahiki.

- Wizara kupitia Idara hii iendelee kuhamasisha jamii kuandaa miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kupata huduma na kutekeleza shughuli zao bila vikwazo.
- Serikali iendelee kuboresha vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwa ni pamoja na vituo vya watoto yatima, walemavu, makazi ya wazee na mahabusu ya watoto ili kuwawezesha kuishi katika mazingira mazuri.

**5.9 Huduma kwa Watu wenye Ulemavu wa Ngozi**

Mheshimiwa Spika, ni wazi ukatili na mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi "Alibnism" yamekuwa janga linaloisumbua nchi yetu na kuharibu jina zuri la Tanzania. Kamati inaungana na jamii nyingine kulaani na kukemea uendekezaji wa mila potofu za kutafuta mafanikio kwa kutumia viungo vya wenzetu hawa. Aidha wenzetu hawa wanahitaji kuthaminiwa na kupata huduma stahiki kama makundi mengine katika jamii. Kwa mantiki hiyo Kamati inashauri yafuatayo:

- Kesi za Watuhumiwa wa mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, zipewe kipaumbele na vyombo vya sheria na hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaotiwa hatiani.

- Serikali kupitia Wizara ya Fedha iangalie uwezekano wa kutoa msamaha wa kodi kwa malighafi na vifungashio vya mafuta ya kulainishia ngozikwa watu wenye albinism ili kuzuia mionzi ya jua (Sun Skin Cream)ili bidhaa hiyo izalishwe kwa wingi hapa nchini na kwa gharama nafuu.

- Kuwe na mkakati maalum wa kutoa elimu kwa jamii dhidi ya imani potofu kwamba wanaweza kufanikiwa katika maisha kwa kutumia viungo vya watu wenye albinism.

**5.10 Sheria ya Madaktari ya Mwaka 1959 *(The Medical and Dental Practitional Act, 1959)***

**Mheshimiwa Spika,** katika Bunge la bajeti lililopita Kamati ilishauri Serikali kuwasilishwa Muswada waSheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno kwani iliyopo ni ya muda mrefu sana (1959).

Muswada huo ni muhimu kwani tasnia ya udaktari nchini imekuwa ikipitia mabadiliko mbalimbali ambayo yanahitajika kujumuishwa katika taaluma ya Tiba. Kamati inaishauri Serikali kukamlisha Muswada huo wa Sheria na kuuwasilisha Bungeni ili kupata Sheria ambayo itawezesha Madaktari kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kwa weledi.

**5.11Huduma ya Tiba ya Saratani nchini**

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Saratani limeendelea kuongezeka nchini ambapo Wagonjwa wengi wamekuwa wakipokelewa na kupatiwa matibabu katika Taasisi ya Saratani Ocean Road. Hata hivyo matibabu hayo yamekuwa ya gharama kubwa kiasi cha kuwafanya watu wa kipato cha chini washindwe kumudu. Kamati inashauri mambo yafuatayo:

- Serikali iongeze ruzuku yake kwa taasisi hii ili kuiwezesha iendelee kutoa huduma kwa gharama nafuu kwa Wagonjwa wa Saratani,

- Serikali ianzishe vituo katika Hospitali za Kanda kama vile, Bugando, KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, na kadhalika ili viweze kutoa huduma za awali kwa Wananchi wa mikoani kabla hawajalazimika kuja Ocean Road,

- Serikali iangalie namna ya kutumia teknolojia ya wa Tele - Medicine kwa kushirikiana na Hospitali za nchini India ambazo ziko tayari kwa ushirikiano huo. Utaratibu huo utasaidia Wagonjwa wa Saratani nchini kupata huduma ya Madaktari Bingwa kutoka nchini India bila kulazimika kwenda huko,

- Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha ili kuhakikisha ukarabati wa Mashine za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*muda wote.

**5.12 Uanzishwaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, ili Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu (GCLA) uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu unahitaji kuwa na sheria ya uanzishwaji wa Maabara yake. Mchakato wa Muswada huo ulienda sambamba na ule wa Wataaluma wa Kemia, lakini umeshindwa kukamilishwa katika Mikutano Miwili ya Bunge iliyopita. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Miswada hiyo inakamilika kabla ya kumalizika kwa Muda wa Uhai wa Bunge hili ili kuwezesha chombo hicho kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutunza Kanzi data (data base) ya Vinasaba vya Binadamu (DNA).

**5.13 Upungufu wa Watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo ya pembezoni**

Mheshimiwa Spika, ni wazi maeneo ya pembezoni katika nchi yetu yanakabiliwa na uhaba wa Watumishi wakiwemo wa Sekta ya Afya, ili kupunguza uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo hayo Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iandae mkakati maalum wa kupata Watumisi walio tayari kufanya kazi katika maeneo hayo;

- Serikali iangalie uwezekano wa kusomesha vijana kutoka maeneo husika na kuingia nao mkataba wa utumishi mara wanapohitimu;

- Kuingia mkataba na wahitimu wa Sekta ya Afya wa kufanya kazi maeneo ya pembezoni kwa kipindi maalum kabla ya kuhama. Mkataba unaweza kuhusisha pia posho maalum kwa watumishi hao.

**5.14 Deni la Matibabu nchini India**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea moja ya Hospitali za Apollo nchini India, iligundua kwamba, deni inalodaiwa Serikali yetu kutokana na gharama za matibabu ya Watanzania katika hospitali hizo limefikia takribani dola za Marekani milioni 9. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kulipa deni hilo ili kutokiuka mkataba wa makubaliano baina ya Serikali na Hospitali za Apollo wa kuwadumia Wagonjwa wa Tanzania.

**6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati.Nikushukuru pia namna ambavyo umekuwa tayari kutoa ushauri na maelekezo kwa Kamati pale tulipokuhitaji.

**Mheshimiwa Spika**, pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za jamii kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, na hasa wakati wa kuandaa taarifa hii. Niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Stephen Hillary Ngonyani, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera, Mb | - " |
| 5. Mhe. Faki Haji Makame, Mb | - " |
| 6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda, Mb | - " |
| 7. Mhe. Riziki Omar Juma, Mb | - " |
| 8. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje, Mb | - " |
| 9. Mhe. Antony Gervas Mbassa, Mb | - " |
| 10. Mhe. Ali Juma Haji, Mb | - " |
| 11. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb | - " |
| 12. Mhe. Gregory George Teu, Mb | - " |
| 13. Mhe. Abia Muhama Nyabakari, Mb | - " |
| 14. Mhe. Salome Daudi Mwambu, Mb | - " |
| 15. Mhe. Zabein Muhaji Mhita, Mb | - " |
| 16. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb | - " |

17. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - "
18. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mb - "
19. Mhe. Asnain Muhamed Murji, Mb - "
20. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - "
21. Mhe. Abdulaziz Muhamed Abood, Mb - "

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ninawapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dkt. Seif Suleiman Rashid (Mb), na Naibu Waziri Dk. Kebwe Steven Kebwe (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati katika kipindi chote hiki. Aidha, ninampongeza Katibu Mkuu Dkt. Donald Mbandona Wataalam wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Pia niwanawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Happyness Ndalu, wakisaidiwa na Ndugu Jane Ndulesi,kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, **Fungu 52,** jumla ya **shilingi 813,976,870,000/=** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII**
02 Juni, 2014

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Umbulla. Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya ya Afya Na Ustawi Wa Jamii. Mheshimiwa Dokta Antony Gervase Mbassa. Nusu saa! *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.**
**KAMA YALIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuniamini na ushirikiano mkubwa anaonipa katika kuisimamia Serikali katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru sana na kuwapongeza sana wenyeviti wenza wa UKAWA, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe – Mwenyekiti CHADEMA, Mheshimiwa James Francis Mbatia - Mwenyekiti wa *NCCR*-MAGEUZI Taifa, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Haruna Lipumba – Mwenyekiti wa *CUF* na Mheshimiwa Dokta Emmanuel Makaidi – Mwenyekiti wa *NLD* kwa kazi kubwa wanayoifanya kuunganisha nguvu ya pamoja. Hakika UKAWA ndio mpango mzima na tumaini la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati napenda sana kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa ushirikiano wao mkubwa na wa dhati wanaonipa katika majukumu yangu ya kibunge. Hakika nimefanya kazi hii kwa moyo mkunjufu na naahidi kuendelea kufanya kazi hiyo, kamwe sitowaangusha, bali nazidi kuwaahidi uwakilishi uliotukuka. Hakika kazi tuliyoianza wote mwaka 2010 mnaiona ilivyoleta mabadiliko na maendeleo ya kweli katika jimbo letu. Uzi ni uleule na kamba ni ileile katika kuhakikisha tunaivusha Biharamulo yetu. Pamoja tutasonga mbele! Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu mkubwa na kwa jinsi wanavyonipa moyo hususan katika majukumu haya muhimu ya kuwatumikia wananchi. Mke wangu Benedicter Justinian, watoto wangu Thecla Mbassa, Bernard Mbassa na Beatha Mbassa. Nasema ahsanteni sana na muzidi kunivumilia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee, niwashukuru watia nia ya urais waliojinadi wiki iliyopita kwa kukubaliana na kile ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisemea kuwa Serikali ya CCM imejaa rushwa, kutokuwajibika, kufanya kazi kwa mazoea, upendeleo katika kugawana keki ya Taifa, isiyoweza kuchukua uamuzi na uchafu mwingine mwingi. Watia nia hao wa urais walikuwa, na bado ni sehemu ya Serikali hiyo hiyo ya awamu ya nne iliyopo madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kuna kila sababu kwa Watanzania kuwapuuza watu kwa kuwa ni watu hao hao, wa chama kile kile, maneno ni yale yale, hawana uwezo wa kutuondoa kwenye tope walilotuingiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeendelea kutekelezwa kwa kiwango kidogo mno kiasi cha kutokidhi mahitaji ya huduma kwa Watanzania wote. Wizara hii imekuwa kila mara inatengewa fedha ambazo kimsingi haziletwi toka Hazina na kusababisha maisha ya Watanzania wengi kuwa rehani hususan wale waishio vijijini na wale wenye hali duni kifedha. Ni wazi na kweli kwamba ni Watanzania wachache sana wenye uwezo wa kusafiri na kutibiwa nje ya nchi yao. Hali hii sio ya kuinyamanzia hata kidogo kwani ni jukumu la Serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora ya afya na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kuwa bajeti inayotekelezwa ni finyu, bado fedha hazitolewi kwa awamu zinazotakiwa kulingana na mpango wa Wizara, bali fedha nyingi zinatolewa katika awamu ya mwisho *(robo ya mwisho)*. Jambo hili linapelekea kwa kiwango kikubwa fedha hizo kutumika nje ya utaratibu na maksudio na hivyo kukosa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ni kuwa, fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikuwa Shilingi 305,729,492,000. Hadi Machi, 2015, zilizopokelewa ni Shilingi 73,723,224,000. Kati ya fedha hizo za ndani ni Shilingi 8,800,000,000. Fedha zilizopokelewa ni sawa na asilimia 26.1 ya mahitaji hadi mwezi Machi, lakini mahitaji halisi ya Wizara hadi kufikia mwezi Machi yalikuwa ni Shilingi 282,577,522,000. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua kiasi kilichosalia kitatolewa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwenendo huo wa utoaji wa fedha za afya ni kweli Serikali hii ya CCM ina dhamira njema na afya ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Abuja: Tangu Azimio la Abuja lisainiwe mnamo Aprili, 2001 huko Abuja, Nigeria, mpaka sasa azimio hilo limekuwa ni kitendawili kisichoteguliwa. Kwa kipindi chote cha miaka 15, Serikali imeshindwa kutimiza agizo hilo la kutenga asilimia 15 ya bajeti yake ya pesa za ndani kuhudumia wananchi wake. Kwa muda wote Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo sana. Mpaka leo hii tumeshindwa kufikia lengo tulilolisaini wenyewe kwa utashi wetu wenyewe bila kushurutishwa na mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taifa lolote kama haliwezi kuwa na mipango thabiti ya kuimarisha afya ya watu wake, hakika taifa hilo haliwezi kuwa na maendeleo wala mafanikio katika ustawi wa wananchi wake. Ni lazima kama taifa kuwa na juhudi za makusudi na za wazi za kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya nchi ili kuweza kuhudumia watu wake wapate afya bora na ustawi mzuri wa maisha. Tanzania kama nchi yenye rasilimali za kutosha tumeshindwa kuiga mfano wa nchi ndogo, tena maskini kama Rwanda, Botswana, Malawi, Niger, Zambia na Burkina Faso ambao wamefanikiwa walau kufikia tengeo la asilimia 15 kama walivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua, kama tumeshindwa kutimiza azimio hilo la kutenga asilimia 15 ya mapato ya ndani na sasa tunaanza kutekeleza *BRN*, je, tutafanikiwa? Au ni kuwa na mipango mingi ili hali hatuwezi kutekeleza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi imeendelea kuwa ya kutotosheleza katika vituo vya kutolea huduma. Hali hii inatokana na kutokuwepo upatikanaji mzuri wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Bohari yetu ya Dawa *(MSD)*. Aidha, hali hii inapelekea wananchi kukosa huduma ya afya katika vituo vingi vya kutolea huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukosekanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi limekuwa sugu kwa kipindi kirefu sana, na hii imetokana na kutokuwa na dhamira ya dhati ya kupokea ushauri unaotolewa na Kamati au kutokufikiria mbinu mbadala ya kuboresha huduma hii muhimu sana. Mara zote Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kufikiria suala la kuwa na mbia wa *MSD* ili kuleta hali ya ushindani katika kutoa huduma. Ushauri huu haukuwahi kufuatwa wala kutekelezwa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utafiti inaonyesha kuwa asilimia 76% ya maombi ya dawa kutoka kwenye Ofisi za Dawa za Kanda kwenda kwenye vituo vya afya zinawasilishwa zikiwa zimechelewa na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwenye vituo vya afya na asilimia 24% tu ya maombi ndiyo inayofika kwa wakati.

Aidha, kwa wastani asilimia 54% ya maombi ya Ofisi za Dawa za Kanda nayo yanacheleweshwa na kulinganisha na muda uliowekwa wa siku 14, lakini 20% ya maombi yanachukua kati ya siku 15 na 21 na asilimia 34% ya maombi yanachukua zaidi ya siku 21 hadi kupokelewa kwenye Ofisi za Kanda za Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa la kiutendaji ambalo kwa sasa ni wazi kabisa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kulipatia ufumbuzi. Ni vyema Watanzania wakaachana na Serikali hii ya CCM ambayo imechoka na hivyo kushindwa kusimamia afya za Watanzania na kuipa ridhaa Serikali mpya itakayokuwa chini ya vyama vinavyoundwa na UKAWA ili iweze kuhakikisha afya za Watanzania zinapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati suala hili la bima ya afya ya jamii linaanza katika Wilaya ya Igunga, kila halmashauri ilitenga muda na fedha kupeleka timu ya wataalamu kwenda kujifunza na kuona uhalisia wa suala lenyewe linavyotekelezwa. Leo hii bahati mbaya hatujapata mrejesho wa ufanisi wa suala hilo kwa sasa, kama wanazidi kufanya vizuri, ni mbinu zipi za ziada wameongeza, ni mikakati ipi ya ziada iliyopo kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni jambo la hekima hata kama mfuko huu umepatwa na msukosuko, ni vema kuwa na maelezo ya kina ya sababu za msingi, kwa nini mfuko huu umeshindwa kuendelea kutimiza adhima yake ya kuwahudumia wananchi kama ilivyokuwa hapo awali, na ni nini sababu za msingi za kuporomoka kwa misingi imara iliyokuwa imewekwa na waasisi wa mfuko huu, imekiukwa na waliofanya hivyo wamechukuliwa hatua gani za kiutendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoelekea kuwa na mfuko wa pamoja wa huduma ya afya kwa mwanchi, ni vyema masuala haya yakapata ufafanuzi wa kina ili kila mwananchi aondokane na uoga au mashaka juu ya uhakika wa huduma iliyokusudiwa na vilevile uhakika wa mchango wake atakaoutoa utalindwa vipi na kufanikisha lengo lililokusudiwa. Sehemu nyingi wananchi hawapati taarifa sahihi za matumizi ya michango ya fedha zao zinafanya nini na hivyo kusababisha mwitikio hasi wa wananchi kuchangia miradi mbalimbali ikiwemo hata bima ya afya ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali kupitia Wizara hii kuwaeleza wananchi ni nini hatima ya afya zao hapo baadae maana wamekosa imani hususan wazee, wastaafu, akina mama na wajane ambao hao wote wanabeba mzigo mkubwa wa kulea watoto yatima na wajukuu walioachwa na wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Shirika la Afya la Dunia *(WHO)* ya mwaka 2014 inasema kuwa, tatizo kubwa sana hapa nchini la upatikanaji wa dawa muhimu hasa kwenye vituo vya afya vya Serikali, inaendelea kueleza kuwa mara zote dawa muhimu kwenye vituo hivyo hazipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, takwimu za *WHO* kuhusiana na upatikanaji wa dawa muhimu kati ya vituo vya afya vinavyomilikiwa na Serikali na vile vya binafsi zinaonyesha kuwa vituo vya Serikali ni 24% wakati kwa vituo vya binafsi ni takriban mara mbili yake, yaani 47.9%

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazitolea tafsiri takwimu hizo za *WHO* kuwa, dawa zinazosambazwa na *MSD* zinafika kwenye vituo binafsi kabla ya kufika kwenye vituo vya Serikali. Hivyo basi ni jukumu la watendaji kuangalia chanzo cha tatizo hilo ni nini hasa, au kuna uwezekano mkubwa watumishi katika vituo vya afya vya umma ndio wamiliki wa vituo binafsi, na hapo ndipo mgongano wa maslahi unapoingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa utendaji kazi wa *MSD* unazidi kushuka kadri siku zinavyokwenda, hii inatokana na ukweli kwamba fedha za uendeshaji wa taasisi hiyo *(working capital)* imeendelea kushuka kwa zaidi ya asilimia 69% katika kipindi cha miaka mitano kutoka Shilingi bilioni 81 mwaka 2008 hadi Shilingi bilioni 25 mwaka 2015, jambo hili limepunguza uwezo wa *MSD* kuagiza dawa zinazokidhi mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kushuka kwa mtaji wa uendeshaji linaweza kuwa limetokana na menejimenti ya *MSD* kushindwa kufanya kazi yake kama inavyotakiwa. Aidha, inaweza kuwa imetokana na uwezo mdogo wa uongozi huo kuweza kuongoza taasisi hiyo, kwani Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini taasisi hiyo inatakiwa ijiendeshe kibiashara. Kama ndio hivyo inakuwaje wanashindwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni

zinavyohitaji? Pia ni muda muafaka sasa kuwa na watendaji wakuu wa *MSD* wenye uwezo wa uendeshaji na siyo tu kwa kuwa ni wafamasia tu, bali wawe na utaaalam wa uendeshaji wa biashara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la deni la Bohari Kuu ya Dawa limekuwa halina majibu sahihi na tafsiri ya kweli. Kila mwaka deni limekuwa aidha likiongezeka na hali na kasi ya ulipaji wa deni hilo ikiwa ndogo sana. Inasikitisha kuona kwamba wananchi wanakosa dawa na vifaa tiba ili hali Serikali inashindwa kulipia sehemu ya deni lake. Kila mara majibu ya Serikali yanasema kuna sehemu ya deni halijahakikiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata jibu ni lini hesabu hii kamili itahakikiwa na kupata jibu? Isije kuwa kila siku deni linaongezeka ili hali ni kichaka cha kuficha maovu na hivyo kuonekana kinacholipwa ni deni hewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya deni hili inasemekana ni kugomboa dawa na vifaa tiba tunavyopewa kama misaada toka kwa wahisani mbalimbali hapo bandarini! Jambo la kushangaza, ni dawa zipi ambazo hata zikiletwa hazifiki kwa wahitaji huko vijijini? Lakini wakati huo kuna ongezeko kubwa sana la dawa ambazo zimeisha muda wake hapo ghalani. Sasa suala la kujiuliza ni kwamba, kwa nini tupoteze fedha nyingi kugomboa dawa ambazo muda wake wa kutumika umefika ukingoni au kuisha kabisa. Tunapopokea misaada hiyo huwa tunajiuliza maswali hayo au inabaki kuwa huku kwetu ndiyo maeneo muafaka ya kutupia au kuteketezea dawa zao ambazo zimeisha muda waake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahala sasa hata kama tunategemea misaada, tujisimamie na tuseme hapana imetosha. Suala hili linatugharimu mara mbili zaidi, kwani tunagharimika kugomboa dawa hizo bandarini, lakini tunagharimia pia kuziteketeza dawa hizo kwa gharama kubwa. Haiwezekani kuendelea kupokea misada isiyokuwa na tija kwa taifa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata jibu la uhakika ni lini hasa hesabu hizi zitahakikiwa kupata jibu kamili ili Serikali ilipe deni hilo na wananchi waache kutaabika kwa kukosa dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la matibabu ya nje ya nchi: Suala la deni la matibabu nje ya nchi linazidi kuongezeka kila uchao, na hakika sio heshima kwa nchi yetu hata kidogo. Tanzania tunaongoza kwa kuwapeleka wagonjwa wetu hospitali za nchini India na pia tunaongoza kwa kutolipa deni la hospitali hizo za nchini India, hii ni hatari kubwa sana. Inasikitisha kuona ni tabaka la watu wachache tu wanaoweza kwenda kuhudumiwa huko ili hali haki ya kupata huduma bora ni ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi tunayo rasilimali watu hapa kwetu nchini yaani madaktari, wauguzi hodari na fani nyinginezo. Wataalam hawa wameshirikishwaje katika kutoa ushauri wao ili kusudi Serikali iweze kuja na mpango mahsusi wa kutengeneza mazingira ya wao kutumia taaluma yao kuwahudumia wananchi hapa nchini? Tunao madaktari bingwa, lakini kila mara hawana vitendea kazi katika idara zao, na hii ni sawa na kumpeleka mvuvi hodari kina kirefu cha bahari wakati hana vifaa vya kuvulia hao samaki, atafanya nini? Ni wakati sasa wa Serikali kuwatumia wataalam hao na kusikiliza ushauri wao ili uweze kufanyiwa kazi na wapatiwe vifaa vya kutosha watumie taaluma yao kusaidia wananchi wanyonge hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali kufikiria kununua vifaa tiba na vitendanishi ili kuboresha huduma za wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kubwa ambazo

zingeweza kufanyika hapa nchini, lakini inabidi wakatibiwe nje ya nchi hali inayoongeza uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha, gharama za malazi, usafiri na hata nafasi ya familia kutoa huduma kwa wapendwa wao wanaohitaji uuangalizi maalum wa wanafamilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi gharama za kuwapeleka wagonjwa hawa huko nje ya nchi kwa matibabu kama zikitumiwa vizuri kununua vifaa tiba na vitendanishi, hakika litakuwa ni suruhisho kwa mahitaji ya wagonjwa wengine watakaohitaji huduma hiyo na hii itarahisisha hata kupata wataalam wengine kutoka nje ya nchi. Tumekuwa na tatizo kubwa la wataalam wetu kwenda kufanya kazi nje ya nchi, lakini mojawapo ya sababu ni kukosekana kwa hivi vifaa tiba na vitendanishi, jambo ambalo linawafanya wasiweze kutumia taaluma yao vizuri na kupoteza muda wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali kulipa deni la hospitali za India haraka iwezekanavyo ili kupisha hali ilivyo sasa, kwani mpaka sasa tunadaiwa zaidi ya bilioni 17 na kila uchao wagonjwa hawa wanazidi kupelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali sasa kufikiria kununua vifaa tiba na vitendanishi ili kazi hiyo iweze kufanyika hapa hapa nchini. Serikali itengeneze mazingira bora ya kuwa na mikataba na madaktari toka nje ya nchi waweze kutoa huduma hapa nchini na hii itaongeza morali ya kazi na pia kutengeneza mazingira ya urafiki katika kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu katika sekta ya afya. Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa 2007 hadi 2017 na mpango mkakati wa rasilimali watu sekta ya afya wa mwaka 2008 hadi 2015 iliweka mikakati ya kuongeza watumishi katika sekta hiyo, ni wazi na kweli ulikuwa mkakati dhati na wenye malengo mazuri, lakini jambo moja mpaka sasa hakuna taarifa za wazi zinazoonyesha moja kwa moja jinsi gani mpango huu umefanikiwa kuhuisha na kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa na vigezo muhimu katika sekta hii ya afya. Leo tuna muda mfupi sana MMAM kukamilisha muda wake na wakati bado hali halisi ya watumishi katika sekta ya Afya bado hairidhishi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua, mpaka sasa MMAM imefaniwa kwa kiasi gani katika kufanisha mpango huo? Kwani mpaka sasa mipango imekuwa mingi na bado sasa tunazidi kuongeza! Je tutafanikiwa kukamilisha miradi na mipango tuliyonayo katika muda uliopangwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana ya watumishi wa sekta ya afya hapa nchini. Hii inatokana na kutopandishwa vyeo kwa muda muafaka, kutolipwa stahili zao kwa muda na mbaya zaidi mtumishi anapojiendeleza katika kada yake hucheleweshewa kubadilishiwa mshahara wake na stahili zake mbalimbali. Hali hii inawafanya baadhi ya watumishi wakate tamaa ya kujiendeleza na wengine kufikiria sasa ni bora kuhamia fani nyingine kwani maslahi yao hayatekelezwi pamoja na kutimiza wajibu wao. Suluhisho la hili ni kuipa ridhaa Serikali mpya ya vyama vinayounda UKAWA madaraka ili kutatua kero hizi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na madaraja mbalimbali ya watumishi ambayo kimsingi hayaoneshwi na kuhuishwa kwenye ngazi za kiutumishi na mishahara yao stahiki. Mfano ngazi ya Madaktari Wasaidizi *(AMO'S),* wanaojiendeleza katika ngazi mbalimbali mfano wa Mionzi, Madaktari Wasaidizi Tiba na Magonjwa ya Ngozi (*AMO Dermatology*), Madaktari Wasaidizi Tiba na Upasuaji wa Jicho na Madaktari Wasaidizi wanaotoa huduma ya Dawa ya usingizi. Kundi hili hakika linamezwa katika mfumo mzima wa mapango wa ngazi za mishahara na madaraja ya kiutumishi kiasi kwamba haikubaliki wapate mafunzo halali kwa mitaala iliyopitishwa na Wizara Kitengo cha Mafunzo lakini utumishi hawazingatii taaluma zao na

matokeo yake wanakosa moyo wa kufanya kazi. Ni wakati sasa Serikali kuwa na mipango mizuri na kuiweka bayana kwa watumishi wao ili wapate maslahi mazuri na wafanye kazi zao vizuri kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za Serikali kukabiliana na ugonjwa huu wa malaria hususan katika maeneo ya Kanda ya Ziwa, zoezi la kunyunyizia dawa ya ukoko majumbani imefanyika na takribani nyumba 400,000 zimenyunyuziwa dawa hiyo, vyandarua vimegawiwa kwa wingi. Jambo la kujiuliza ni kwamba kila mara idadi ya wagonjwa wapya wa malaria katika vituo vya kutolea huduma inaongezeka na ilhali ya upatikanaji dawa na damu salama katika vituo hivyo ni ya kusuasua. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua, tangu zoezi hili limeanza ni awamu karibia tatu linafanyika lakini bado tatizo lipo palepale, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutafuta suluhisho la tatizo hili kwa kuongeza wigo wa tafiti ili kubaini tatizo la msingi ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kunyunyuzia dawa hizi kuwa ni muhimu na mbinu nyingine mfano uhamasishaji wa wananchi juu ya usafi wa mazingira, nyumba bora, matumizi sahihi ya dawa, kuhakiki maduka ya dawa baridi ya binadamu ambayo yapo kila kona ya mtaa, wataalam wetu hususan Maafisa Afya wametumiwa ipasavyo?

Je, tunao Maafisa Afya wa kutosha katika maeneo yetu? Haiwezekani unatoa chandarua ilhali huna uhakika mtumiaji ana kitanda cha ukubwa gani! Ndiyo maana badala ya vyandarua kutumika kukinga mbu, vyandarua hivyo tunaviona bustanini na sehemu nyingine kwenye mabanda ya kufugia kuku. Hali ya makazi ya wananchi wetu ni duni, baadhi ya wananchi hawana makazi ya kudumu mfano, baadhi ya jamii ya wafugaji, kundi hili muhimu unategemea litakuwa na makazi ya kudumu? Kundi hili litasaidiwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magonjwa yasiyoambukiza. Ni wazi na kweli kuwa sasa wimbi la magonjwa yasiyoambukiza limekuwa kubwa kiasi kwamba linagharimu Serikali pesa nyingi ilhali mikakati ya kupambana na magonjwa haya bado haijawa ya kuridhisha. Ni wazi kuwa suala la mfumo wa maisha tuliyo nayo unatofautiana sana baina ya waishio mjini na vijijini. Magonjwa hayo ni shinikizo la damu, kisukari, figo na kadhalika. Hali ya upatikanaji wa huduma muhimu za afya katika mazingira ya waishio vijijini bado ni ngumu kama wote tunavyofahamu. Uhakika wa kipato cha kugharamia matibabu ni mdogo sana na hivyo kupelekea watu kutojua hali zao za afya na hivyo kuwa na mtazamo hasi juu ya upimaji wa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeingia gharama kubwa sana kupeleka wagonjwa wengi wenye matatizo ya figo kutibiwa huko India kutokana na kutokuwa na vifaa vya kutosha kuhudumia wagonjwa hawa. Ni wazi na kweli kuwa mpaka sasa Serikali haijawekeza sana katika kuandaa rasilimali watu hususan katika fani mbalimbali kwa maana ya *succession plan*. Hii inatokana na kutokuwa na mpango wa kuandaa wataalamu kabla ili wapate uzoefu na pale wanapostaafu wakongwe basi nafasi zao ziwe tayari na watu wa kuzitumikia kuliko kusubiri mpaka wataalamu watakapotoka vyuoni ndipo wazibe hizo nafasi.

Ni wazi tukiwa na wataalam hao na vifaa vya kutosha, hakika tutapunguza gharama za sasa zinazotumika kuwasafirisha wagonjwa na matibabu yao kwa ujumla wake. Ni wazi kuna mabadiliko makubwa ya teknolojia hivyo basi na wataalamu wetu tukiwaandaa mapema itakuwa rahisi kuendana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya mama na mtoto. Serikali ilitoa taarifa kwa mara ya kwanza kwenye hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/201, kuwa zitasambazwa pikipiki za miguu mitatu almaarufu bajaj 400 ili zitumike kama *ambulance* ya kusafirisha wajawazito kwenda

hospitalini. Mpango huo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya afya tuulipinga kwani kwa mazingira halisi ya nchi yetu lisingeleta tija kwa sekta hiyo, sanasana lingeleta balaa katika kusafirisha akina mama wajawazito kwenda hospitali. Serikali ilibeza ushauri huo na sasa ni muda mwafaka kwa Serikali kutoa tathmini ya mafanikio au matatizo ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA DR ANTONY GERVASE MBASSA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2013)*

**1. UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi rehema kwa kunijalia afya njema kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya upinzani Bungeni kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuniamini na ushirikiano mkubwa anaonipa katika kuisimamia Serikali katika Wizara ya Afya na ustawi wa jamii. Nashukuru sana.

**Mheshimiwa Spika** napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana wenyeviti wenza wa UKAWA, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe Mwenyekiti CHADEMA,Mheshimiwa James Francis Mbatia mwenyekiti wa NCCR-MAGEUZI Taifa, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Haruna LIPUMBA mwenyekiti wa CUF, na Mheshimiwa Dr. Emmanuel MAKAIDI mwenyekiti wa NLD kwa kazi kubwa wanayoifanya kuunganishanguvu ya pamoja. Hakika UKAWA ndio mpango mzima na tumaini la wananchi. Aidha kwa moyo wa dhati napenda sana kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa ushirikiano wao mkubwa na wa dhati wanaonipa katika majukumu yangu ya kibunge, hakika nimefanya kazi hii kwa moyo mkunjufu na naahidi kuendelea kufanya kazi hiyo kamwe sitowaangusha bali nazidi kuwaahidi uwakilishi uliotukuka. Hakika kazi tuliyoianza wote mwaka 2010 mnaiona ilivyo leta mabadiliko na maendeleo ya kweli katika jimbo letu, hakika uzi ni uleule na kamba ni ileile katika kuhakikisha tunaivusha Biharamulo yetu. Pamoja tutasonga mbele, nawashukuru sana.

**Mheshimiwa Spika**, pianaishukuru familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu mkubwa na kwa jinsi wanavyonitia moyo hususan katika majukumu haya muhimu ya kuwatumikia wananchi. Mke wangu Benedicter Justinian, watoto wangu Thecla Mbassa, Bernard Mbassa na Beatha Mbassa. Nasema asanteni sana na muzidi kunivumilia sana.

**Mheshimiwa Spika,**kwa umuhimu wa kipekee niwashukuru watia nia ya urais waliojinadi wiki iliyopita kwa kukubaliana na kile ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisemea kuwa Serikali ya CCM imejaa rushwa, kutokuwajibika, kufanyakazi kwa mazoea, upendeleo katika kugawana keki ya Taifa, isiyoweza kuchukua uamuzi na uchafu mwingine mwingi. Watia nia hao wa Urais walikuwa na bado ni sehemu ya Serikali hiyo hiyo ya awamu ya nne iliyopo madarakani. Hakika kuna kila sababu kwa watanzania kuwapuuza watu kwa kuwa ni watu hao hao wa chama kile kile, maneno ni yale yale hawana uwezo wa kutuondoa kwenye tope walilotuingiza.

**2. MWENENDO WA BAJETI:**

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Wizara ya afya na ustawi wa jamii imeendelea kutekelezwa kwa kiwango kidogo mno kiasi cha kutokidhi mahitaji ya huduma kwa Watanzania wote. Wizara hii imekuwa kila mara inatengewa fedha ambazo kimsingi haziletwi toka hazina na kusababisha maisha ya Watanzania wengi kuwa rehani hususan wale waishio vijijini na wenye hali duni kifedha. Ni wazi na kweli kwamba ni Watanzania wachache sana wenye uwezo wa kusafiri na kutibiwa nje ya nchi yao. Hali hii si ya kunyamanzia hata kidogo kwani ni jukumu la serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora ya Afya na si vinginevyo.

**Mheshimiwa Spika,** mbali ya kuwa bajeti inayotekelezwa ni finyu bado lakini bado fedha hazitolewi kwa awamu zinazotakiwa kulingana na mpango wa wizara, bali fedha nyingi zinatolewa katika awamu ya mwisho wa mwaka (robo ya mwisho). Jambo hili linapelekea kwa kiwango kikubwa fedha hizo kutumika nje ya utaratibu na maksudio na hivyo kukosa tija.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya wizara ni kuwa fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 ni Tshs 305,729,492,000/- hadi Machi zilizopokelewa ni shilingi 73,723,224,000. Kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 8,800,000,000. Fedha zilizopokelewa ni sawa na asilimia 26.1 ya mahitaji hadi mwezi machi. Lakini mahitaji halisi ya wizara hadi kufikia mwezi machi yalikuwa ni shilingi 282,577,522,000/-. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua kiasi kilichosalia kitatolewa lini?

**Mheshimiwa Spika**,kwa mwenendo huo wa utoaji wa fedha za afya ni kweli Serikali hii ya CCM ina dhamira njema na afya ya watanzania?

**3. AZIMIO LA ABUJA:**

**Mheshimiwa Spika**, tangu azimio la Abuja lisainiwe mnamo April 2001 huko Abuja Nigeria, mpaka sasa azimio hilo limekuwa ni kitendawili kisichoteguliwa. Kwa kipindi chote cha miaka 15 serikali imeshindwa kutimiza agizo la kutenga asilimia 15 ya bajeti yake ya pesa za ndani kuhudumia wananchi wake. Kwa muda wote serikali imekuwa ikitenga kama ifuatavyo; 2010/11 (12.1%), 2011/12 (10.0%), 2012/13 (10.4%), 2013/14 (10.4%) na 2014/15 (10.2%). Mpaka leohii tumeshindwa kufikia lengo tulilo saini wenyewe kwa utashi wetu wenyewe bila kushurutishwa na mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Taifa lolote kama haliwezi kuwa na mipango thabiti ya kuimarisha Afya ya watu wake, hakika Taifa hilo haliwezi kuwa na maendeleo wala mafanikio katika ustawi wa wananchi wake. Ni lazima kama Taifa kuwa na juhudi za maksudi na za wazi za kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya nchi ili kuweza kuhudumia watu wake wapate afya bora na ustawi mzuri wa maisha.Tanzania kama nchi yenye rasilimali za kutosha tumeshindwa kuiga mfano nchi ndogo na tena maskini kama sisi mfano Rwanda,Botswana, malawi,Niger, Zambia na Burkina faso ambao wamefanikiwa walau kufikia tengeo la asilimia 15 kama walivyoahidi.

**Mheshimiwa Spika**, kambi rasmi ya upinzani Bungeni inapenda kujua kama tumeshindwa kutimiza azimio hilo la kutenga asilimia 15 ya mapato ya ndani, na sasa tunaanza kutekeleza BRN, jee tutafanikiwa au ni kuwa na mipango mingi ili hali hatuwezi kutekeleza!

**4. HALI YA UPATIKANAJI WA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI:**

**Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi imeendelea kuwa ya kutotosheleza katika vituo vya kutolea huduma. Hali hii inatokana na kutokuwepo upatikanaji mzuri wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika bohari yetu ya madawa (MSD). Aidha hali hii inapelekea wananchi kukosa huduma ya afya katika vituo vingi vya kutolea huduma.

**Mheshimiwa Spika,** suala la ukosekanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi limekuwa sugu kwa kipindi kirefu sana, na hii inatokana kutokuwa na dhamira ya dhati ya kupokea ushauri unaotolewa na kamati au kutokufikiria mbinu mbadala ya kuboresha huduma hii muhimu sana kwa wananchi wetu. Ni mara zote kambi rasmi ya upinzani Bungeni imekuwa ikitoa ushauri kwa serikali kufikiria suala la kuwa na mbia wa MSD ili kuleta hali ya ushindani katika kutoa huduma. Ushauri huu haukuwahi kufuatwa wala kutekelezwa hata kidogo.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utafiti inaonesha kuwa asilimia 76% ya maombi ya dawa kutoka kwenye ofisi za madawa za kanda kwenda kwenye vituo vya afya zinawasili zikiwa zimechelewa na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwenye vituo vya afya na asilimia 24% tu ya maombi ndiyo inayofika kwa wakati.

Aidha, kwa wastani asilimia 54% ya maombi ya ofisi za madawa za Kanda nayo yanacheleweshwa kwa kulinganisha na muda uliowekwa wa siku 14 lakini 20% ya maombi yanachukua kati ya siku 15 na 21 na asilimia 34% ya maombi yanachukua zaidi ya siku 21 hadi kupokelewa kwenye ofisi za kanda za madawa.

**Mheshimiwa Spika**, Hili ni tatizo kubwa la kiutendaji, ambalo kwa sasa ni wazi kabisa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kulipatia ufumbuzi. Ni vyema watanzania wakaachana na Serikali hii ya CCM ambayo imechoka na hivyo kushindwa kusimamia afya za watanzania na kuipa ridhaa Serikali mpya itakayokuwa chini ya Vyama vinavyoundwa na UKAWA ili iweze kuhakikisha afya za watanzania zinapewa kipaumbele.

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Masasi ni mfano wa kuigwa kupitia mfumo huu wa kuwa na mbia wa MSD. Ni hospitali ambayo suala la ukosekanaji wa dawa muhimu sasa halisikiki wala kufikiriwa na wananchi wa eneo hilo. Hakika hali hiyo imepelekea wananchi kuwa na ustawi mzuri na kuwa na afya bora. Hakika hali hii inapelekea wananchi kuwa na mwitikio mkubwa hata wa kujiunga na mfuko wa bima ya afya ya jamii. Ni wazi mwananchi anapochangia au kujiunga na mfuko wa Bima ya afya ya jamii na serikali ikatimiza wajibu wake wa kuwapatia huduma muhimu ya afya, hali hiyo inawafanya kuwa na mwitikio chanya wa huduma za afya. Lakini pale anapochangia na asiweze kupata huduma hiyo hakika hawezi kuwa na imani tena wala mwitikio mzuri.

**Mheshimiwa Spika,** wakati suala hili la Bima ya afya ya jamii linaanza katika Wilaya ya Igunga, kila halmashauri ilitenga muda na fedha kupeleka timu ya wataalamu kwenda kujifunza na kuona uhalisia wa suala lenyewe linavyotekelezwa. Leo hii bahati mbaya hatujapata mrejesho wa ufanisi wa suala hilo kwa sasa, kama wanazidi kufanya vizuri ni mbinu zipi za ziada wameongeza, ni mikakati ipi ya ziada iliyopo kwa hatua zaidi. Lakini pia mheshimiwa spika bado ni jambo la hekima hata kama mfuko huu umepatwa na msukosuko ni vema kuwa na maelezo ya kina ya sababu za msingi kwa nini mfuko huu umeshindwa kuendelea kutimiza adhima yake ya kuwahudumia wananchi kama ilivyokuwa hapo awali.

Ni nini sababu za msingi za kuporomoka kwa misingi imara iliyokuwa imewekwa na waasisi wa mfuko huu imekiukwa na waliofanya hivyo wamechukuliwa hatua gani za kiutendaji?

**Mheshimiwa Spika**, tunapoelekea kuwa na mfuko wa pamoja wa huduma ya afya kwa mwanchi, ni vema masuala haya yakapata ufafanuzi wa kina ili mwananchi aondokane na woga au mashaka juu ya uhakika wa huduma iliyokusudiwa na vilevile uhakika wa mchango wake atakao utoa utalindwa vipi na kufanikisha lengo lililokusudiwa. Sehemu nyingi wananchi hawapati taarifa sahihi za matumizi ya michango ya fedha zao zinafanya nini na hivyokupelekea kuleta mwitikio hasi wa wananchi kuchangia miradi mbalimbali ikiwemo hata

bima ya afya ya jamii. Ni wakati sasa Serikali kupitia Wizara hii kuwaeleza wananchi ni nini hatima ya afya zao hapo baadae maana wamekosa imani hususan wazee, wastaafu, akina mama na wajane ambao hao wote wana beba mzigo mkubwa wakulea watoto yatima na wajukuu walioachwa na wazazi wao.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya shirika la afya la Dunia-WHO ya mwaka 2014 inasema kuwa tatizo kubwa sanahapa nchini la upatikanaji wa madawa muhimu hasa kwenye vituo vya afya vya Serikali. Inaendelea kueleza kuwa mara zote madawa muhimu kwenye vituo hivyo hayapatikani.

Aidha**, Mheshimiwa Spika**, takwimu za WHO kuhusiana na upatikanaji wa madawa muhimu kati ya vituo vya afya vinavyomilikiwa na serikali na vile vya binafsi zinaonesha kwa vituo vya serikali ni 24% wakati kwa vituo vya binafsi ni takriban mara mbili yake yaani 47.9%

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, takwimu hizo za WHO inazitolea tafsiri kuwa, madawa yanayosambazwa na MSD yanafika kwenye vituo binafsi kabla ya kufika kwenye vituo vya Serikali. Hivyo basini jukumu la watendaji kuangalia chanzo cha tatizo hilo ni nini hasa. Au kuna uwezekano mkubwa watumishi katika vituo vya afya vya umma ndio wamiliki wa vituo binafsi na hapo ndipo mgongano wa maslahi unapoingia.

**5. UTENDAJI WA BOHARI YA MADAWA NA DENI LA SERIKALI:**

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa utendaji kazi wa MSD unazidi kushuka kadri siku zinavyokwenda mbele,hii inatokana na ukweli kwamba fedha za uendeshaji wa taasisi hiyo (working capital) umeendelea kushuka kwa zaidi ya asilimia 69% katika kipindi cha miaka 5 kutoka shilingi bilioni 81 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 25 mwaka 2015. Jambo hili limepunguza uwezo wa MSD kuagiza madawa yanayokidhi mahitaji ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** suala la kushuka kwa mtaji wa uendeshaji linaweza kuwa limetokana na menejimenti ya MSD kushindwa kufanyakazi yake kama inavyotakiwa. Aidha inaweza kuwa imetokana na uwezo mdogo wa uongozi huo kuweza kuongoza taasisi hiyo, kwani Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini taasisi hiyo inatakiwa ijiendeshe kibiashara. Kama ndio hivyo inakuwaje wanashindwa kufanyakazi kwa mujibu wa sheria na kanuni zinavyohitaji? Pia ni muda mwafaka sasa kuwa na watendaji wakuu wa MSD wenye uwezo wa uendeshaji na sio tu kwakuwa ni wafamasia tu, bali wawe na utaaalam wa uendeshaji wa biashara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la deni la bohari kuu ya madawa limekuwa halina majibu sahihi na tafsiri ya kweli. Kila mwaka deni limekuwa aidha likiongezeka na hali au kasi ya ulipaji wa deni hilo ikiwa ndogo sana. Inasikitisha kuona kuona wananchi wanakosa dawa na vifaa tiba ili hali serikali inashindwa kulipia sehemu ya deni lake. Kila mara majibu ya serikali yanasema kuna sehemu ya deni halijahakikiwa!

**Mheshimiwa Spika**,ni wakati sasa Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata jibu ni lini hesabu kamili itahakikiwa na kupata jibu sahihi kuhusu deni hilo, isije kuwa kila siku deni linaongezeka ili hali ni kichaka cha kuficha maovu na hivyo kuonekana kinacholipwa ni deni hewa!

**Mheshimiwa Spika**, sehemu kubwa ya deni hili inasemekana nikugomboa dawa na vifaa tiba tunavyopewa kama misaada toka kwa wahisani mbalimbali hapo bandarini! Jambo la kushangaza ni dawa zipi ambazo hata zikiletwa hazifiki kwa wahitaji huko vijijini? Lakini wakati huo kuna ongezeko kubwa sana la madawa ambayo yameisha muda wake hapo ghalani. Sasa suala la kujiuliza ni kwa nini tupoteze fedha nyingi kugomboa dawa ambazo muda wake wa kutumika umefika ukingoni au kuisha kabisa, tunapopokea misaada hiyo huwa tunajiuliza

masuala hayo au basi inakuwa huku kwetu ndiyo maeneo muafaka ya kutupia au kuteketezea dawa zao ambazo zimeisha muda waake?

**Mheshimiwa Spika**, ifike mahala sasa hata kama tunategemea misaada tujisimamie na tuseme hapana imetosha. Suala hili inatugharimu mara mbili zaidi, kwani tunagharimika kugomboa dawa hizo bandarini lakini tunagharimia pia kuziteketeza dawa hizo kwa gharama kubwa, haiwezekani kuendelea kupokea missada isiyokuwa na tija kwa taifa na wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kambi rasmi ya upinzani bungeni inapenda kupata jibu la uhakika ni lini sasa hesabu hizi zitahakikiwa na kupata jibu kamili ili serikali ilipe deni hilo na wananchi waache kutaabika kwa kukosa dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma.

**6. DENI LA MATIBABU NJE YA NCHI:**

**Mheshimiwa Spika**, suala la deni la matibabu nje ya nchi linazidi kuongezeka kila uchao, na hakika si heshima kwa nchi yetu hata kidogo. Tanzania tunaongoza kwa kwa kuwapeleka wagonjwa wetu Hospitali za nchini India na pia tunaongoza kwa kutolipa deni la hospitali hizo za nchini India, hii ni hatari kubwa sana. Inasikitisha kuona ni tabaka la watu wachache tu wanaoweza kwenda kuhudumiwa huko ili hali haki ya kupata huduma bora ni ya watanzania wote.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi tunayo rasilimali watu hapa kwetu nchini yaani Madaktari na Wauguzi hodari na fani nyinginezo, wataalamu hawa wameshirikishwaje katika kutoa ushauri wao ili kusudi serikali iweze kuja na mpango mahsusi wa kutengeneza mazingira ya wao kutumia taaluma yao kuwahudumia wananchi. Tunao madaktari bingwa lakini kila mara hawana vitendea kazi katika idara zao, hii ni sawa na kumpeleka mvuvi hodari kina kirefu cha bahari wakati hana vifaa vya kuvulia hao samaki, atafanya nini? Ni wakati sasa serikali kuwatumia wataalamu hawa na kuwasiliza ili ushauri wao uweze kufanyiwa kazi na wapatiwe vifaa vya kutosha watumie taaluma yao kusaidia wananchi wanyonge hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ni wakati sasa serikali kufikiria kununua vifaa tiba na vitendanishi ili kuboresha huduma za wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kubwa ambazo zingeweza kufanyika hapa nchini lakini inabidi wakatibiwe nje ya nchi hali inayoongeza uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha, gharama za malazi, usafiri na hata nafasi ya familia kutoa huduma kwa wapendwa wao wanao hitaji uuangalizi maalum wa wanafamilia.

**Mheshimiwa Spika**, Ni wazi gharama za kuwapeleka wagonjwa hawa huko nje ya nchi kwa matibabu kama zikitumiwa vizuri kununua vifaa tiba na vitendanishi, hakika litakuwa ni suruhisho kwa mahitaji ya wagonjwa wengine watakao hitaji huduma hiyo, nahii itarahisisha hata kupata wataalamu wengine kutoka nje ya nchi. Tumekuwa natatizo kubwa la wataalamu wetu kwenda kufanya kazi nje ya nchi lakini moja wapo ya sababu ni kukosekana kwa hivi vifaa tiba na vitendanishi jambo ambalo linawafanya wasiweze kutumia taaluma yao vizuri na kupoteza muda wao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri serikali kulipa deni la hospitali za India haraka iwezekanavyo ili kupisha hali ilivyo sasa, kwani mpaka sasa tunadaiwa zaidi ya bil 17 na kila uchao wagonjwa hawa wanazidi kupelekwa huko. Tunaitaka serikali sasa kufikiria kununua vifaa tiba na vitendanishi ili kazi hiyo iweze kufanyika hapahapa nchini. Serikali itengeneze mazingira bora ya kuwa na mikataba na madaktari toka nje ya nchi waweze kutoa huduma hapa nchini na hii itaongeza morali ya kazi na pia kutengeneza mazingira ya urafiki katika kutoa huduma bora.

**7. RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi 2007 hadi 2017 (MMAM) na mpango mkakati wa rasilimali watu sekta ya afya 2008/15 iliweka mikakati ya kuongeza watumishi katika sekta hiyo. Ni wazi na kweli ulikuwa mkakati dhati na wenye malengo mazuri. Lakini jambo moja mpaka sasa hakuna taarifa za wazi zinazoonyesha moja ni jinsi gani mpango huu umefanikiwa kuhuisha na kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa na vigezo muhimu katika sekta hii ya afya. Leo tuna muda mfupi sanaMMAM kukamilisha muda wake na wakati bado hali halisi ya watumishi katika sekta ya Afya bado hairidhishi kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua mpaka sasa MMAM imefaniwa kwa kiasi gani katika kufanisha mpango huo? Kwani mpaka sasa mipango imekuwa mingi nabado sasa tunazidi kuongeza BRN! Je tutafanikiwa kukamilisha miradi na mipango tuliyonayo katika muda uliopangwa?

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana ya watumishi wa sekta ya afya hapa nchini. Hii inatokana na kutopandishwa vyeo kwa muda muafaka, kutolipwa stahili zao kwa muda na mbaya zaidi mtumishi anapojiendeleza katika kada yake hucheleweshewa kubadirishiwa mshahara wake na stahili zake mbalimbali. Hali hii inawafanya baadhi ya watumishi wakate tamaa ya kujiendeleza na wengine kufikiria sasa ni bora kuhamia fani nyingine kwani maslahi yao hayatekelezwi pamoja na kutimiza wajibu wao.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na madaraja mbalimbali ya watumishi ambayo kimsingi hayaoneshwi na kuhuishwa kwenye ngazi za kiutumishi na mishahara yao stahiki. Mfano ngazi ya madaktari wasaidizi (AMO'S), wapo wanaojiendeleza katika ngazi mbalimbali mfano madaktari wasaidizi wa mionzi (AMO radiology), madaktari wasaidizi tiba na magonjwa ya ngozi (AMO dermatology), madaktari wasaidizi Tiba na upasuaji wa jicho (AMO Ophthalmology and cataract surgery) na madaktari wasaidizi wanaotoa huduma ya dawa ya usingizi (AMO anaesthesia). Kundi hili hakika linamezwa katika mfumo mzima wa mapango wa ngazi za mishahara na madaraja ya kiutumishi kiasi kwamba haikubali wapate mafunzo halali kwa mitaala iliyopitishwa na wizara kitengo cha mafunzo lakini utumishi hawazingatii taaluma zao na matokeo yake kuthamini zaidi wale wanaohitimu mafunzo kwa ngazi ileile upande wa afya ya kinywa na meno tu!

**Mheshimiwa Spika**,ni wakati sasa serikali kuwa na mipango mizuri na kuiweka bayana kwa watumishi wao ili wapate maslahi mazuri na wafanye kazi zao vizuri kwa mujibu wa taratibu sahihi za kiutumishi.

**8. UDHIBITI WA MALARIA**

**Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za serikali kukabiliana naugonjwa huu wa malaria hususan katika maeneo ya kanda ya ziwa, zoezi la kunyunyizia dawa ukoko majumbani imefanyika na takriban nyumba 400,000 zimenyunyiziwa dawa hiyo, vyandarua vimegawiwa kwa wingi. Jambo la kujiuliza ni kwamba kila mara idadi ya wagonjwa wapya wa malaria katika vituo vya kutolea huduma inaongezeka na ili hali ya upatikanaji dawa na damu salama katika vituo hivyo ni ya kusuasua.

**Mheshimiwa spika**, Kambi rasmi ya upinzani bungeni inapenda kujua, tangu zoezi hili limeanza ni awamu karibia tatu linafanyika lakini bado tatizo lipo palepale, Je serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kutafuta suruhisho la tatizo hili kwa kuongeza wigo wa tafiti ili kubaini tatizo la msingi ni nini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kunyunyizia dawa ni muhimu kuwa na mbinu nyingine mfano uhamasishaji wa wananchi juu ya usafi wa mazingira, nyumba bora, matumizi sahihi ya

dawa, kuhakiki maduka ya madawa baridi ya binadamu ambayo yapo kila kona ya mtaa. Pamoja na hayo wataalam wetu hususan maafisa afya wametumiwa ipasavyo? Je tunao wa kutosha katika maeneo yetu. Haiwezekani unatoa chandarua ili hali huna uhakika mtumiaji ana kitanda cha ukubwa gani! Na ndio maana badala ya vyandarua kutumika kukinga mbu, vyandarua hivyo tunaviona bustanini na sehemu nyingine kwenye mabanda ya kufugia kuku. Hali ya makazi ya wananchi wetu ni duni, baadhi ya wananchi hawana makazi ya kudumu mfano baadhi ya jamii ya wafugaji, kundi hili muhimu unategemea litakuwa na makazi ya kudumu? Kundi hili litasaidiwaje?

**9. UDHIBITI WA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA**

**Mheshimiwa Spika,**ni wazi na kweli kuwa sasa wimbi la magonjwa yasiyoambukiza limekuwa kubwa kiasi kwamba linagharimu serikali pesa nyingi ili hali mikakati ya kupambana na magonjwa haya bado haijawa ya kuridhisha. Ni wazi kuwa suala la mfumo wa maisha tuliyo nayo unatofautiana sana baina ya waishio mjini na vijijini. Magonjwa hayo ni shinikizo la damu, kisukari, figo n,k. Hali ya upatikanaji wa huduma muhimu za afya katika mazingira ya waishio vijijini ni ngumu kama wote tunavyofahamu. Uhakika wa kipato cha kugharimia matibabu ni mdogo sana na hivyo kupelekea watu kutojua hali za afya zao na hivyo kuwa na mtazamo hasi juu ya upimaji wa hiari wa afya zao.

**Mheshimiwa Spika**, serikali imeingia gharama kubwa sana kupeleka wagonjwa wengi wenye matatizo ya figo kutibiwa huko India kutokana na kutokuwa na vifaa vya kutosha kuhudumia wagonjwa hawa. Ni wazi na kweli kuwa mpaka sasa serikali haijawekeza sana katika kuandaa rasilimali watu hususan katika fani mbalimbali. Na hii inatokana na kutokuwa na mpango wa kuandaa wataalamu kabla ili wapate uzoefu na pale wanapostaafu wakongwe basi nafasi zao ziwe tayari na watu wa kuzitumikia kuliko kusubiri mpaka wataalamu watakapo toka vyuoni ndipo wazibe hizo nafasi. Ni wazi tukiwa na wataalam hao na vifaa vya kutosha hakika tutapunguza gharama za sasa zinazotumika kuwasafirisha wagonjwa hawa na matibabu yao kwa ujumla wake. Ni wazi kuna mabadiriko makubwa ya teknolojia hivyo basina wataalamu wetu tukiwaandaa mapema itakuwa rahisi kuendana na mabadiriko hayo.

**Mheshimiwa Spika**, suala la ugonjwa saratani linatisha na kushutua sana, hali hii inatokana na kutokuwa nauchunguzi wa mara kwa mara kuhusu afya zetu. Hakika suala hili ni kubwa sana japo takwimu tunazozipata ni wale wachache wanao weza kufika kwenye vituo vikubwa vya huduma. Lakini vijijini kuna idadi kubwa sana ya watu wenye matatizo ya saratani ambao wanapoteza maisha kwa kukosa elimu na pia kupimwa mapema na kupewa matibabu yanayostahili. Ni wazi saratani ikigundulika mapema yaweza kudhibitiwa na hivyo kurefusha maisha. Kambi rasmi ya upinzani inaitaka serikali kuweka mikakati ya dhati ya kuongeza vifaa tiba, na pia wataalamu ili kusogeza huduma hii katika hospitalizetu za mikoa na wilaya. Aidha kwa kufanya hivyo tutaokoa maisha ya walio wengi.

**10. AFYA YA MAMA NA MTOTO**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa taarifa hiyo kwa mara ya kwanza kwenye hotuba ya bajeti ya Mwaka 2010/2011, kuwa zitasambazwa bajaj 400 ili zitumike kama 'ambulace'ya kusafirisha wajawazito kwenda hospitalini. Mpango huo Kambi Rasmi yaUpinzani Bungeni pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya afya ililipinga kwani kwa mazingira halisi ya nchi yetu lisingeleta tija kwa sekta hiyo, Sanasana lingeleta balaa katika kusafirisha wakinamama wajawazito kwenda hospitali.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilibeza ushauri huo, sasa ni muda mwafaka kwa Serikali kutoa tathmini ya mafanikio au matatizo ya mpango huo.

**11. MAGONJWA YANAYOTOKA KWA WANYAMA NA KUSHAMBULIA BINADAMU**-*ZOONOTIC DESEASES*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika mawasilisho yake ilitoaushauri kwa Serikali kuwa na maabara ambazo zitaweza kugundua kwa haraka magonjwa ambayo yataambukizwa kutoka kwa wanyama. Magonjwa hayo yanaweza kusabishwa na bakteria na virus. Hii ni kutokana na sababu kubwa kwamba pindi magonjwa hayo yanapotokea Serikali inatumia fedha nyingi sana ili kukabilianoa nayo.Magonjwa **kama Dengue, mafua ya ndege na chikungunya.**

**Mheshimiwa Spika**, mbali na mafua ya ndege ambayo pindi yanapotokea, karantini zinawekwa, pia kuna magonjwa mengine ambayo sio ya mlipuko kama yale yanayoambukizwa nabakteria anaeitwa "***Brucella abortus***"na kusababisha ugonjwa unaoitwa brucellosis kwa wale wanaotumia bidhaa zitokanao na mifugo hasa ng'ombe.

**Mheshimiwa Spika,** tulitoa ushauri huu kutokana na ukweli kwamba jamii kubwa ya watanzania inajihusisha na mifugo au inaishi katika maeneo ambayo yanamifugo. Hivyo dalili za magonjwa hayo au uambukizwaji wa magonjwa hao haziwezi kugundulika kwa kutumia maabara zetu za ma-hospitalini. Je hadi sasa ushauri umefanyiwa kazi kwa kiwango gani?

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

**…………………………………………..**
**Dr. Antony Gervase Mbassa (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni-Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.**
**02.06.2015**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dokta Mbassa. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hamad na Mheshimiwa Raya Ibrahimu Khamis ajiandae.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii ya Afya. Naomba ni-*declare interest* kabla sijazungumza. Namshukuru Mwenyezi Mungu kutupa afya na uzima na kupata nafasi ya kukutana tena na kupata nafasi pia ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niushukuru uongozi wa Bunge kwa kuendesha shughuli Bunge vizuri licha ya changamoto nyingi tunazoziona. Maana Bunge ninaloliona mimi na lile la zamani linashangaza sana. Shukrani za pekee ziende kwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti, Katibu wa Bunge na Watendaji wote kwa kutusaidia Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi zetu. Nawapongeza sana wapiga kura wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa imani walionionyesha na nawahaahidi kwamba sitawachoka, nawapenda wote na nitaendelea kuwapa ushirikiano kwa muda huu wote. Kwanza, kabla sijasahau, naomba niunge mkono hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie ufinyu wa bajeti ya Wizara hii. Wizara hii inapata hela ndogo sana kutokana na huduma nyingi walizonazo wanashindwa kutekeleza majukumu yao mengi. Niwape pongezi wa wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya popote walipo kwa kufanya kazi kwa kujitoa na ujasiri. Fani yetu sisi watu wa afya ni ngumu sana na hatuna mashamba ya bibi ya kulima ili tuongeze kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fani hii hata ukitupa mashamba ya kulima hatuna muda wa kulima kwa sababu tunajitoa kwa ajili ya wagonjwa wote. Tunapata faraja sana tukiona wagonjwa tunaowatibu wamepona, wako wazima na tunawakuta barabarani wanafanya shughuli zao. Tunasema Mwenyezi Mungu atupe moyo wa juhudi tuweze kuwasaidia wote wenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zetu siyo za kubahatisha wala si za kufanyia majaribio. Kwa hivyo, tutafarijika sana kuona kwamba tunapatiwa vitendea kazi vya kutosha ili tuweze kutekeleza majukumu yetu. Tutaongozwa na utashi wa mapenzi kwa wagonjwa wetu na vitendea kazi vikiwepo basi tunashukuru sana tutaongeza juhudi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, bajeti ya Wizara hii ni tegemezi inasaidiwa sana na wafadhili. Mashirika 52 yanasaidia Wizara hii, washirika wa maendeleo 66 wanasaidia Wizara hii na watu binafsi na *NGOs* zisizopungua 45 zinasaidia Wizara hii. Mpaka mimi nafikiri laiti kama hawa wangekuwa hawa hawakuwepo Wizara ya Afya ingekuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya uamuzi mzuri tu nchi za Afrika tulipokutana tukaja na Azimio la Abuja. Katika Azimio hili tulikubaliana kwamba 15% ya bajeti ya Serikali iingie kwenye sekta ya afya na ingesaidia sana kwenye huduma zetu za afya. Hadi hii leo uamuzi huu haujaweza kutekelezwa. Bado tunaendelea kukimbizana na miradi inayofadhiliwa na wafadhili tunajua wana matakwa yao na mambo yao ambayo yanataka yatekelezwe. Naomba Serikali ifikirie, kama ilivyofikiria kuisaidia Wizara ya Miundombinu, sasa angalau tunatengeneza barabara zetu kwa kutegemea bajeti yetu, tufike mahali na Wizara ya Afya tuweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie masuala ya *MSD*. Shirika hili linatusaidia sana kwa ajili ya dawa lakini linashindwa kufanya kazi zake kutokana na madeni makubwa inayoidai Serikali. Mpaka sasa *MSD* inadai zaidi ya shilingi bilioni 100, hivi unafikiria kama ni duka la mtu binafsi si angekuwa amefilisika. Niombe basi Serikali ifirikie kuipa *MSD* pesa zake inazodai na iongezwe za ziada ili iweze kutoa huduma inayohitajika. Naisihi Serikali ione umuhimu wa kuisaidia *MSD* kwa kuilipa fedha zake na kuipa fedha za ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kuzungumzia ni hospitali ya *Ocean Road*. Hospitali hii tunahitaji tuitazame kwa macho mawili au matatu kwa sababu pesa zinazotumika ni nyingi sana, hawapati hela ya kutosha, dawa za kutibu kansa ni ghali sana na hazipatikani madukani, bajeti inayotengwa ni ndogo na haitolewi yote. *Dose* moja tu ya dawa hizi za kansa inafika shilingi laki tatu, mnyonge ataweza wapi? Serikali imesema itatoa bure lakini kwa watu wote haiwezi, tunafanyaje? Vifaa vya kutibu magonjwa ya kansa ni pesa nyingi sana na havipatikani kwenye maduka ya madawa mpaka uagize. Licha ya juhudi kubwa inazofanya Wizara hii, Wizara hii isaidiwe kuona umuhimu wa *Ocean Road* kuweza kutibu wagonjwa wa kansa wasikate tamaa, wengi wanafia vijijini hawafiki katika hospitali.

Naishauri Serikali kama tulivyokuwa tunawasaidia wengine, basi maduhuli wanayokusanya Wizara hii yarudi kwenye Wizara yaweze kuziba pengo dogo kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wa kansa wa *Ocean Road. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Hospitali ya Muhimbili. Wodi ya wazazi wanalala wawili au watatu kwenye magodoro. Nafikiri sasa wakati umefika wa ku-*decongest* Muhimbili. Tunafanya nini? Tujitahidi basi hizi hospitali zetu za Amana, Ilala na sehemu wodi za *maternity* tuziboreshe, tuongeze na vitanda, tuongeze na *Nurse Midwives* na Madaktari wanaohusika ili

wagonjwa wengi watibiwe kule, wanaokwenda Muhimbili iwe ni *real referral case* ili wawe wachache. Naomba tufanye hilo ili tuisaidie mzigo mzito ilionayo Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa juhudi zinafanywa na Wizara ya Afya za kujenga Hospitali ya Mloganzila ambayo ni *teaching hospital,* nawapongeza sana. Hospitali hii inategemea sana ufadhili. Naomba kama tutaendelea hivyo na Serikali ikaachia Wizara tu itafute wafadhili itakuwa ni kazi sana. Naomba hospitali hii isaidiwe ili imalizike kujengwa kwa haraka kwani itatusaidia sana na ikiwezekana kukamilika kwa wakati bila wafadhili itakuwa ni jambo la busara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni *TFDA*. Watu hawa wanafanya kazi vizuri na chombo hiki ni kizuri sana cha kulinda afya zetu. Mambo makubwa tunayoyafanya, sisi wenyewe ni wafanyabisahara. *TFDA* iliweka lengo la kupunguza kiwango cha dawa, vyakula na vipodozi na vifaa tiba duni na bandia kwa asilimia hamsini ifikapo 2013, sasa tuko 2015, hebu watuambie wamefikia lengo gani? Lengo hilo walilolipanga kweli limefikia? Je, inawezekana kupunguza bidhaa zisizo na ubora na zisizo na tija kwa kufanya ukaguzi?

Je, wanakagua, wanafikia maeneo yote? Navyoona sasa hali inazidi kutisha kidogo. Baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kuingiza bidhaa ambazo hazina ubora na zisizo na tija. Tunakuta tu kunabadilishwa magaloni ya *tomato* mapya lakini ukiiangalia *tomato* inakuwa kama gundi lakini ukilitazama *gallon* ni jipya na *label* ni mpya lakini kilichomo ndani mle ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, kule nyumbani tuna mchele wa mapembe, unabadilishwa viporo tu, vya rangi ya kijani, rangi nyekundi, mara leo unaambiwa unaitwa hivi kesho unaitwa vile, lakini ukiula kama chicha.

Niombe sasa wakati umefika wale ndugu zetu wafanyabisahara ambao hawana uaminifu wanaoamini kwenda India wanaochukua mchele na ku-*polish* tu unawekwa na mafuta kidogo halafu unabadilishwa na viporo unakuja nyumbani lakini sidhani kama wananunua mchele uliokuwa *produced* mwaka huu 2015 au 2014 yote hiyo ni kutaka faida kubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba nimuite Mheshimiwa Azza atafuatiwa na Mheshimiwa Raya na Mheshimiwa Grace Kiwelu ajiandae.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru wanawake wa Mkoa wa Shinyanga kwa kuniamini na naomba waendelee kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya imekuwa ikipewa bajeti ndogo sana na hata bajeti kidogo inayokuwa imetengewa hailetwi yote kwa asilimia 100. Suala hili linaifanya Wizara ya Afya kufanya kazi kwa kusuasua na kutotimiza yale ambayo walikuwa wamekusudia.

Naomba sana bajeti ya Wizara iweze kuongezwa kwa sababu ndiyo Wizara mama ambayo kila mtu anaitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze madaktari, manesi na wauguzi kwa kufanya kazi ngumu na kwenye mazingira magumu. Wanafanya kazi kutoka ndani ya nafsi zao. Naiomba Serikali iwatazame watu hawa kwa macho mawili kwa sababu bila wao hakuna ambaye anaweza akasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niingie katika Mkoa wa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga kuna ujenzi wa hospitali ya rufaa. Ujenzi huu wa hospitali ya rufaa gharama ya kukamilisha ujenzi huu ni shilingi bilioni mia moja. Nikiangalia namna ambavyo fedha zinatoka, shilingi bilioni mia moja mpaka sasa hivi tumekwishapewa shilingi bilioni moja peke yake, inakatisha tamaa. Sioni kwa nini tunasema tunajenga hospitali ya rufaa wakati fedha ya kujengea hospitali hii haitoshi. Kwa thamani ya shilingi bilioni mia moja unatoa bilioni moja, ujenzi wa hospitali hii utakamilika baada ya miaka mingapi? Namuomba Waziri atakapokuja kujibu aniambie wamejipanga vipi kuhakikisha kwamba badala ya kuwa wanatuletea shilingi bilioni moja wabadilishe utaratibu mwingine ili hospitali ikamilike na kutoa huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa wa Shinyanga imekuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa na hili kila ninaposimama humu ndani nalisema lakini sielewi kwa nini mmeamua kuziba masikio na kutokusikiliza kilio cha wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. Tuna hospitali moja tu ya Wilaya ambayo ipo Wilaya ya Kahama lakini Wilaya nyingine zote hatuna Hospitali za Wilaya. Tumejitahid kuanzisha Hospitali za Wilaya kwa nguvu zetu na nguvu za Halmashauri lakini bado utoaji wa fedha wa Serikali unakuwa wa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Kahama inapokea idadi kubwa ya wagonjwa kwa sababu inahudumia mpaka wagonjwa kutoka mikoa ya jirani kama Geita na Tabora kwa maana ya Bukene. Ukiangalia dawa wanazopelekewa Hospitali ya Wilaya ya Kahama hazitoshelezi kabisa ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa ambayo inapokea. Sijui Serikali ina mpango gani na Hospitali ya Wilaya ya Kahama kuhakikisha wanaongeza gawio la dawa kutokana na huduma ambazo wanazitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwa uhalisia Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu, lakini Wilaya ya Kahama ndiyo imezungukwa na migodi, huduma zinazotoka hazifanani na wingi wa wagonjwa wanaokwenda kupata huduma. Madaktari, Manesi na Wauguzi waliopo katika Hospitali ya Kahama hawatoshelezi ukilinganisha na watu wanaokwenda kuhudumiwa katika Hospitali ya Kahama.

Naiomba na naisihi Serikali iangalieni kwa jicho la huruma Hospitali ya Wilaya ya Kahama lakini muwahurumie pia Madaktari, Manesi na Wauguzi wanaotoa huduma pale kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu na wanahudumia watu wengi zaidi ya uwezo walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka Wilaya ya Kahama, naomba niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu tumeanzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, majengo yote yamekamilika, tumewaomba Serikali basi vile vifaa mtuletee ili hospitali hii ya Wilaya iweze kufanya kazi. Tumeomba kibali lakini mpaka hivi tunavyoongea hakuna ambalo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Seif amefika katika Hospitali ya Wilaya ya Kishapu, ameona ujenzi wa hospitali ile lakini mpaka sasa sijui ana

majibu gani? Mheshimiwa Waziri naomba niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo anakushukuru kwa kufika katika Jimbo lake lakini yale mliyokubaliana ulipofika Kishapu hakuna hata moja ambalo limetekelezwa. Nakuomba sana na nawaomba sana muangalie majengo yale yanachakaa, yameshaisha lakini hayafanyi kazi, thamani ya pesa inakuwa haipo. Namwomba Mheshimiwa Waziri akisimama ajibu yale aliyoahidi akiwa katika Halmashauri ya Kishapu yamefikia wapi na kibali cha kuanza Hospitali ya Wilaya ya Kishapu kimefikia wapi mpaka leo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini tumeanzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Rais alifika pale akaahidi na akaomba tuandike ombi maalum kwa ajili ya ujenzi ule, tumeanzisha kwa nguvu zetu wenyewe. Ahadi ile alivyoitoa Mheshimiwa Rais mpaka leo hakuna hata shilingi moja iliyokuja. Halmashauri imekuwa ikiandika ombi maalum kila mwaka lakini hatujawahi kupewa hata shilingi kumi. Haitoshi, Waziri Mkuu amefika mpaka pale kwenye ujenzi ule, ameahidi na akasema atasimamia ombi lile maalum lakini mpaka leo ombi lile maalum hatujawahi kupewa hata shilingi kumi. Tumewakosea nini Wanashinyanga? Kila siku tunasimama humu tunalia na tunaongea lakini kila tunapoleta maombi maalum hata shilingi moja hatupewi. Kuna sababu gani za msingi kama Mheshimiwa Rais aliahidi na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi lakini bado hatupati fedha hizi, labda mtuambie tufanye nini ili tuweze kupata fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majengo ambayo yamekamilika kama jengo la *OPD* kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga basi tupewe kibali ili majengo yaliyokamilika yaanze kufanya kazi, napo ni tatizo. Mimi nadhani Wizara mnafurahia msongamano uliopo katika Hopitali ya Mkoa ndiyo maana hayo tunayoyaomba yote hakuna hata moja ambalo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Manispaa ya Shinyanga ndipo ilipo Hospitali yetu ya Mkoa wa Shinyanga, wananchi wote waliopo Manispaa ya Shinyanga wanapata huduma katika Hospitali ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie muda huu kuwapa pole sana Madaktari, Manesi na Wauguzi waliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kwani wanafanya kazi kubwa na ngumu kutokana na msongamano uliopo pale lakini hii yote mnaisababisha Wizara kwa sababu hamtaki kuhakikisha kwamba Halmashauri nyingine zinapata hospitali zao na kufanya kazi. Hatuwatakii mema Madaktari, Manesi na Wauguzi waliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kwa sababu wanafanya kazi mpaka unawahurumia, msongamano ni mkubwa sana. Waziri wa Afya umefika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga umejionea mwenyewe lakini sijui kwa nini kunakuwa na kigugumizi cha kutoa vibali vya hospitali nyingine zianze kufanya kazi ili kupunguza msongamano uliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, Manispaa ya Shinyanga ina Kituo cha Wazee Kolandoto. Vituo vyote hivi vya wazee vinahudumiwa na Wizara ya Afya. Hata mwaka jana niliposimama nilisema kwamba Kituo cha Wazee Kolandoto kipo katika hali mbaya, nyumba zinataka kuanguka lakini sijaona kitu chochote ambacho kimefanyika. Bado fedha ambazo zinatakiwa kwenda kwenye vituo hivi kikiwemo na cha Kolandoto haziendi kwa wakati, hata upatikanaji wa chakula nao umekuwa wa shida na upatikanaji wa dawa umekuwa wa shida. Mimi naomba Waziri utakaposimama uniambie kwa sababu hata mwaka jana kwenye bajeti nilikisemea Kituo hiki cha Wazee cha Kolandoto kilichopo Manispaa ya Shinyanga lakini mpaka leo sijapata majibu yoyote na wala sielewi mna mpango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Manispaa ya Shinyanga kuna kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu wa ngozi. Mwaka jana niliposimama hapa nilisema kwamba kituo kile hakina huduma za afya, hakina zahanati, kituo kile ni kikubwa, tunawaweka katika mazingira gani watoto wenye ulemavu wa ngozi. Tuliomba angalau tupewe zahanati na *ambulance* katika kituo kile lakini mpaka leo hakuna ambacho kimefanyika. Namwomba Waziri atakaposimama aniambie toka mwaka jana nilipochangia na nilipouliza swali kuhusu kituo cha Buhangija cha watoto wenye ulemavu wa ngozi wamekipelekea nini mpaka sasa hivi ninavyochangia. Kwa sababu wale ni watoto wetu, tunapoiachia Manispaa ya Shinyanga peke yake na kituo kile kinalea watoto wa Kanda yote ya Ziwa, Manispaa ya Shinyanga inashindwa kumudu wingi wa huduma zinazotakiwa katika kituo kile na hili lipo katika Wizara ya Afya lakini hakuna ambacho mmekifanyia kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Raya atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiweli na Mheshimiwa Sylvestry Koka ajiandae.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Napenda kuchangia hususani katika maslahi ya Madaktari ama Wauguzi wetu katika hospitali zetu. Kuna *Medical Officer Assistant* ambao wanafanya kazi hospitalini na baadaye wanapata nafasi ya kwenda kuongeza taaluma yao. Wanaongeza taaluma katika nyanja mbalimbali kama mambo ya mionzi, macho, ngozi na mengineyo lakini unakuta bado mtu anakwenda kuongeza taaluma na yule ambaye hajaongeza taaluma ama mshahara aliokuwa nao kabla na aliokuwa nao baadaye unafanana. Kwa kweli hili linawavunja moyo wauguzi wetu na tusipoliangalia linaweza kupelekea rushwa ikaendelea kutokea katika maeneo ya hospitali maana siyo kwamba haipo, ipo. Tunataka Serikali kupitia Wizara ya Afya iliangalie hili jambo hususani katika maslahi ya Madaktari wetu na Wauguzi ambayo huenda ikapelekea kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichangie suala zima la usafi katika vituo vya afya na hospitali zetu. Tunaona kwamba hospitali na vituo vya afya ni sehemu za afya lakini unakuta mgonjwa anakwenda na gonjwa moja sasa hospitali inakuwa ni sehemu ya mlipuko wa magonjwa mengine kutokana uchafu au kutokuwa na usafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili napenda Serikali katika kuhitimisha leo jioni kupitia Wizara hii ituambie ina mpango gani wa kuhakikisha vituo vya afya vinakuwa safi na vinapata maji. Kwa sababu unakuta katika kituo cha afya maji hakuna, wagonjwa ni wengi na kila mmoja ana maradhi yake, unakwenda na gonjwa moja unarudi na magonjwa mengine kumi na moja. Kwa hiyo, hili nafikiri siyo lengo la vituo vya afya wala siyo lengo la hospitali hizi ambazo zinawekwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, sasa inakuwa ni kuwaangamiza badala ya kupata matibabu wanakwenda kuokota magonjwa mengine huko. Hivyo basi, nashauri Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kila kituo cha afya kinakuwa na maji ya uhakika na vilevile kinakuwa na visima. Kwa sababu unakuta kinakosa maji labda yamekwisha ama vinginevyo lakini unapokuwa na kisima unakuwa na uhakika wa kuwa vituo vipo safi na maji kupatikana katika vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nipo hapohapo kwenye vituo vya afya katika mpango mzima ambao Wizara hii inausema, ina mikakati mingi ambayo tumeiona na jitihada zake katika kuokoa maisha ya mama na mtoto. Mipango hii ni mizuri, kwa upande wake tunaweza tukasema inajaribu kujitahidi kukwamua mipango hii lakini bado Serikali hiyohiyo inakwamisha mipango ya kuokoa maisha ya mama na mtoto. Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake cha hotuba ametuelezea mikakati mizuri ambayo wanafanya ili kuokoa maisha ya mama na mtoto lakini nasikitika kwamba katika mikakati hiyo bado kuna vitu ambavyo vinakwamisha, siyo kuendeleza bali vinakwamisha na vinajulikana lakini havijaelezwa jinsi gani watavifanya ili kukwamua vifo vya mama na watoto kupitia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kukosekana kwa umeme katika vituo vya afya. Vituo hivi vinaokoa maisha ya mama na mtoto na maisha ya Watanzania, inafika kipindi mama anashindwa ku-*deliver* kwa njia ya kawaida inabidi afanyiwe upasuaji, umeme unakatwa katika kituo cha afya, sawa, wakate sehemu nyingine lakini mpaka katika vituo vya afya? Ni aibu gani ambayo inaikuta Serikali hii katika vituo hivi? Kateni umeme maeneo mengine siyo kukata umeme katika kituo cha afya ni aibu kwa Serikali kama hii, inatakiwa hili jambo iliangalie vizuri. Mnapanga mikakati mizuri, mnatumia fedha nyingi lakini kitu kidogo kinakwamsha ile mikakati haionekani umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nataka Waziri anapojibu atuhakikishie wana mpango gani ama wana kitu gani ambacho wanataka kutuambia sisi tuone kwamba katika vituo vya afya hili suala la ukatikaji wa umeme linaondoka. Maana kuondoa suala hili la ukataji wa umeme katika hivi vituo linapelekea kusitisha huduma kwa wagonjwa ambao inabidi wafanyiwe upasuaji na linapelekea pia hata kutokuwa na uhakika wa huduma katika kituo cha afya ama katika hospitali zetu. Hivyo basi, napenda Waziri atuambie katika kuhitimisha ni kitu gani ambacho wanataka watueleze ama wanafanya nini katika kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala zima la Wakunga katika hospitali zetu. Tunaona kwamba katika hospitali zetu hususani katika zahanati na hospitali nyingine, unafika hospitali unakuta Mkunga mmoja lakini wagonjwa wamekwenda wanne au watano, siyo wote watafanikiwa. Sawa mmoja atakayefika atafanikiwa kumpata yule mmoja akamsaidia wengine bado wanashindwa kuokoa maisha yao ama wanashindwa kupata matibabu kutokanana ukosefu wa Wakunga hospitalini. Siyo kwamba hakuna watu ambao wana taaluma ile mitaani na si kwamba hakuna watu ambao wana uwezo wakukaa pale na kufanya hizo kazi lakini cha kushangaza watu wengi wapo mitaani, watu wengi wana sifa za kuwa Wakunga lakini wanakosa ajira katika vituo hivi na wananchi wanapotea wanapokwenda kutafuta matibabu wanashindwa kupata matibabu yanayostahiki. Hivyo basi, naitaka Serikali kupitia Wizara hii ituambie ina mpango gani na ina utaratibu gani wa kuhakikisha kila hospitali inakuwa na Wakunga wa kutosha bila hivyo tutaendelea kupoteza malengo ambayo tunayaandika, tutakuwa tu tunayatazama kwenye makaratasi yanafanikiwa kupitia makaratasi, yanapita tu Bungeni kwa kura ya 'ndiyo' na 'hapana' na kwa wingi wa watu lakini bado wananchi wanaendelea kunyanyasika na kupata taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia na suala zima la mpango wa udhibiti wa dawa hospitalini. Kuna utaratibu wa kutolewa dawa hospitali na kuna utaratibu pia wa kupata huduma bure kwa wazee na watoto wadogo. Unakuta mgonjwa anakwenda asubuhi anakaa mpaka jioni, mzee huyo amekwenda kupata matibabu, inafika jioni anafanikiwa kumwona Daktari dawa anaambiwa akachukue dirishani, anapofika kwenye dirisha la dawa anaambiwa dawa zimekwisha. Haitokei mzee huyu ama mtoto huyu akafanikiwa kupata dawa, hizi dawa zinakwenda wapi na zinafanyiwa shughuli gani maana zipo kwa ajili yao na wao wanapokwenda wanaambiwa dawa zimekwisha ama utakuta wanaelekezwa *pharmacy* nje ya hospitali wakachukue dawa hizo. Nataka kujua hizi dawa zipo kwa ajili ya kuwasaidia hawa

wazee ama Serikali mpango wake ni kuwasaidia ama waendeee kupata taabu katika sekta hii hasa katika masuala mazima ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha jinsi gani Wizara inashindwa kudhibiti dawa kwa ajili ya wagonjwa wake. Kama ingekuwa na utaratibu na mipango mizuri ya kudhibiti dawa basi ni uhakika kwamba watoto na wazee wangekuwa wanapata dawa pale hospitali kama wanavyosema tiba ni za bure na dawa inabidi wapate pale panapostahiki kwa muda ambao unastahiki. Nasikitika kwamba Serikali katika jambo hili bado haijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Sylvestry Koka na Mheshimiwa Deo Sanga wajiandae.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu. Pia niwapongeze Madaktari, Manesi na watumishi wote wa sekta hii ya afya kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na kwamba wapo wachache ambao wanafanya ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mkoa wangu wa Kilimanjaro, hospitali ya rufaa ya *KCMC*. Bajeti iliyopita nilizungumzia ukosefu wa *CT Scan* katika hospitali yetu ya rufaa ya *KCMC* na huu ni mwaka wa nne sasa hatuna mashine hiyo. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini tunapata mashine hiyo ya *CT Scan* kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanapata adha kubwa sana kuifuata huduma hii katika Mkoa wa Arusha. Kwanza, wagonjwa wanapata usumbufu lakini pia na gharama ya kipimo hiki ni kubwa sana huko wanakoifuata. Ni kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, naiomba Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu msikie kilio hiki cha wananchi wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijatoka katika hospitali hiyo, lipo tatizo ambalo linaendelea na limeandikwa sana na vyombo vya habari lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri leo asubuhi nimeongea naye na amenihakikishia kwamba wamesimamisha jambo hilo. Jambo lenyewe ni Mwenyekiti wa *TUGHE* katika hospitali hiyo inasemekana alitoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais kuhusu utendaji au uongozi wa hospitali hiyo na Mheshimiwa Rais alipeleka maelekezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ili matatizo hayo yafanyiwe kazi. Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya akapeleka kwa uongozi *KCMC* na kumtaja mhusika kinyume na taratibu. Tulitegemea angepeleka maelekezo kujua taarifa iliyopelekwa kwa Mheshimiwa Rais ina ukweli gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa niulize uongozi, hivi ni sahihi kweli yule anayepeleka taarifa za utendaji mbovu wa eneo husika ili lifanyiwe kazi badala ya kutunziwa siri ili kuondoa matatizo kwenye maeneo au mashirika ya Serikali anashindwa kutunziwa siri na matokeo yake amechukuliwa hatua, amesimamishwa na kutaka kufukuzwa kazi, napenda Waziri atoe kauli. Serikali imeendelea kusisitiza wananchi watoe taarifa *either* kwenye vituo vya afya au maeneo yanayohusika kama TAKUKURU na maeneo mengine. Kwa utaratibu huu tunategemea kweli kupata taarifa za Watendaji wetu kwenye maeneo wanayofanya kazi? Ningependa kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na kunipa majibu kwamba wamesimamisha lakini siyo utaratibu mzuri na hatuwatendei haki watumishi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie hospitali yetu ya Mkoa ya Mawezi. Kwanza hospitali ile ni ya muda mrefu, majengo yamechakaa, madaktari hawana ofisi za kufanyia kazi, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Nimuombe Mheshimiwa Waziri

aiangalie hospitali ile. Tunahitaji majengo mapya, wagonjwa waweze kupata huduma nzuri kwani msongamano ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko jengo nalolisemea kila napopata nafasi, jengo la wazazi katika hospitali hiyo. Mheshimiwa Waziri ni kilio cha muda mrefu sana. Kazi ya kujifungua siyo rahisi, tunahitaji nafasi, eneo zuri la kujifungulia na vifaa vya kutosha. Jengo lile limechukua muda mrefu sana kukamilika, tukiuliza wanasema liko TAMISEMI, ukienda TAMISEMI wanasema liko Afya. Nawaomba TAMISEMI na Wizara ya Afya, hebu pelekeni fedha basi mmalize jengo lile la wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mawenzi ili akina mama wa Mkoa wa Kilimanjaro wapate huduma nzuri na salama pamoja na vifaa wakati wa kujifungua. *(Makofi)*

Kabla sijatoka kwenye mkoa wangu, nizungumzie suala la vituo vya wazee. Mzungumzaji mmoja hapa amevizungumzia, vituo hivi vinatia aibu na majengo yake yamechakaa. Tukumbuke kwamba wazee ni dhamana na sisi pia ni wazee watarajiwa. Kwa hiyo, tuwatendee haki wazee hawa ambao wengine hawana familia za kuwatunza lakini Serikali mnao wajibu wa kutekeleza ahadi yenu hasa ya Chama cha Mapinduzi, ambapo mlisema mtawaenzi wazee lakini bado kuna tatizo kubwa sana kwenye hivyo vituo, hakuna chakula na hawapati dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kituo cha Njolo kilichocpo Manispaa ya Moshi. Nilishasema tena hapa kwamba wana upungufu wa wafanyakazi na tatizo la usafiri. Wale ni wazee wakati mwingine wanazidiwa usiku na wengine wamefariki. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema itapeleka gari kila kituo, napenda kujua ni vituo vingapi vimeishapewa magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nyumba za watumishi ni chache na hawapewi fungu la dharura na matokeo yake wanatumia fedha zao za mifukoni. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwenye suala hili, waangalie vituo hivi vya wazee tukawatendee haki wazee wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upandaji wa vyeo na madaraja katika hospitali zetu. Liko tatizo kwa watumishi kupandishwa vyeo au kurekebishiwa mishahara yao pindi wanapokwenda kusoma. Tatizo hili liko katika Wilaya nayotoka ya Hai. Katika hospitali yetu ya Wilaya, watumishi wana malalamiko makubwa, wanasema wengi hawapati nafasi ya kwenda kusoma lakini wanaobahatika kupata nafasi hizo hawarekebishiwi mishahara yao.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, watumishi hawa wa sekta ya afya wanafanya kazi ngumu sana ya kuokoa maisha yetu. Hali hii ni pamoja na kwa Mdogo wangu Esther Matiko kule Tarime. Tunaomba sana tuwatendee haki watumishi hawa wa afya kwa sababu wanafanya kazi ya kuokoa maisha yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu matibabu kwa wazee, watoto na akina mama wajawazito. Naomba nimuambie Mheshimiwa Waziri kwamba ahadi hii haitekelezeki. Hospitali nyingi wanapokwenda wazee, akina mama wajawazito na watoto huduma hizi hazipatikani na wanadaiwa fedha. Upo ushahidi wa akina mama wajawazito waliokwenda kwa kukosa tu *gloves*, siwalaumu watumishi wa afya kwa sababu na wao wanajikinga na maradhi, wanakosa huduma ya kuzalishwa na wengine wamepoteza maisha na ushahidi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la madaktari waliomaliza mafunzo yao wanaosubiri kwenda *internship* lakini Wizara haina fedha. Hili ni jambo la aibu sana. Tunajua uhaba wa madaktari tulionao katika nchi yetu, leo Wizara inasema haina fedha, wakati tunasema tunataka kuokoa maisha ya watu wetu, toka mwaka jana. Baadhi ya wazazi

wa madaktari hao wenye fedha wamepeleka watoto wao kwa mkataba na Serikali kwamba watarejeshewa fedha.

Sasa wale ambao wanatoka kwenye familia za kimasikini watapelekwa na nani? Napenda Serikali hii iniambie ni nini hatma ya madaktari hawa? Ni lini watapewa fedha ili waweze kwenda kwenye hiyo *internship* ili tupunguze kilio cha madaktari katika hospitali zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi hii lakini naomba sana jengo la wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi, nimelisemea sana. Katika miaka yangu mitano niliyokaa hapa nimelizungumzia, naomba kauli sasa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba watalikamilisha lini ili akina mama waweze kupata eneo zuri la kujifungulia. Nimesema ni pamoja na vifaa kwa sababu juzi tulikuwa kwenye semina ya akina mama kuhusu suala la uzazi yako mambo mengi tumeelezwa ambayo yanafanyika kwenye hospitali zetu au vituo vya afya, kwamba akina mama wanapokwenda kujifungua wanaambiwa waende na ndoo ili wabebe uchafu wao waondoke nao nyumbani. Huu ni udhalilishaji wa akina mama. Tunaomba Waziri mkalifanyie kazi suala hili na kama hakuna vifaa vya kuchomea tafuteni fedha mzipeleke ili muache kuwadhalilisha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace. Sasa namuita Mheshimiwa Sylvestry Koka, Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila wajiandae.

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema machache katika Wizara yetu hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kituo chetu cha afya pale Kibaha Mjini, kwa jina maarufu Mkoani. Kituo hiki cha afya ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba kipandishwe hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya kwa maana ya kuboresha majengo pamoja na miundombinu na vifaa vya kufanyia kazi. Tangu ahadi hii imetolewa hadi leo jambo hili halijafanyika na ukizingatia tayari mji wetu wa Kibaha una wakazi zaidi ya 128,000 mbali na wengine wanaotoka maeneo mbalimbali hata Dar es Salaam kuja kupata matibabu na hususani kujifungua. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na mipango yote, tuna sababu ya kuinua hadhi ya kile kituo cha afya kuwa angalau hospitali ya Wilaya ili hospitali ya Tumbi iliyotangazwa kuwa ni hospitali ya rufaa, iweze kutumika kwa rufaa na kadri inavyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa la huduma na hususan malalamiko makubwa ni wazee. Popote utakapopita katika Majimbo yetu wazee wanalalamika sana. Tujaribu kufikiri tunao wazee wengi ambao hawana hata watoto wa kuwatunza badala yake wanatunza hata vitukuu walioachwa na wajukuu wao hasa wanapofariki kwa magonjwa na mambo mengine. Tumewaambia wanapata matibabu bure, kweli wanakwenda dirishani na nikiri wakati mwingine dirisha la wazee lipo lakini wakitoka pale hakuna dawa. Sasa matokeo yake nia nzuri ya Serikali inageuka kuwa kero. Ni vyema jambo hili lifanyiwe marekebisho ili ile kazi nzuri ambayo tayari Serikali imeishaifanya hata ya kutenga dirisha na wahudumu iweze kuleta manufaa kwa wazee hawa na iweze kuwa na tija ili Serikali iendelee kutoa huduma bora kwa wazee. Naomba nia nzuri ya Serikali ienziwe kwa kuhakikisha wazee hawa wanapata dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo katika hospitali hii hasa la wodi ya wazazi, hakuna vitanda vya kutosha, wakati mwingine wazazi wawili wanajifungulia katika kitanda kimoja na hata vifaa vya *labour* na vyenyewe ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, niiombe Serikali na Mheshimiwa

Waziri ajaribu kuangalia namna ya kusaidia kituo hiki cha afya na kukipa hadhi ya Hospitali ya Wilaya ili kiweze kutoa huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo kero nyingine hasa ya watumishi. Nitolee mfano kwenye kituo hiki, watumishi wanakaa pale hasa wale Wakunga wanaosaidia akina mama kujifungua usiku na mchana, wanafanya kazi *over time* lakini hawapati hata ile *call allowance*. Wakati mwingine hii kero inahamia kwa wagonjwa, kwa sababu watumishi wanakosa haki zao, matokeo yake hata namna wanavyopokea na kuwahudumia wale wagonjwa inakuwa si sawasawa na si kama inavyostahili kwa sababu tayari mtu anakuwa hana raha na ile kazi anayoifanya. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri ufanyike utaratibu mzuri wa kuhakikisha hawa watumishi wanapata zile stahili zao ili na wenyewe wawajibike kutoa huduma iliyo bora kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma katika hospitali na vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu hospitali ya Tumbi na umuhimu wake lakini uhakika na uhalisia ni kwamba Serikali imeitupa hospitali hii. Wote tunafahamu ndiyo hospitali pekee ambayo ina uwezo na inahudumia majeruhi wengi wanaopata ajali katika barabara hii ya Morogoro kuja mpaka Arusha na kwenda mpaka Mbeya lakini uhalisia hali ya hospitali hii ni tete. Hata pale *causality* ambapo wagonjwa wanapokelewa ili kupata msaada wa kwanza hakuna vifaa, ni vitanda tu viko pale. Hakuna hata vile vifaa muhimu ambavyo vinastahili kumpokea mgonjwa ili angalau kutambua hali aliyonayo ili Daktari aweze kuamua anakwenda kupata matibabu ya namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hakuna mashine ya kupumlia, mashine ya ku-monitor moyo *(heart monitor)* ambavyo ni vifaa muhimu vya kumfanya yule mgonjwa anayeletwa pale hasa kwa ajali aweze kujulikana yuko katika hali gani na anakwenda kupata matibabu gani. Sisi sote hata Wabunge tulioko hapa kwa maana ya safari katika barabara hii ya Morogoro, wote tu majeruhi watarajiwa kwa sababu hatujui ni lini tutapata ajali. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na Serikali watupie macho hospitali hii kwa sababu kwa kweli ni aibu. Ukipokelewa pale *causality* hakuna namna yoyote ya Daktari kutambua hali yako ya afya na hili ni jambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *ICU,* Madaktari wamejitahidi kuchukua vyumba ambavyo havikuwa kwa ajili ya *ICU*, wamejitahidi kuvibadilisha lakini tatizo kubwa hakuna vifaa. Tunahitaji mashine zaidi ya sita kwa ajili ya kusaidia *ICU* hii iweze kuhudumia wagonjwa. Matokeo yake hata mgonjwa ambaye alitakiwa apate huduma pale Tumbi analazimika kupelekwa Muhimbili. Kama tunavyofahamu foleni ya Kibaha mpaka Muhimbili, hakika mgonjwa aliyepata ajali umtoe pale mpaka Muhimbili hajapata matibabu husika, nina imani kwamba, wengi wanapoteza maisha njiani bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kama hospitali hii itapewa kipaumbele kwa kupewa vifaa na wataalam wa kutosha wagonjwa wengine maisha yao yatakuwa yanaokolewa pale kuliko kuwakimbiza Muhimbili bila sababu. Hiyo ndiyo maana halisi ya ile hospitali kutangazwa kwamba ni ya rufaa ni ili ifanye kazi za rufaa, lakini matokeo yake inafanya kazi karibu sawasawa na hospitali tu ya wilaya kwa sababu ya ukosefu wa vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa lingine lililopo ni pamoja na Madaktari. Hivi ninavyozungumza na Mheshimiwa Waziri katika hospitali kama ile hakuna hata Madaktari wa Usingizi, Madaktari wa *X-ray* na hakuna *Physician*, unaweza ukafikiri hilo. Hata Daktari wa Magonjwa ya Akili hakuna, aliyekuwepo amestaafu, basi hayupo. Sasa hebu fikiria hospitali tayari imekwishatangazwa kwamba ni ya rufaa, iko katika hali hii, tunategemea kweli ule mgawanyo wa wananchi kupata huduma karibu au katika mkoa wao inawezekana? Matokeo yake ni lazima tutaishia kurundika wagonjwa Muhimbili na kuzifanya huduma hizi kuwa duni na

matokeo yake kazi nzuri inayofanywa na Serikali inakuwa ni malalamiko kutoka kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri alikuja pale tulitembea na haya mambo tunayozungumza aliyaona kwa macho na tulikubaliana atachukua hatua mbalimbali ili kuanza kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ta Tumbi kwa ujumla wake ina upungufu wa wafanyakazi kwa maana ya Madaktari, Manesi na wengine kwa asilimia 48. Ina wafanyakazi ambao wanastahili kutoa huduma pale kwa asilimia 52 tu. Sasa utategemea kupata huduma nzuri katika hospitali kama hii? Nina imani hali hii vilevile iko katika hospitali nyingine. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tuchukue hatua ili kuboresha afya kwa sababu hakuna maisha yaliyo bora nje ya afya. Yote tunayofanya hapa na yote yanayofanyika katika nchi hii kwa wananchi wetu, jambo kubwa na la msingi ni pamoja na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe masikitiko yangu makubwa sana. Katika nia nzuri ya Serikali ya kutoa huduma bora na kuitangaza Hospitali ya Tumbi kuwa ya rufaa, kuna upanuzi uliofanyika pale ikiwa ni pamoja na kujenga jengo lingine la kisasa. Kilichofanyika jengo lile limejengwa nusu na wala halikumaliziwa vizuri. Awamu ya pili ya jengo lile imefikia hatua ya nguzo kusimamishwa, ni zaidi ya miaka sita. Toka mwaka 2010 hadi leo nguzo zimesimama na nondo zinaoza, kila kilichofanyika pale kwa fedha nyingi zilizowekwa kinaendelea kuwa ni bure. Matokeo yake Serikali inapata hasara, jengo halikamiliki na hata ile awamu ya kwanza inashindikana kutumika vizuri kwa sababu miundombinu inaambatana vilevile na hii awamu ya pili ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio yalikuwa ni takribani shilingi bilioni 18 lakini hadi leo fedha ambazo zimepatikana ni shilingi bilioni 4.7 peke yake. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwa takribani miaka sita jengo lile halijaweza kukamilika. Matokeo yake ile nusu iliyojengwa inaendelea kuharibika na nina hakika tutakapotaka kujenga tena itabidi kuvunja na kuanza upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, hapa tunapoteza fedha. Kama Serikali imekwishawekeza fedha hizi na jengo hili halijaweza kutumika, nimuombe Mheshimiwa Waziri achukue hatua za dharura kuhakikisha fedha hizi haziendelei kukaa bure na ahakikishe kwamba, hata fedha zilizowekezwa hapa jengo hili haliendelei kuoza na kuleta hasara kwa Serikali na wakati wananchi wanahitaji kuhudumiwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazame afya kwa ujumla wake…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, muda umeisha.

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Namuita Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kushiriki kuchangia juu ya Wizara hii ya Afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, samahani, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpishe Mheshimiwa Naibu Spika aweze kuja kuchukua nafasi hii. Mheshimiwa Deo Sanga, usichangie Mheshimiwa Naibu Spika anakuja.

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuchukua nafasi hii kuwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo limepata msiba wa kufiwa na Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Mheshimiwa Eugine Mwaiposa ambaye amefariki nyumbani kwake hapa Mjini Dodoma akiwa amelala usiku wa kuamkia leo tarehe 2 Juni, 2015. Marehemu alikuwa na tatizo la shinikizo la damu kwa muda mrefu. Mwili wa marehemu umepelekwa kuhifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa uchunguzi zaidi wa kitaalam. Taarifa nyingine tutazisambaza baadaye kwa kupitia njia ya mtandao.

Waheshimiwa Wabunge, nyumbani kwa marehemu ni eneo la Chadulu, *opposite* na jengo jipya la hoteli ya Shabiby, barabara ya Dar es Salaam. Shughuli ya kuaga itafanyika kesho baada ya familia yake kuwasili hapa Dodoma.

Nitawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane mara moja baada ya kuahirisha kikao hiki katika ukumbi wa mikutano wa Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tutatumia mtandao wa simu kuwajulisha kuhusu ratiba na taratibu za kuuaga mwili wa marehemu. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu, amina.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, natumia Kanuni ya 152 kuahirisha Bunge hadi kesho kutwa siku ya Alhamisi, tarehe 4 Juni, 2015, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Juni, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*